SUPA JACKPOT
TZS.1,051,207,683
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**WAKULIMA** wahofia usalama kwa madai wafugaji kuwavamia




UKURASA 13

Alhamisi Novemba 17, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581132

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Mhasibu mbaroni akidai kutekwa, kuporwa mil. 60/-



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, akionyesha fedha Sh. milioni 60 kwa waandishi wa habari jijini humo jana, ambazo Mhasibu wa Kampuni ya Wachina ya Your Home Choice, alidai ameporwa na majambazi na kutoa taarifa ya uongo katika vituo vya polisi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

**ABANWA** hatimaye kuonyesha ziliko, mwingine akamatwa kujifanya askari *Endelea ukurasa 2*

## Mfugaji matatani kumtishia maisha DC

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimkabidhi Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, nakala ya sera ya ubia ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) baada ya kuizindua jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala. **PICHA: OWM**

UKURASA WA 2

### MAAGIZO 10 KUKABILI UHABA WA MAJI NCHINI

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa maagizo kumi kwa wizara za kisekta nchini kukabiliana na tatizo la maji ikiwamo wananchi waliovamia vyanzo...



UKURASA WA 4

### BIL. 1.1/- ZA HALMASHAURI ZAINGIA MIFUKO YA WAJANJA

HALMASHAURI saba za Mkoa wa Singida zimekusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.107 lakini fedha hizo hazikuingizwa benki badala yake zimefujwa kwa kuingia kwenye mifuko ya watu...

UKURASA WA 5

### RIPOTI YA NIPASHE MONDULI YAZAA MATUNDA

SERIKALI imesema inakamilisha utaratibu wa kumtafuta mkandarasi ili kuhakikisha maji yanafika wilayani Monduli.
Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alitoa kauli hiyo jana wakati akizindua rasmi kampeni ya kitaifa...

## Sera ubia ya NHC kubadilisha mandhari miji, majiji

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA, SINGIDA BIG STARS MECHI KIWANGO UK. 32

**KATUNI** UK. 6

# Mhasibu mbaroni madai kutekwa, kuporwa mil. 60/-

**Na Maulid Mmbaga**

MHASIBU wa Kampuni ya Your Home Choice ya Keko, Dar es Salaam, Deodatus Luhela (35), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kutoa taarifa za uongo kuwa ametekwa na kujeruhiwa na majambazi kisha kuporwa Sh. milioni 60 za mwajiri wake.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi (ACP) Jumanne Muliro, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa mtuhumiwa alitoa taarifa kituo kidogo cha polisi cha Gongo la Mboto na baadaye kufungua jalada katika Kituo cha Polisi Chang'ombe akidai kufanyiwa kitendo hicho.

Muliro alisema Novemba 14, mwaka huu, mtuhumiwa huyo katika taarifa alizotoa polisi, alidai kuwa majambazi walimjeruhi na kumpora Sh. milioni 60 alizokuwa ametumwa na mwajiri wake kuzichukua katika benki ya CRDB tawi la TAZARA.

Alisema Luhela alidai kuwa siku hiyo, saa 3:30 asubuhi, alikamatwa na majambazi wawili waliokuwa na gari jeusi baada ya kumtishia kwa silaha na baadaye akaingizwa kwenye gari.

Kwa mujibu wa Muliro, mtuhumiwa alidai kuwa majambazi hao walimjeruhi mkono wa kushoto na shavuni na hatimaye kumpora fedha zote alizokuwa nazo.

"Alidai kuwa baada ya tukio hilo alitupwa maeneo ya Gongo la Mboto njia panda ya Pugu na Mbezi, akajikongoja hadi kituo cha Polisi ambako alipewa PF. 3 (Fomu namba tatu ya polisi) kwa ajili ya matibabu. Baadaye mtuhumiwa huyo alifungua kesi ya unyang'anyi na kuporwa Sh. milioni 60 katika kituo cha Polisi Chang'ombe," alisema Muliro.

Baada ya taarifa hizo, Muliro alisema polisi walimhoji kwa kina na kubaini kuwa taarifa hizo zilikuwa za uongo.

Alisema ilipofika Novemba 15, saa 8:00 mchana, mtuhumiwa aliwaongoza askari hadi Chanika Kitunguu, jijini Dar es Salaam, alikokuwa ameficha fedha hizo.

**POLISI FEKI MBARONI**

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi Kanda maalum ya Dar es Salaam, limamshikilia Joseph James (32) mkazi wa Kijitonyama, Dar es Salaam, kwa kujifanya askari polisi kutoka makao makuu ya upelelezi, Dodoma.

Kamanda Muliro alisema James amekamatwa baada ya ufuatiliaji kutokana na taarifa za kuwapo kundi la watu wanaojifanya polisi na kuwanyanyasa watu pamoja na kuwatishia kwa tuhuma mbalimbali za uongo.

"Uchunguzi umebaini mtuhumiwa huyu amekuwa akishirikiana na wenzake ambao wamekuwa wakitumia gari aina ya Subaru lenye namba za usajili T 550 DST alilokamatwa nalo," alisema Muliro. Kamanda alibainisha kuwa jeshi linawafuatilia watu wengine waliokuwa wakishirikiana naye wakijifanya askari polisi na maofisa wa usalama wa taifa ambao hukamata watu ovyo, kuzunguka nao mitaani kwa kutumia gari huku wakiwatishia kuwa watafikishwa katika vyombo vya dola na baadaye kuwataka watoe pesa ndipo wawaachie.

"Jeshi la Polisi halikubaliani na hali hiyo. Ulinzi na ufuatiliaji wa mambo mbalimbali upo katika kiwango cha juu na yeyote atakayejihusisha na vitendo vya kihalifu atakamatwa, atahojiwa kwa kina na baadaye atafikishwa kwenye vyombo vya sheria," alisisitiza.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (wa pili kushoto), akizindua kampeni ya kitaifa ya upandaji miti rafiki wa mazingira kwenye vyanzo vya maji katika Jiji la Mbeya jana. Kushoto ni Spika wa Bunge na Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Maagizo 10 kukabili uhaba wa maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa maagizo kumi kwa wizara za kisekta nchini kukabiliana na tatizo la maji ikiwemo wananchi waliovamia vyanzo vya maji kuondoka. Pia ameagiza kushushwa bei gesi za nyumbani ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Dk. Mpango alitoa maagizo hayo jana kwenye Mkutano wa Nane wa Bodi ya Mabonde ya Maji nchini unaofanyika jijini hapa.

Katika agizo la kwanza, aliitaka Wizara ya Maji kutekeleza miradi ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ambayo yatatumika kwa ajili ya mifugo na wananchi.

Pia alisema viongozi wa serikali wanapaswa kutoa agizo mara moja la wananchi kuondoka kwenye vyanzo vya maji pamoja na waliovamia safu za milima ya Uluguru huku serikali ikiwatafutia maeneo mengine ya makazi.

Dk. Mpango pia alisisitiza wakuu wa mikoa yote nchini kuzindua programu ya upandaji miti ili kuwa na utunzaji endelevu wa vyanzo vya maji kwa ustawi na ukuaji wa uchumi.

"Mkutano huu ni muhimu kwa ajili ya kizazi chetu na kijacho kwani tunajadili usalama wa maisha yetu. Hali ni mbaya, hivyo jitihada za makusudi zinahitajika kunusuru vyanzo vya maji ambavyo kwa kiasi kikubwa vimeharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu" alisema Dk. Mpango.

Aidha, aliagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuandaa miche ya kutosha na kugawa kwa kila mikoa kupanda miti rafiki kwa maji kwa kushirikiana na wananchi kutambua miti yote ya kienyeji na kutengeneza vitalu vyake.

Pia aliagiza kamati za ulinzi na usalama kwa kushirikiana na wizara za kisekta, kuwachukulia hatua waliohusika na uchepushaji wa maji ya mito na mifereji ambayo inapeleka maji kwenye Mto Ruaha ambao unategemewa kwa kiasi kikubwa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kunusuru Mto Ruaha Mkuu kuwa na maji mengi kama ilivyokuwa awali. Aliitaja mito hiyo kuwa ni Kimani, Chimala na Ruaha Mdogo ambayo yote inapatikana wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya.

Sambamba na hilo, aliitaka Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, kushusha bei ya gesi za majumbani huku akiweka bayana kwamba hatua hiyo itasaidia wananchi kuondokana na matumizi ya mkaa ambayo yanachangia uharibifu wa mazingira.

# Mfugaji matatani kumtishia maisha DC

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Zaynab Telack, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani Lindi, kumkamata na kumfikisha mahakamani mfugaji anayedaiwa kumtishia maisha, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Zainabu Kawawa ili kujibu tuhuma zinazomkabili za kutishia kumuua kiongozi wa serikali.

Alitoa agizo hilo baada ya Kawawa kudai kwenye kikao cha viongozi na wafugaji, kuwa mmoja wa wafugaji amemtishia maisha baada ya kumhoji kama ameingiza mifugo wilayani humo kihalali.

Akitoa agizo hilo kwa polisi, Telak alisema haiwezekani kusikia kiongozi wa serikali aliyepewa dhamana ya kuongoza watu Kilwa, akitishiwa usalama wa maisha yake, huku yeye akiendelea kunyamaza bila ya kuchukua hatua za kisheria.

"Huyu ni kiongozi aliyepewa kazi ya kumsaidia Rais wa Tanzania kwenye wilaya, iweje anatishiwa usalama wake wa maisha tuendelee kukaa kimya, haiwezekani," alisema Telak.

Alisema mtu au kikundi cha watu wasiotaka kutii na kuheshimu wenzao wakiwamo viongozi wa serikali mkoani Lindi, hawawezi kuachwa waendelee kutamba bila kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikisha mahakamani.

"Ninakuagiza RPC hakikisha huyu mfugaji anakamatwa na kumfikishwa mahakamani kujibu shtaka linalomkabili," alisisitiza Telak.

Alisema, amepewa dhamana ya kumsaidia rais, hawezi kukubali kuona wananchi na watumishi wa umma wanaonewa na wachache bila sababu za msingi.

Awali, Kawawa alisema siku moja akiwa katika ziara zake za kikazi vijijini, alifika eneo la Zingakibao na kukuta kundi kubwa la mifugo, hali iliyomshangaza na kutaka kufahamu uhalali wa mifugo hiyo.

Alisema alipouliza namna ya mifugo hiyo ilivyoingia ndani ya Wilaya ya Kilwa alijikuta akikumbana na vitisho vya kutaka kumuua kutoka kwa mfugaji huyo kama angeendelea kuhoji.

Kawawa alidai kuwa alimwelekeza dereva wake kuendelea na safari ya kuelekea ofisini kwake.

Mkuu huyo wa wilaya alisema hadi sasa zaidi ya watu 15 wamepoteza maisha kutokana na mapigano kati ya wafugaji na wakulima, tangu serikali iruhusu wafugaji kutoka Ihefu Mbeya kwenda mikoa ya Kusini.

HABARI KITAIFA

# Wakulima wahofia usalama madai wafugaji kuwavamia

Na Halfani Chusi

WAKULIMA wa Ruvu eneo la Minazi Mikinda wilayani Kibaha, mkoani Pwani, wamedai maisha yao yapo hatarini kutokana na mgogoro dhidi ya wafugaji jamii ya Wasukuma waliovamia maeneo hayo.

Wakulima hao kwa nyakati tofauti wakiongea na mwandishi wa gazeti hili, walidai kuwapo ugomvi mkubwa kati ya wakulima na wafugaji, hali iliyosababisha baadhi yao kuvunjwa mikono na miguu huku wengine wakipigwa hadi kukimbizwa hospitali. Walidai, wafugaji hao huingiza mifugo kwenye mashamba yao kinyume na sheria na wanawafanyia hivyo mara kwa mara.

Mmoja wa wakulima katika eneo hilo, Meshack Samson, alisema alikuwa na shamba kubwa alilopanda bamia ambalo limeharibiwa lote na mifugo hiyo na kumsababishia kuyumba kiuchumi. "Nilikuwa nina shamba kubwa nililopanda bamia na zilikuwa zimestawi sana ndio nilikuwa nategemea kwa ajili ya kuuza na kupata chochote kitu, wakaja Wasukuma na mifugo yao wakaingiza humu wakaanza kulisha, shamba lote likateketezwa sasa hivi nimebaki nalia njaa tu sina njia nyingine tena ya kuingiza kipato," alilalamika.

Alisema shamba hilo alilitegemea kwa kuwa akienda kuchuma na kuziuza bamia zake hakosi Sh. 10,000 kwa siku zinazomwezesha yeye na familia yake kupata chakula na watoto kwenda shule.

"Nilipowafuata kuwakataza wasiendelee kulisha mifugo yao kwenye shamba langu walianza kunishambulia kwa kunipiga mpaka wakanivunja mkono, kwa hiyo hapa nilipo mkono mmoja haufanyi kazi nauguza jeraha," alisimulia mkulima huyo. Abeid Ally, alisema shamba lake hawakufanikiwa kulivamia, lakini alipojaribu kuwazuia walimshambulia na kumuumiza miguu ambayo anaiuguza hadi sasa.

"Mimi walitaka kuja kulisha shambani kwangu kwa bahati nzuri siku hiyo walinikuta, tukaanza zogo wao wanataka kuingiza mifugo shambani kwangu mimi natetea baada ya kuona wameshindwa, wakaanza kunishambulia kwa marungu, fimbo wakanipiga miguu mpaka leo nimepata ulemavu siwezi tena kutembea kama zamani na bado naendelea kutumia gharama kutibu jeraha langu," alisimulia.

Mkulima aliyepasuliwa mkono, Husein Mfaume, alisema alipoona ng'ombe wanavamia shambani kwake aliomba wanajeshi wamsaidie kuwapeleka kituo cha polisi baadaye wafugaji walimfuata na kumvunja mkono.

"Nilipoona ng'ombe wanaingia shambani kwangu nikaomba msaada kwa wanajeshi kwaajili ya kunisaidia kuwakamata na kuwapeleka polisi, kumbe wale Wasukuma waliikariri sura yangu baadaye baada ya kutoka kituo cha polisi pale Mlandizi, walinifuata na kuanza kunipiga mpaka wakanivunja mkono kwa sababu tu nimewapeleka polisi."

"Kwa sasa hali ni mbaya sana huku kuna vita kubwa kati ya wakulima na wafugaji kila siku kuna matukio ya ajabu sana yanatokea huku," alisema Mfaume.

**KAULI YA DIWANI**

Diwani wa kata hiyo, alipopigiwa simu na Nipashe kuzungumzia malalamiko hayo, alikiri kuwapo kwa mgogoro huo huku akibainisha hatua kadhaa zilizochukuliwa kukabili madhila hayo.

"Huu mgogoro ni sugu ni wa muda mrefu ni janga la kitaifa kati ya wakulima na wafugaji ni vita kabisa huku kuna mchanganyiko kati ya wafugaji wa jamii ya Kimasai na Wasukuma. Hawa wasukuma ndio wanashida sana wao hawaangalii shamba la mtu wanachojali mifugo yao ile ishibe, kwa hiyo wanaingiza mifugo yao usiku wanavizia wakulima wamerudi nyumbani kupumzika." Alisema, mkulima anaamka asubuhi kwenda shambani anakuta shamba jeupe, ng'ombe wameshalipitia hakuna kitu chochote. "Kwa mfano huku wakulima wanategemea sana bamia sasa mtu ameshachuma mara ya kwanza anategemea akae wiki akachume tena halafu linatokea hilo unafikiri inakuwaje?"

"Tumejaribu kutoa taarifa kwa polisi, lakini wanatujibu kuwa sisi ndio tuwakamate tuwapeleke polisi, lakini shida inayokuja wale wanavamia na silaha, mkulima hawezi kupambana na mfugaji anayeenda na silaha."Alisema alitoa taarifa kwa Jeshi la Polisi na kwa Mkuu wa wilaya, zikaundwa kamati za watu watano, watano kutoka pande zote mbili ili inapotokea shida wakae kuitatua.

**MKUU WA WILAYA**

Akiongea kwa njia ya simu, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, alikanusha kuwapo malalamiko hayo ofisini kwake.

"Mimi hizo taarifa sina hawajafika katika ofisi yangu kutoa malalamiko wanatakiwa kufika ofisi za serikali kutoa malalamiko, waambie walete malalamiko yao na sisi tutashughulikia," alisema Sara.



Mkulima Hussein Mfaume, akionyesha mkono kwa mwandishi wa gazeti hili juzi, aliojeruhiwa na wafugaji wa jamii ya Kisukuma alipokuwa akijaribu kuwazuia wasiingize mifugo kwenye shamba lake eneo la Minazi Mikinda, wilayani Kibaha, mkoani Pwani. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Sera ubia NHC kubadilisha mandhari miji, majiji

Na Romana Mallya

SERA ya ubia kati ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), wawekezaji na sekta binafsi iliyozinduliwa jana, inatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya makazi ikiwamo kubadilisha mandhari katika majiji na miji mikubwa nchini.

Katika uzinduzi huo uliohudhuriwa na wawekezaji katika sekta ya makazi na mabalozi wanaowakilisha nchi zao Tanzania, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema ni matumaini yake baada ya kuzinduliwa, shirika litachambua aina ya wawekezaji ambao wataleta maombi ya ujenzi wa nyumba ambao hawataishia njiani.

"Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Jerry Silaa, ameshauri NHC katika mipango ya ujenzi, iangalie maegesho ya magari hasa kwenye majiji.

"Jiji limejaa nyumba maeneo yote, uegeshaji umekuwa wa shida, kwa hiyo kupitia mpango huu wa ujenzi msisahau kuweka maeneo haya ili wale wanaoishi maeneo jirani au walioamua kuishi kuanzia ghorofa ya sita, wapate mahali pa kuegesha magari yao.

"Hali ya hewa mfano Dar es Salaam ni joto. Watu badala ya kutegemea viyoyozi ndani ya nyumba zao, wanataka kuwe na sehemu ya kupata hewa safi. Ni jukumu la shirika wakati mwingine kwenye majengo ambayo mmeamua kujenga muyabomoe watu wapate kitalu cha kupumzika, kama miji mingine wanavyofanya," alisema.

Majaliwa alisema utekelezaji wa ujenzi wa nyumba katika miji na majiji unapaswa kujumuisha maegesho ya magari, sehemu za kupumzikia na burudani na kwamba kwa kufanya hivyo, itakuwa fahari kubwa kwa sababu hakutakuwa na shida ya ofisi, nyumba za biashara na za kuishi. Pia alisema thamani ya ardhi kila mwaka itaongezeka.

Sambamba na hilo alisema mpango huo utapunguza tatizo la nyumba huku akibainisha kuwa: "Takwimu zilizopo zinaonyesha taifa lina uhaba wa zaidi ya nyumba milioni tatu na mahitaji yanaongezeka kwa wastani wa nyumba 200,000 kila mwaka.

"Upungufu huo wa nyumba unachangia wamiliki binafsi wa nyumba kutoza kodi kubwa na wakati mwingine kudai kodi ya mwaka mzima. Lengo la NHC ni kujenga nyumba nyingi kwa mahitaji ya wananchi."

Pia alisema uamuzi wa kushirikisha sekta binafsi ni sahihi na unatoa fursa kwa wafanyabiashara mmoja, kuwekeza sekta ya nyumba.

"Ninatoa wito kwa wawekezaji na mabalozi mnaowakilisha nchi zetu Tanzania, kuwaita wawekezaji wenu kwamba milango ya uwekezaji sekta ya nyumba imefunguliwa rasmi ili malengo yafikiwe" alisisitiza. Kwa mujibu wa Majaliwa, kwa kipindi cha takribani miongo mitatu iliyopita, tangu kutungwa Sera ya Ardhi ya mwaka 1995, kumekuwa na mapinduzi makubwa katika ardhi na kuipa thamani, hivyo kufanya mijini na vijijini kuwa na mabadiliko makubwa.

Alisema nyumba 25,239 zimejengwa na takriban asilimia 97 ya nyumba nchini, zimejengwa na watu binafsi tofauti na maeneo mengine.

Pia alisema kumekuwa na mikopo iliyotolewa kwa ajili ya uendelezaji milki ikiwamo mikopo ya nyumba, akibainisha kuwa hadi Septemba, mwaka huu, taasisi za fedha 33 zimetoa mikopo ya nyumba yenye jumla ya Sh. bilioni 147.7 kwa wananchi 6,177, hivyo kuongeza mchango wa sekta milki.

Kuhusu kampeni ya 'Pendezesha Jiji' inayohamasishwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, Majaliwa alilitaka shirika kuangalia nyumba ambazo hazijafikiwa na wawekezaji ili zipakwe rangi.

"Nyumba zimechakaa ziboreshwe, usafi uzingatiwe ili jiji liwe zuri zaidi. Watanzania tumieni fursa za mikopo ya kibenki kuwekeza kwenye majengo. Kwa mujibu wa hesabu za Mkurugenzi Mkuu wa NHC (Nehemiah Mchechu), uwekezaji huu unalipa.

"Uamuzi huu unakwenda kuongeza idadi ya nyumba na kupunguza pengo la uhaba wa nyumba tulizo nazo. Wenyeviti wa kamati za bunge walivyokuja hapa, wamesema mambo mbalimbali.

"Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii, Ally Makoa, amesisitiza usimamizi wa miradi hii ambayo leo (jana) tunaizindua kwa sera yake, kuhakikisha inanufaisha Watanzania na NHC," alisema.

Majaliwa alisema anaungana na Makoa kusisitiza kuwa serikali itakuwa karibu ili mkakati huo uwe na tija na hauletwi ili kuangamiza wawekezaji bali kuwapatia faida.

"Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, amesisitiza miradi iwe na thamani ya fedha. Nisisitize kuwa hili ni jambo muhimu kuepusha kuporomoka kwa majengo yatakayojengwa na kuleta madhara na kuepusha serikali isipate hasara baada ya miaka kadhaa," alisema.

Mkurugenzi Mkuu NHC, Mchechu alisema sera ina vipengele tofauti, wakati wa ujenzi inategemea watajenga ndani ya mwaka au miaka miwili.

"Katika uwekezaji sera ya kutoa ardhi kama mtaji, mtu ana uamuzi wa kuchukua kipengele cha miaka 15 ambacho kitamuacha na umiliki wa asilimia 40 za umiliki ardhi au kipengele cha miaka 25 ambacho kitamuacha na umiliki wa asilimia 25.

"Sera ya pili inayotoa ardhi na mtaji, watakachokubaliana ni kwa maisha, sera ya tatu ya ujenzi wa kugawana faida, wanategemea ndani ya miaka mitano wamemaliza mradi na wamegawana na nyumba wamewaachia wananchi na nyingine ni ya miaka 10 mpaka 30," alisema.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema miradi ya ubia ilikuwa ikikwamishwa na utoaji wa hati na tayari suala hilo limeshughulikiwa kwa kuanzisha dawati maalum.

# Bil. 1.1/- za halmashauri zaingia mifuko ya wajanja

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

HALMASHAURI saba za Mkoa wa Singida zimekusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.107 lakini fedha hizo hazikuingizwa benki badala yake zimefujwa kwa kuingia kwenye mifuko ya watu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema hayo jana kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ambacho kiliwashirikisha wakuu wa wilaya, wakurugenzi na wenyeviti wa halmashauri, wabunge, wakuu wa taasisi na viongozi wa dini.

Alitoa mchanganuo kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ndiyo inaongoza kwa kukusanya Sh. milioni 376 ikifuatiwa na Halmashauri ya Itigi Sh. milioni 330 na Halmashauri ya Wilaya Manyoni Sh. milioni 232 lakini fedha zote hizo, baada ya kukusanywa ziliingia mifukoni mwa watu.

Serukamba alisema Manispaa ya Singida ilikusanya Sh. milioni 73, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Sh. milioni 60, Halmashauri ya Wilaya ya Singida Sh. milioni 31 na Mkalama Sh. milioni 5 lakini baada ya kukusanywa hazikupelekwa benki. Kutokana na hali hiyo, aliagiza viongozi wa wilaya kwa kushirikiana na kamati za ulinzi na usalama za wilaya na mkoa kuhakikisha wanasaidia katika suala la ukusanyaji wa mapato.

"Tuko dhaifu sana katika ukusanyaji wa mapato. Viongozi tusisubiri kutibu mgongwa aliyeumwa badala yake tuzuie. Fedha hizi zilizokusanywa zirejeshwe," alisema. Kwa mujibu wa Serukamba, halmashauri zikikusanya fedha nyingi itasaidia kutekeleza miradi mingi ya maendeleo kwa kuwa serikali kuu inajitahidi kutoa fedha nyingi kwenye halmashauri lakini hiyo isiwe sababu ya kutokusanya mapato ya kutosha katika vyanzo vya ndani.

"Wakurugenzi hivi sasa hawahangaiki kukusanya mapato kwa sababu serikali kuu inatoa fedha nyingi. Hii isiwe sababu, nawaombeni tujitahidi kukusanywa mapato ya kutosha," alisema.

Serukamba aliongeza kuwa madiwani wana nafasi kubwa ya kuongeza mapato kwenye halmashauri zao kwa sababu wao wanaishi na watu huko kwenye kata ambako mapato yanapatikana.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Elia Digha, alisema vyombo vya ulinzi na usalama visaidie katika suala la ukusanyaji wa mapato kwa kuwa kuna utoroshaji mkubwa unaofanywa.

Digha alisema ukusanyaji wa mapato ya ndani umekuwa na changamoto sana kwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara wanatoroka kutolipa mapato kwenye halmashauri, hivyo kunahitajika nguvu zaidi ili kuziba mianya hiyo.

Awali, Kaimu Katibu Tawala Msaidizi, Mipango na Uratibu, Beatrice Mwinuka, akitoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya 2021/22, alisema katika kipindi hicho mamlaka ya serikali za mitaa zilikadiriwa kukusanya Sh. bilioni 15.6.

Mwinuka alisema hadi kufikia Juni, mwaka huu, zilikuwa zimekusanywa Sh. bilioni 13.6 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato sawa na asilimia 88.

# TRA yabadili 'gia angani' ukusanyaji mapato

**Na Joseph Mwendapole**

NI sawa na kubadili gia angani. Hivi ndivyo inavyoonekana baada ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuachana na mfumo wa kukusanya mapato kwa kutumia nguvu na vikosi kazi.

Matumizi ya nguvu, vikiwamo vikosi kazi vyenye silaha na mitutu ndivyo vilikuwa vimezoeleka katika maeneo mbalimbali huku maofisa na askari wakipita kudai kodi kwa wafanyabiashara. Hatua hiyo sasa haipo tena ndiyo maana inaonekana kama kubadili gia angani.

TRA imesema kwa sasa imeondoa vikosi kazi vilivyokuwa vikitumika kudai kodi na kuwaagiza maofisa wake nchini kote, kuachana na tabia ya matumizi ya mabavu. Pia imewataka maofisa hao kutengeneza mazingira rafiki yatakayowezesha wafanyabiashara kulipa kodi kwa amani huku mazungumzo kwa wale wenye malimbikizo yakitawala zaidi.

Mwenyekiti wa Bodi ya TRA, Uledi Mussa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza kwenye kikao kazi na wajumbe wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

Alisema pamoja na kuacha kutumia mabavu kwenye ukusanyaji, mapato yamekuwa yakiongezeka na kwa Septemba, mwaka huu, TRA ilikusanya trilioni 2.3 na kuvuka lengo la Sh. trilioni 2.2.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliwaambia TRA wajenge utamaduni wa kukusanya mapato ya serikali bila kutumia mabavu ndiyo maana mamlaka hiyo imewaelekeza maofisa wake nchi nzima wafanye majadiliano zaidi kuliko nguvu.

"Hatuna tena vikosi kazi (task force). Tunataka walipakodi wajisikie huru kabisa. Tukae nao kwenye matatizo na tukubaliane jinsi gani watalipa malimbikizo yao ya kodi bila kuathiri shughuli zao za kiuchumi," alisema.

"Hivi umeshawahi kumkuta mfugaji anamchinja kuku anayetaga mayai au anayeatamia au anayetunza vifaranga? Mimi sijawahi kuona hata ikiwa sikukuu mtu kuchinja mbuzi anayenyonyesha. Kwa hiyo walipakodi tunawaangalia kwa macho mawili," alisema.

Uledi alisema makusanyo yanaendelea kuongezeka na yanaonyesha dalili nzuri siku za usoni kwa kuwa mapato hayo yamepatikana kukiwa bado na madhara yaliyosababishwa na hali mbaya ya vita vya Ukraine na Russia pamoja na UVIKO - 19.

Alisema kuwapo kwa vita hivyo na ugonjwa huo, kuliathiri kwa kiwango kikubwa uchumi wa dunia, Tanzania ikiwamo. Alisema pamoja na mazingira hayo magumu, taifa limeendelea kushirikiana na wananchi wake kukusanya mapato. "Ndiyo sababu tumeona kwa nini tusiwashukuru walipakodi waadilifu wa taifa letu. Kwa nini tusiwashukuru wahariri na waandishi wa habari, makundi ambayo tumekuwa tukishirikiana nayo kwenye ukusanyaji mapato," alisema Uledi.

Alisema iwapo TRA itashindwa kuwashukuru wanaolipa kodi kwa hiari, itakuwa imekosa fadhila na aliahidi kwamba wataendeleza ushirikiano uliopo kwa waandishi wa habari, wahariri na wananchi ambao ni walipakodi wazuri.

Uledi alisema kilele cha wiki ya shukrani kwa wateja kitakuwa leo kwa kutoa tuzo kwa wafanyabiashara mbalimbali ambao ni walipakodi wazuri kama motisha ya kuendelea kulipa kodi kwa hiari.

"Kuna rafiki yangu alikuwa ananitania akasema hao watu watakaopewa tuzo za walipakodi bora kwa nini wakienda makanisani na misikitini wasikae viti vya mbele wakati wa sala. Nikacheka sana nikasema usinigombanishe na viongozi wa dini lakini alikuwa na maana sana kwa sababu kitendo cha kulipa kodi bila shuruti ni uzalendo wa hali ya juu sana," alisema.



Mhitimu wa Shahada ya Kwanza ya Mawasiliano ya Umma katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Dar es Salaam ambaye ni Mwandishi wa Habari wa gazeti la Nipashe, Beatrice Moses (kushoto), akiwa na wahitimu wenzake katika mahafali ya 16 ya chuo hicho, mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi Pwani wasalimisha silaha 111

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi mkoani Pwani, limekusanya silaha 111 zilizosalimishwa na wananchi wakati wa ziara ya kamanda wa mkoa huo iliyohusu kampeni ya kusalimisha silaha.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alisema silaha zilizokusanywa ni kutoka Wilaya za Chalinze, Kibaha, Kisarawe, Mlandizi na Bagamoyo.

Alitaja mchanganuo kiwilaya na idadi ya silaha kwenye mabano kuwa ni Chalinze (70), Mlandizi (19), Bagamoyo (13), Kisarawe (4) na Kibaha (3). Alisema silaha zilizosalimishwa na aina yake kwenye mabano ni shotgun (7), riffle (2) na bastola (1) zilizosalimishwa baada ya wananchi kuelimishwa kuhusu notisi ya msamaha kwa wamiliki wa silaha kinyume na sheria ya mwaka 2022.

"Silaha zilizotakiwa kusalimishwa ni ndogo na nyepesi hata hivyo wananchi walipewa ufafanuzi na kusalimisha silaha zilizoachwa na ndugu baada ya kufariki au kuondoka," alisema na kuongeza:

"Silaha zisizo na taarifa au kibali, iliyowahi kumilikiwa kihalalali lakini imepoteza uhalali kisheria na iliyookotwa au kutelekezwa pasipo taarifa."

Kamanda alisema, baada ya kumaliza kazi hiyo hatua inayofuata ni kukamata wanaomiliki silaha kinyume cha taratibu.

# Ripoti ya Nipashe Monduli yazaa matunda

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema inakamilisha utaratibu wa kumtafuta mkandarasi ili kuhakikisha maji yanafika wilayani Monduli.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alitoa kauli hiyo jana wakati akizindua rasmi kampeni ya kitaifa ya upandaji miti rafiki kwenye vyanzo vya maji iliofanyika jijini Mbeya, mgeni rasmi akiwa Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango.

"Mkoa wa Arusha tunatekeleza mradi mkubwa wa maji ambao ukikamilika tutakuwa tumetatua tatizo la maji katika mkoa huo, mradi huu ukikamailika utakuwa unazalisha lita milioni 200 kwa siku," alisema Aweso.

"Mkandarasi tutampata hivi karibuni kuhakikisha maji yanafika Monduli."

Kauli hiyo ya Aweso ya mikakati ya wizara yake kufikisha maji katika Wilaya ya Monduli imekuja baada ya mwishoni mwa mwezi Oktoba na Novemba mosi, mwaka huu, gazeti la Nipashe kuchapisha ripoti maalumu iliyoelezea jinsi wakazi wa wilaya hiyo hususani katika vijiji vinane vya kata za Repurko na Sepeko wanavyotumia maji yaliyochanganyika na tope.

Wananchi katika eneo hilo walisema wanalazimika kutumia maji hayo ambayo pamoja na kutokuwa safi na salama kwa afya zao, pia wanachangia na mifugo ambayo hata hivyo upatikanaji wake ni shida kwa kuchimba mashimo pembezoni mwa bwawa pekee la Nanja ambalo limebaki baada ya vyanzo vingine kukauka kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.Walisema wanapochimba mashimo hayo ni kwa ajili ya kutegesha maji kutoka katika bwawa hilo na huyasubiri mpaka siku inayofuata ndipo wachote yakiwa wamechanganyika na tope zito na kulazimika kutumia majivu kulichuja.

Aidha, alipoulizwa Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Dharura, Deus Katapondya, alisema majivu husaidia kuchuja taka kwenye maji, lakini si kuua wadudu na kwamba hayana madhara kiafya kwa sababu yana madini ya kawaida.

"Majivu husaidia kuchuja na hayana madhara kwa binadamu isipokuwa huwezi kuyatumia yakusaidie kuua wadudu kwenye maji au kukuhakikisha usalama wake hasa kwa kutumia katika hizo njia za kiasili ambazo wanatumia wanavijiji wa Monduli," alisema Katapondya.

Ripoti hiyo maalumu ya Nipashe ilionyesha madhira wanayopitia wakazi wa Monduli ya adha ya maji, na kuchapishwa kwa siku mbili mfululizo, Oktoba 31 na Novemba mosi, mwaka huu.

# Fedha za mabadiliko tabianchi kurudisha uhalisia wa Tanzania

**Na Jenifer Gilla,** MISRI

NAIBU Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Khamis Hamza Khamis, amesema fedha zitakazopatikana kupitia mfuko wa kusaidia majanga yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabianchi, zitasaidia kurudisha uhalisia kwenye maeneo yaliyoathirika.

Pia amesema fedha hizo kama zitatumiwa vizuri, zitasaidia kukabiliana na athari hizo na kurudisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwenye maeneo yaliyo katika hatari ya kupotea na kutishia maisha ya Watanzania.

Naibu Waziri Khamis alisema hayo jana alipozungumza na Watanzania katika Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP27) unaoendelea katika mji wa Sharm El Sheikh, Misri.

Alisema baadhi ya maeneo yameanza kupoteza uhalisia wake kutokana na kupatwa na majanga yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabianchi yakiwamo mafuriko, ukame na kuvamiwa na maji ya bahari.

"Kwa hiyo fedha hizo tukizipata badala ya kujenga madaraja, tutarejesha uhalisia na kuwanusuru wananchi kuwa na hofu kutokana na kufikiwa na maji yasiyo salama. Pemba kule maji ya bahari yanaingia mitaani na kama unavyofahamu kuna baadhi ya kilimo hakistawi katika maji ya bahari," alisema Khamis.

Alisema nchi zilizoendelea, ikiwamo Tanzania, zina mategemeo makubwa ya kupata fedha kutoka nchi zilizoendelea ili kutatua changamoto za mabadiliko ya tabianchi na wako huko kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa.

"Jambo kubwa tunalolipigia kelele tunapokutana na wenzetu wa nchi zilizoendelea ni kuwaambia waharakishe kutupatia fedha ambazo zitatusaidia kutatua changamoto za athari za mabadiliko ya tabianchi katika nchi zetu.

"Anga letu limeharibika, vyanzo vyetu vya maji hususan Tanzania vimeharibika. Sasa suluhisho la hili ni kuendelea kuwaomba watekeleze ahadi walizoweka ili na sisi tutekeleze kile tulichokiahidi kupitia Mkataba wa Paris," alisema.

Khamis alisema mijadala inayoonyesha mafanikio ni ile ya fedha za kusaidia yanapotokea majanga yanayohusiana na athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja fedha za kusaidia kuhimili athari hizo.

"Lakini suala la 'climate financing' (upatikanaji wa fedha za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi) limejadiliwa kwa upana wake na wamelielewa na wamefahamu ni nini tunachokitaka, kwa kuwa wametuelewa na sisi tumepata picha kwamba jambo hili linakwenda vizuri," alisema.

Mafanikio hayo, alisema yametokana na msukumo kubwa uliowekwa na nchi zinazoendelea kwa kuwa kila mkutano wa pembeni unaofanywa na nchi hizo, unasisitiza suala la utekelezaji na ukamishwaji wa fedha.

Nchi za Afrika zikiongozwa na mwenyekiti wake, Ephraim Shitima kutoka Zambia, zimekwenda katika mkutano huo na ajenda sita muhimu za kulisaidia kukabiliana na athari hizo ikiwamo utekelezaji wa ahadi ya dola bilioni 100 za mfuko wa kukabiliana na athari hizo, iliyotolewa mwaka 2009 na nchi zilizoendelea.

Nyingine ni uwezeshwaji wa teknolojia nafuu ili izisaidie nchi hizo kuendeleza miradi yenye uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta mbalimbali zikiwamo kilimo, ufugaji na nishati ili zijikwamue kiuchumi kwa njia salama kwa mazingira.

Ajenda nyingine ni jitihada za kudhibiti ongezeko la joto ambalo sasa ni nyuzi 1.09 kwa mujibu wa Jopo la Umoja wa Mataifa linaloundwa na serikali mbalimbali juu ya mabadiliko ya tabianchi (IPCC), likifika nyuzi joto 1.5 hali itakuwa mbaya.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala (kulia), akizindua Hoteli ya Ubungo Executive Lodge katika stendi ya mabasi ya Magufuli, Mbezi Louis mkoani Dar es Salaam juzi. Wengine ni Meya wa Jiji la Dar, Japhari Nyaigesha (wa pili kulia), Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ubungo, Logati Mbowe. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Waziri ataka huduma za LATRA kwa saa 24

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kupitia Kitengo cha Huduma kwa Wateja, kufanya kazi saa 24 ili kutatua kwa wakati changamoto za wasafirishaji.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Ujenzi na Uchukuz, ilisema Mwakibete alitoa agizo hilo jana jijini Mwanza baada kukagua shughuli za udhibiti wa usafiri wa ardhini na kubaini kasoro mbalimbali ikiwamo utoaji wa vibali vya safari na utoaji wa stika.

"Wasafirishaji hawa ni wafanyabiashara, akichelewa saa mawili au tatu tayari amepoteza fedha nyingi na hili ninyi ndio mnasababisha kwa kuchelewesha kuwapa vibali na stika. Jipangeni vizuri kuanzia mkoa mpaka makao makuu ili malalamiko haya yaishe," alisema.

Mwakibete aliitaka LATRA kukaa na Jeshi la Polisi ili kufanya ukaguzi wa kushtukiza na kupanga mikakati inayotekelezeka itakayopunguza ajali nchini kwa sababu ajali zimeendelea kuongezeka na kupoteza nguvu kazi ya taifa katika maeneo mbalimbali nchini.

Naye Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Mwanza, Halima Lutavi, alisema mfumo unapokuwa na shida katika utoaji vibali, LATRA huwasiliana na Jeshi la Polisi ku waruhusu wasafirishaji kuendelea na safari.

Lutavi alisema kwa sasa mamlaka inaweka mikakati ya kuboresha usafiri wa pikipiki na bajaji kwa kutengeneza njia maalum ili kuhakikisha kunakuwa na utaratibu mzuri wa usafiri huo katika miji.

Naibu Waziri Mwakibete yuko mkoani Mwanza kwa ziara ya siku mbili kukagua miradi ya maendeleo na kuangalia utendaji kazi wa taasisi zilizo chini ya sekta ya uchukuzi.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuyalinde, tuyatunze mazingira kukabiliana mabadiliko tabianchi

**HALI** ya ukosefu wa mvua na baadhi ya maeneo kukumbwa na ukame ni moja ya sababu za uharibifu wa mazingira hasa ukataji wa miti ovyo.

Ukiwa unasafiri kwa njia ya barabara unaweza kushuhudia jinsi baadhi ya maeneo yalivyoathirika kwa kukosa mvua baada ya mazao kukauka na wanyama kuhangaika kutafuta malisho na maji ya kunywa.

Hii inatokana na uharibifu mkubwa wa mazingira wa kukata miti ambayo inasaidia kuleta mvua.

Miti inakatwa kwa wingi kwasababu ya biashara ya mkaa na imeshamiri kwa kiasi kikubwa kutokana na malori na pikipiki zilizosheheni magunia hayo yanavyotoka msituni kuyabeba.

Katika kudhibiti hali hiyo, serikali imechukua juhudi mbalimbali kwa kufanya kampeni ya kupanda miti ili kuweza kurudisha uoto wa asili na kuhifadhi mazingira.

Kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032) kwa lengo la kutoa mwongozo wa hatua za kuchukua ili kutatua changamoto za mazingira nchini kwa kuzingatia upekee wa changamoto katika sehemu husika na hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis wakati wa mjadala ulioandaliwa na Benki ya Dunia kuhusu jitihada za Tanzania katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni sehemu ya mijadala katika Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi unaoendelea Sharm El-Sheikh, Misri, anaeleza mpango kabambe huo unaonesha changamoto za mazingira zinazoikabili Tanzania ikiwa ni pamoja na uharibifu wa ardhi; uharibifu wa vyanzo vya maji; athari za mabadiliko ya tabianchi; uchafuzi wa mazingira; ukataji ovyo wa miti na uharibifu wa misitu; upotevu wa makazi ya wanyamapori na bioanuai.

"Uharibifu wa mfumo-ikolojia ya pwani na baharini; uharibifu wa ardhi oevu; usimamizi hafifu wa taka; kuenea kwa viumbe vamizi; na changamoto za mazingira katika miji zimeainishwa katika Mpango huo," alisisitiza Naibu Waziri Khamis.

Mpango huo kabambe unatoa hatua za kimkakati na mahsusi kwa kuzingatia jiografia na mifumo ikolojia ya maeneo husika. Hatua hizo zinazingatia utofauti wa mtawanyiko wa changamoto za mazingira na hatua muafaka zinazopaswa kuchukuliwa na kutoa mwongozo kuhusu usimamizi wa mazingira.

Kupitia ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mfuko wa Uendelezaji Mitaji (LoCAL), serikali imeanza kutekeleza miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika halmashauri tatu za Kondoa, Chamwino na Mpwapwa pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi wa kuhuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Wito unatolewa kwa jamii kuhakikisha zinaendelea kutunza na kuhifadhi mazingira kwa kuwa Mabadiliko ya Tabianchi ni halisi na kusisitiza utekelezaji wa Sera na Mikakati kwa pamoja kwa kesho iliyo bora kwa kizazi cha sasa na kijacho.


Serikali inaishukuru Benki ya Dunia (WB) kwa kuunga mkono jitihada zake katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi nchini.

Itakumbukwa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira ulizinduliwa Juni 5, 2022 na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa niaba ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Habari njema, shinikizo la bungeni limejibiwa wanavyuo kupata mikopo

Na Anaeli Mbise

**SERIKALI** imeridhia wanafunzi 28,000 waliokidhi vigezo vya kupata mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka 2022/23, waende vyuoni kuendelea na usajili, chini ya utaratibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, wakati taratibu muhimu zikikamilishwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB).

Hatua hiyo, ni habari njema kwa wanafunzi waliokuwa tayari wamekata tamaa ya kuanza masomo. Pia ni ya kuungwa mkono kutokana na serikali kuona umuhimu wa kufadhili wanafunzi hao.

Kilio hicho cha wanafunzi kimesikika, baada ya wiki iliyopita Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipoahirisha Mkutano wa Tisa wa Bunge la 12, hadi Januari 31, 2023 akitoa kauli ya kuwapatia wanafunzi hao mikopo.

Sakata hilo la wanafunzi hao, liliibuliwa na wabunge akiongozwa na Mbunge wa Biharamulo (CCM), Ezra Chilewesa, alipoomba bunge kuahirisha shughuli zilizopangwa kwa muda, ili kujadili tatizo la wanafunzi kukosa mikopo ya elimu ya juu.

Hoja hiyo iliungwa mkono na wabunge na Spika, Dk. Tulia Ackson, akitoa nafasi ijadiliwe na hatimaye bunge liliazimia wanafunzi hao wawezeshwe fedha za kujikimu ili kuendelea na masomo.

Wabunge hapa wametimiza vyema majukumu ya kuisimamia serikali, kama ambavyo katiba inawataka kufanya hivyo.

Wabunge walijadili hoja hiyo, iliyotokana na maazimio ya bunge ya taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali iliyowasilishwa tarehe 5, mwezi huu kuhusu kuifanyia ukaguzi wa kina Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu katika mchakato mzima wa ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini.

Tayari bodi hiyo imekwishatoa tangazo la kuridhia kauli ya serikali ya kuwapatia mikopo wanafunzi 28,000 wenye sifa za kupata mikopo, lakini hawakupokewa vyuoni na kusajiliwa ili kuendelea na masomo.

Kupitia Mkurugenzi Mtendaji wa bodi hiyo, Abdul-Razaq Badru, bodi pia imefungua dirisha la rufani ili kutoa fursa kwa wanafunzi ambao hawakuridhika na viwango vya mikopo walivyopangiwa, kuwasilisha taarifa za uthibitisho ili kuongezewa viwango vya mikopo ikilinganishwa na uhitaji wao.

Kwa sasa, kuna jumla ya wanafunzi watakaotakiwa kuzingatia taratibu za uwasilishaji wa rufani hizo, kwa njia ya mtandao, ambazo ziko katika tovuti ya bodi. Lengo la bodi ni kuwapatia mikopo wanafunzi wapya 71,000 katika mwaka wa masomo uliokwishaanza.

Ni jambo la kuipongeza serikali kwa hatua hiyo ya kuwapatia wanafunzi wenye sifa za kupata mikopo, kwa sababu ni fedha ambazo wataanza kuzirejesha baada ya kuhitimu masomo yao ya elimu ya juu.

Faida ambayo wanafunzi watapata kutokana na mikopo hiyo, ni pamoja na fedha za kujikimu, gharama za chakula na malazi, ada ya mafunzo, vitabu na nyenzo za kuandiki, mahitaji maalum ya vitivo na idara, utafiti pamoja na mafunzo kwa vitendo.

Mikopo hiyo, pia inasaidia kuondoa mzigo kwa wazazi ama walezi wa wanafunzi hao, kwa sababu kwa kiwango kikubwa wanatoka katika familia duni na wanaotegemea kilimo na ufugaji kama njia ya kupata fedha za kuendesha maisha.

Suala hilo la kuwapa mikopo wanafunzi, naamini litaondoa kabisa msongo wa mawazo wawapo vyuoni na kuwa na umakini zaidi, kwa kile wanachofundishwa darasani, maana tayari watakuwa na uhakika wa fedha. Ni hatua moja ya kisafari kumpata mtaalamu sahihi na mwenye weledi.

Vilevile, kwa wanafunzi itakuwa ni vigumu kwao kujiingiza katika vitendo visivyofaa kama ukahaba, rushwa ya ngono na hata matumizi ya vilevi ambavyo mara nyingi wanapata kwa walio nacho na hawajali kuwa mwanafunzi anatakiwa kusoma na maisha ya kujichunga.

Changamoto kubwa ambayo wanafunzi watakabiliana nayo hasa wanaoishi mkoa wa Dar es Salaam, ni tatizo kubwa la uhaba wa maji, ambao unatokana na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo ni habari njema sasa serikali inajitahidi kulitatua, kama tunavyotaarifiwa kwa namna mbalimbali.

## HABARI KITAIFA

# UVCCM yapewa neno uchaguzi viongozi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIJANA wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), wametakiwa kuchagua viongozi bora ambao hawatawagharimu kwa kipindi cha miaka.

Akizungumza jana kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi mkoani hapa, Katibu wa UVCCM Taifa, Kenani Kihongosi, aliwataka kuchagua viongozi ambao hawafanyi kazi kwa maslahi yao.

"Tunaochagua kiongozi tujue tunachagua mtu wa kutuongoza kwa miaka mitano, tukichagua vizuri tutakwenda vizuri mkichagua vibaya, maamuzi mnayo nyie, uhuru wa kuchagua wa kwenu, lakini mtuletee viongozi bora, imara, madhubuti, wenye hofu ya Mungu, watakaokwenda kusaidia kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM, msituletee viongozi watakaokwenda kufanya kazi kwa maslahi yao."

"Viongozi watakaokwenda kufanya mambo kinyume na kanuni yetu ya Umoja wa vijana, msichaguane kwa urafiki, undugu, nendeni mkachague kiongozi bora, ambaye mwaka 2024 tutavuka uchaguzi wa serikali za mitaa, mwaka 2025 tutavuka uchaguzi mkuu kwa kushinda kata na majimbo yote ya Dodoma, msichague kiongozi mbea, mtoa rushwa, mfitini, anayejali vitu visivyo vya msingi, leo ukichagua kesho usinung'unike tusipoyasema haya tutakuwa wanafiki," alionya.

Alisema uchaguzi ukiisha wanapaswa kuvunja makundi ili kukijenga chama na jumuiya.

"Twendeni tukachague watu watakaokuwa wanyenyekevu na si wanyenyekevu ndani ya watu ndani ya CCM, mkifanya hivyo mtakwenda kukitendea haki chama kumtendea haki rais wetu na vijana wa nchi hii," alisema.

Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma, Pili Augustino, aliwataka wanaochaguliwa kutambua wajibu wao kwenye nafasi wanazozitumikia na si kwa ajili ya kupiga kura pekee.

"Leo wanapatikana viongozi wapya, mmepewa majukumu mkafanye kazi ya kuimarisha umoja wenu, kwenye maeneo yenu na sio nafasi hizo mmepewa kuwa wajumbe tu wa kuja kupiga kura, bado mna kazi kubwa ya kuimarisha umoja wa vijana usimame vizuri," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa UVCCM mkoa huo anayemaliza muda wake, Billy Chidabwa, aliwahimiza viongozi watakaochaguliwa kuwa na mshikamano na ushirikiano na vijana wenzao huku akiwashukuru kwa kumwamini kuongoza kwa miaka mitano.

## DC Mtwara aagiza uundaji klabu gesi msingi, sekondari

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

MKUU wa Wilaya ya Mtwara, Dustan Kyoba, amezitaka shule za msingi na sekondari kuanzisha klabu kwa ajili ya kujenga uelewa wa matumizi ya nishati ya gesi asilia kwa jamii.

Akizindua mbio za marathoni za Shirika la Petroli Tanzania (TPDC), zijulikanazo kama 'Min Marathon' zilizoshirikisha watu mbalimbali wakiwamo wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, alisema endapo wanafunzi hao wataelimishwa ipasavyo watakwenda kwenye jamii kutoa elimu hiyo ili waelewe mambo mengi yaliyomo kwenye nishati hiyo.

Alisema kumeonekana faida kubwa ya matumizi ya gesi asilia kama inavyotumika katika Hospitali ya Kanda Mtwara, viwanja vya ndege na maeneo mengine muhimu na elimu ikitolewa itasaidia kuongeza uelewa wa matumizi ya nishati hiyo.

Kyoaba alisema iwapo shule za msingi, vyuo na sekondari zitaanzisha klabu kama ilivyo kwa klabu za kupinga vitendo vya rushwa, itakuwa njia pekee ya kuongeza uelewa wa matumizi ya gesi asilia kwa jamii.

Alisema wito wake kwa sasa ni kuona ushauri wake unafanyiwa kazi haraka ili baada ya muda mfupi Mkoa wa Mtwara katika shule zake za msingi na sekondari ziwe zimeshaunda klabu hizo na kuwa na uelewa ili wafikishe kwa jamii.

Naye Mkuu wa Kitendo cha Mawasiliano wa TPDC, Maria Mselem, alisema shirika lipo katika mchakato wa kujenga kituo cha kujaza gesi kwenye magari mkoani Mtwara, lengo likiwa ni kuendelea kutoa hamasa ya matumizi ya gesi asilia.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Tanzania Fasihi Fund (TAFF), Hussein Wamaywa, akizungumza katika kikao cha wadau wa fasihi Dar es Salaam juzi, kuhusu maandalizi ya Tamasha la Fasihi ya Kiswahili, linalotarajiwa kufanyika Jumamosi Kisarawe, mkoani Pwani. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Tamasha fasihi Kiswahili kurindima Kisarawe

**Na Sabato Kasika**

TAMASHA la fasihi ya Kiswahili litakalowakutanisha wadau kutoka ndani na nje ya nchi, linatarajiwa kufanyika kesho Kisarawe, mkoani Pwani.

Mratibu wa Tamasha hilo, Goima Mwamwingila, aliliambia gazeti hili jana kuwa litakuwa na wageni kutoka katika nchi za Ghana, Nigeria na Kenya na litafanyika kwa siku mbili.

"Tamasha hili litafanyika kuanzia Novemba 19 hadi 20 katika uwanja wa wazi wa Chanzige Sekondari ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe likiwa na kaulimbiu ya 'Kitabu kila mahali -kusoma siachi ng'o," alisema Goima.

Aliwataja wadau wengine walioalikwa kuwa ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Chama cha Hakimiliki (COSOTA).


"Wengine ni Idara ya Kiswahili na Sanaa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, ofisi ya Mbunge wa Kisarawe, Mkuu wa wilaya na wadau wengine wa fasihi," alisema.

Alisema tamasha hilo linalofanyika mara moja kwa mwaka, linalenga kurejesha ari ya jamii kupenda kusoma vitabu ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo kwa watunzi wa kazi za kubuni, fasihi zenye tija na maslahi kwa jamii zao.

"Malengo mengine ni kutoa tuzo za umahiri kwa kazi za fasihi ya Kiswahili zilizofanya vizuri mwaka huu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, kufanya uzinduzi wa vitabu viwili vya hadithi za wanafunzi walioshinda mwaka 2021 na kufanya maonyesho na mauzo ya vitabu," alisema.

Alifafanua kuwa, tamasha hilo pia litatumika kuchangia vitabu, kwa ajili ya maktaba ya shule ya msingi na sekondari, kuzindua riwaya za aina mbalimbali, kufanya utalii wa kifasihi katika eneo la ushoroba na kuwakumbuka wanafasihi waliofanya kazi iliyotukuka ambao kwa sasa wametangulia mbele ya haki.

## KABWELA



## HABARI KITAIFA

# Ufaransa yasema ziara ya Samia imeibua fursa za sayansi, teknolojia

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, amesema ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini humo kukutana na Rais Emmanuel Marcon, imezaa matunda kwa elimu ya juu na sasa fursa za Watanzania kwenda kusoma zimeongezeka.

Akizungumza juzi kwenye uzinduzi wa maonyesho ya elimu ya juu mwaka 2022 yaliyoandaliwa na Ubalozi wa Ufaransa kwa ajili ya wanafunzi wa kitanzania kuona na kusikia maelekezo ya namna ya kujiunga pamoja na kupata ufadhili, alisema nchi hiyo ina vyuo bora vinavyopokea wanafunzi wengi duniani.

Alisema Rais Samia alipokwenda nchini humo Februari, mwaka huu na kukutana na Rais Marcon, walikubaliana kuongeza ushirikiano zaidi kwenye sayansi na teknolojia.

"Rais Samia alitembelea kituo cha sayansi na teknolojia ambacho ni bora duniani na kuahidi kushirikiana kuchota ujuzi na maarifa, ndiyo maana leo (juzi) tuna maonyesho haya na kuendelea kuimarisha uhusiano kwenye sayansi na teknolojia.

"Tuna malengo ya kuvutia wanafunzi nusu milioni ya vyuo vikuu hadi mwaka 2027. Kwa mwaka huu, tuna maombi ya wanafunzi 37,000 wanakuja kutoka nchi mbalimbali na wengi ni Afrika, lakini si kutoka Tanzania ndiyo maana tumeleta maonyesho haya," alisema.

Balozi Hajlaoui alisema maonyesho na mjadala huo umeandaliwa ili kuangalia namna ya kuimarisha uhusiano wa kisayansi na ujuzi ambao Watanzania watanufaika nao na kwamba mshindi wa Tuzo za Nobel ni Mfaransa ambaye ni mwanasayansi, yuko tayari kushirikiana nao.

"Unaweza kuja kama Mtanzania unayezungumza Kiswahili, Kiingereza ukajifunza Kifaransa, ukakutana na kampuni na kwenda maeneo mbalimbali duniani kama Italia, Ujerumani na Canada. Uzoefu unaonyesha wanafunzi wengi waliomaliza masomo yao na kurudi kwenye nchi zao, wamekuwa chachu kubwa ya maendeleo," alisema.

Pia alisema kubadilishana uzoefu wa kisayansi unaamanisha pia timu za vyuo vikuu vya Ufaransa ambavyo ni bora duniani, vitaeleza kazi zao na kutafuta ushirikiano baina yao.

Mwakilishi wa Wizara ya Elimu ya Ufaransa, Matthieu Bragato, alisema vyuo vya Tanzania vilivyoshiriki ni kutoka Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Morogoro, Iringa, Zanzibar na Mwanza na kwamba lengo ni kuwasilisha fursa za masomo kusoma programu zinazofundishwa kwa Kiingereza nchini humo.

Alisema kuna vyuo saba vya Ufaransa vilivyoambatana na kituo cha Kampasi ya Ufaransa, kiongozi wa Kifaransa wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa anayehusika na kuwezesha masomo nchini humo kwa wanafunzi wa kigeni.

"Vyuo vikuu vya Ufaransa vitakuwa na kibanda cha kuwasilisha programu zao mbalimbali zenye ubora zinazofundishwa kwa Kiingereza na Kifaransa na kukutana na wanafunzi. Hizi ni Taasisi saba bora za Elimu ya Juu za Ufaransa, chuo kikuu cha masomo ya kimataifa na kisiasa," alisema.

Alitaja vyuo vya nchi hiyo vitakavyokuwapo kwenye maonyesho hayo kuwa ni Sayansi Po, shule tatu za uhandisi vya IMT Atlantique, IMT Alès, ISEA-SUPAERO, shule mbili za biashara Excelia na SKEMA na shule moja ya kilimo, Institut Agro.




Makamu Mwenyekiti wa Kwanza wa Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI), Hussein Sufian (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Tuzo za Rais kwa Mzalishaji Bora wa Mwaka (PMAYA) zinazotarajiwa kutolewa na Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango kesho. Wengine ni James Meitaron kutoka NBC (kushoto), David Tarimo kutoka Kilimanjaro Cables (kulia) na Hawa Bayumi wa ALAF Ltd. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kitendawili kinara tuzo mzalishaji bora viwandani kuteguliwa

**Na Joseph Mwendapole**

KINARA wa Tuzo za Rais kwa Mzalishaji Bora wa Mwaka (PMAYA), anatarajiwa kupatikana kesho katika hafla ammbayo mgeni Rasmi atakuwa Makamu wa Rais, Dk,. Philip Mpango.

Makamu Mwenyekiti wa Kwanza wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), Hussein Sufian, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa Dk. Mpango atamwakilisha Rais Samia Suluhu Hasssan katika hafla hiyo itakayohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa na kimataifa.

Alisema Rais ndiye mlezi wa tuzo hizo na ndiye amekuwa akitoa kila mwaka kwa mzalishaji bora tangu kuanzishwa kwake mwaka 2005. Nia ya kutoa truzo hizo ni kutambua mchango wa wenye viwanda katika ukuaji wa uchumi.

Sufiani aliwataja mfadhili mkuu wa tuzo hizo kuwa ni Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) akifuatiwa na Tanga Cement Ltd, ALAF Ltd, Kilimanjaro Cables, Coca Cola Kwanza, Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Makamu Mwenyekiti huyo aliwataka wenye viwanda nchini na wanachama wote wa CTI kumuunga mkono Rais Samia katika maono yake ya kuigeuza Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

"PMAYA inatoa changamoto kwa kampuni kubwa na ndogo kuongeza na kuboresha uzalishaji wa bidhaa zao na huduma wanazotoa. Tunashukuru sana kwa msaada tuliopata kutoka kwa wadhamini wa tuzo hizi. Nawahamasisha wenye viwanda waendelee kuzalisha bidhaa bora zitakazoweza kushindana kwenye soko la dunia," alisema.

Alisema lengo la PMAYA ni kutoa zawadi kwa kampuni zilizoonyesha ubunifu kwenye matumizi ya teknolijia na ambazo zimeongeza uuzaji wa bidhaa nje ya nchi na kuisaidia nchi kuwa na fedha nyingi za kigeni.

"Kama mnavyofahamu ili uchumi ukue lazima pia nchi iwe na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Kwa hiyo serikali inaweka mazingira mazuri ili viwanda vya ndani viuze zaidi nje ya nchi ili kupate fedha za kigeni," alisema.

Alisema kazi ya kuwatafuta washindi wa tuzo hiyo imepewa kampuni ya Data Works ambayo imewatembelea wazalishaji na kutumia vigezo vilivyowekwa na katika hafla hiyo, itaweka bayana majina ya kampuni zilizokidhi vigezo na kutajwa kuwa washindi kwenye mashindano ya mwaka huu.

Umoja wa Ulaya (EU), alisema uimedhamini mjadala wa watumiaji wa bandari ya Dar es Salaam hasa wenye viwanda kuhusu namna utoaji wa huduma kwenye bandari hiyo inavyoweza kuboreshwa na kwamba mjadala huo utafanyika kesho asubuhi.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni Kubwa na Uwekezaji kutoka NBC, James Meitaron, alishukuru CTI kwa kuwaamini kuwa wadhamini wakuu wa tuzo za mwaka huu.

"Tunajivunia kuwa sehemu ya ukuzaji wa viwanda nchini. Tunamshukuru Rais Samia kwa kuweka mazingira mazuri ya biashara na kustawisha biashara. Benki yetu ni ya tatu kwa ukubwa wa mali na mtandao wa matawi, hivyo tunaahidi kuendelea kuwa karibu na wafanyabiashara na wenye viwanda," alisema.

# Mamilioni yawakomboa wananchi kero ya afya

**Na Mwandishi Wetu,** MAKAMBAKO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema Sh. milioni 264.3 zilizotolewa na serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) zimetumika kujenga zahanati ya Kijiji cha Ikelu katika Halmashauri ya Mji Makambako na nyumba ya watumishi wa zahanati hiyo.

Mhagama alisema hayo juzi baada ya kukagua ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Ikelu na nyumba ya watumishi, akiwa kwenye ziara ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaoratibiwa na TASAF katika Halmashauri ya Mji Makambako.

Alisema kutokana na maombi ya wananchi wa Kijiji cha Ikelu, serikali iliridhia kutoa Sh. milioni 264.3 kutatua ukosefu wa huduma za afya kwa wananchi wa kijiji hicho.

"Rais kupitia fedha za TASAF alielekeza ijengwe zahanati na nyumba ya watumishi wa zahanati ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora itakayowawezesha kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo," alisema.

Mhagama alisema amekagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo na kubaini kuwa umejengwa kwa ubora na viwango vinavyotakiwa kwa kuzingatia thamani ya fedha iliyotumika.

Waziri Mhagama pia alisema serikali haitaishia katika ujenzi wa zahanati na nyumba ya watumishi pekee kwa kuwa Rais samia ameiagiza TASAF kuleta vifaa tiba ili kuhakikisha huduma za afya ya mama na mtoto pamoja na wananchi kwa ujumla, zinapewa kipaumbe kama ambavyo serikali imekusudia.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema wananchi wa Ikelu wanaishukuru serikali kwa kuwajengea zahanati na nyumba ya watumishi kwa kuwa awali kijiji hicho hakikuwa na zahanati wala kituo cha afya kilicho karibu.

## Kituo chawa mfano EAC

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Wakala wa Vipimo (WMA), Misugusugu Mkoa wa Pwani kimekuwa cha mfano na nchi za Afrika Mashariki zimekuwa zikija kujifunza ubora wa kazi zinazofanywa kwenye kituo hicho.

Kituo hicho kimekuwa kikitumika kuhakiki ujazo wa mafuta kwenye malori, kuhakiki mita za maji na umeme kilijengwa kwa gharama ya Sh. bilioni saba.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, iliyotembelea kituo hicho.

Naibu Waziri alisema kituo hicho ni kipya na kimekuwa mfano bora kutokana na kazi zinazofanywa kiasi cha kuwavutia watu wa nchi jirani kuja mara kwa mara kujifunza kuhusu vipimo.

"Kituo hiki kinafanya kazi nzuri na kitaendelea kuwa mfano hivyo tunaamini mheshimiwa Rais ataendelea kutupa fedha tujenge vituo kama hivi kwa kanda kama ambavyo kamati ya Bunge imeshauri," alisema Kigahe.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa (WMA), Stella Kahwa, alisema wabunge wameona hatua kubwa iliyofikiwa lakini wameshauri kuwe na maabara inayotembea ili kwenda kukagua mita za maji na umeme kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mwenyekiti wa Kamati Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, David Kihenzile, alisema wameona namna mita za maji zinavyohakikiwa na zile za umeme kuhakikisha mwananchi anapewa mita ya maji au umeme yenye ubora ili alipe kile tu anachotumia.

Alipongeza utaratibu huo ambao alisema unamwezesha mwananchi kulipia kile ambacho anatumia na alishauri WMA iendelee kukagua mita hizo kuhakikisha zinakuwa na ubora wa hali ya juu ili kulinda maslahi ya mwananchi.

"Changamoto ambayo tumeiona ni kwamba hivi mtu anayetengeneza mita za maji Katavi au Shinyanga atazisomba zote aje zipimwe hapa Kibaha. Kwa hiyo tumewashauri wakala watazame haya mbeleni ikiwezekana vituo kama hivi vijengwe kwenye kanda lakini kwa kweli wanafanyakazi nzuri sana," alisema.

# Kairuki awacharukia Shirika la Masoko kuhusu nyaraka muhimu

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ameushukia uongozi wa Shirika la Masoko ya Kariakoo, kwa kile walichodai kuwa nyaraka zote muhimu ziliungua katika ajali ya moto iliyotokea Julai 10, mwaka huu.

Aliwataka waliofanya udanganyifu wa aina yoyote kuhusu nyaraka hizo, kujisalimisha mara moja kwa sababu serikali ina mkono mrefu wa kuzipata nyaraka hizo wakati wowote.

Kairuki alitoa tahadhari hiyo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizindua Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Masoko ya Kariakoo iliyoteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Septemba 15, mwaka huu.

"Mnasema vielelezo vyote vimeungua! Taarifa zote ziliteketea, uzuri wa ukaguzi alama huwa hazifutiki. Utakuja kushangazwa kaka (Kaimu Meneja wa Shirika la Masoko ya Kariakoo, Sigsibert Valentine). Mtakuja kushangazwa, nyie mnaamini zimeungua, mtakuja kushangazwa," alisema.

"Kama kuna mtu ambaye hayupo sawa aje ajisalimishe, mtakuja kushangazwa, mwenyekiti wa bodi, nakutamkia hapa mbele yao, mtakuja kushangazwa. Serikali si mjinga, nyie mnaamini mmechomoka, wala hamjachomoka hata kidogo ndugu zangu. Hoja zilizobainika hamjazijibu, serikali ina macho, hakuna atakayesalimika," aliongeza.

Alihoji kutokuwapo kwa mfumo wa kurudisha taarifa muhimu zilizopotea 'backup system' kwa wahasibu na wakaguzi wa ndani wa soko hilo ambao wanatakiwa kuwa nayo.

"Hiki ninachowaambia na kuwapa angalizo serikali ina macho, ninyi mlidhani mmechomoka kwa kusema hamna taarifa, nyaraka haiwekwi sehemu moja, mtakuja kushangazwa, ndio maana nawaambia kama kuna mtu anajua kuna kitu ameficha ajisalimishe haraka sana," alisema Kairuki.

Aidha, aliahidi kusimamia jambo hilo kwa umuhimu mkubwa na kwamba hakuna atakayepona.

"Ndiyo maana nawasisitiza kama kuna jambo unalijua ujisalimishe mapema, maana ukinyamaza nalo ni kosa kisheria. Kuna taarifa unaijua ukakaa kimya, hujasaidia vyombo vya uchunguzi nalo ni kosa kisheria," alisisitiza Kairuki.

Alisema jambo hilo wamelichia vyombo vya uchunguzi kufanya kazi yake na ndio sababu anahimiza watendaji hao kujisalimisha mapema.

"Bado mna nafasi, mkifikiri majibu mliyotoa wakati ule kuwa ndio tumemalizana, bado hatujamalizana ni bora tujisalimishe haraka kuliko kukaa kimya, hela ya serikali haiwezi kupotea hivi hivi tu, pia kama kulikuwa na hujuma itajulikana, kama ni moto wa 'Nature Desaster' itajulikana," alisema Kairuki.

Aliitaka bodi hiyo ya wakurugenzi kufanyia kazi hoja zote za ukaguzi na kufanyia kazi yale yote yaliyobainika.

Sambamba na hilo, aliiagiza bodi hiyo kufanya mapitio ya umiliki wa asilimia 51 ya hisa za soko hilo zinazomilikiwa na Jiji la Dar es Salaam, ambayo awali ilijumuisha halmashauri zote za mkoa huo lakini sasa zinamilikiwa na Ilala pekee.

Pia aliwataka pia kukagua muundo wa kiutendaji wa shirika hilo ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji wa soko hilo.

Aliagiza pia kuangalia mifumo ya TEHAMA kama inasaidiaje kutunza na kuhifadhi nyaraka, usimamizi wa makusanyo na matumizi ya fedha.

Kairuki alisema wanatakiwa kufanya ukaguzi wa ujenzi kama thamani ya fedha na kazi inayofanyika kwa asilimia 49 ulipofikia ujenzi na maendeleo yake.

Awali, Kaimu Meneja Mkuu wa Masoko ya Kariakoo, Sigsibert Valentine, akiwasilisha taarifa kwa Waziri Kairuki, alisema ujenzi wa soko hilo unaojumuisha ukarabati wa jengo la zamani na ujenzi wa jengo hilo jipya umefika asilimia 49.

Alisema utakamilika Oktoba 23, 2023 na linatakuwa na uwezo wa kuajiri watu 4,000 tofauti na awali liliajiri watu 1,600.

Naye Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Hawa Ghasia, alimhakikishia waziri huyo kuwa watafanyia kazi maagizo yake aliyoyatoa na kuchukua hatua stahiki kwa makosa yatakayobainika.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Stephan Ngailo, akifanya jaribio la kuzima moto, wakati wa mafunzo ya kukabiliana na majanga ya moto, yaliyotolewa na wataalamu kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kwa watumishi wa mamlaka hiyo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# TFRA yafundishwa kukabili majanga ya moto

**Na Renatha Msungu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imewajengea uwezo wa kukabili majanga ya moto mahali pa kazi na nyumbani, ili wawe na mbinu mpya janga linapotokea.

Akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika jana Temeke jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, aliwataka watumishi hao kusikiliza na kufuatilia kwa makini hatua zote zinazotakiwa kuzingatiwa wakati wa kuzima moto ili kupunguza madhara ya kupoteza mali na wakati mwingine uhai kwa kushindwa kutumia ipasavyo vifaa na mbinu za kuzima moto pindi majanga yanapotokea.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Koplo Patrick Mwakinunu, alisema moto ni muunganiko wa kemikali ya oksijeni, joto na kitu kinachoweza kuwaka hapo ndipo tutapata kitu kinachoitwa moto.

Alisema kuwa vifaa vinavyobebeka kwa ajili ya kuzima moto kwanza ni mtungi wa kuzimia moto aina ya kabondioxide.

Pia alibainisha hatua zinazotakiwa kuzingatiwa wakati wa kuandaa mtungi kwa ajili ya tukio la kuzima moto.

Alibainisha aina ya madaraja ya moto kuwa ni daraja A unaohusisha vitu vya kawaida vinavyoweza kuungua ikiwa ni pamoja na masofa, mbao, majengo, daraja la pili ni daraja B linalohusisha vimiminika vinavyowaka kama vile petroli, dizeli na aina nyingine za mafuta, daraja C ni moto wa gesi na aina ya nne na ya mwisho ni daraja D unaohusisha moto wa vitu vyenye asili ya kemikali.

Alisema moto wa daraja la A mara nyingi huzimwa kwa maji au mchanga mkavu, daraja B, C na D inazimwa kwa kutumia unga, povu, dawa ya unga, na vifaa vingine na kubainisha poda kavu huzima aina zote za moto.

Naye Sajini Abdulkadir Mchachura alisema jukumu la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kuzima moto na kuokoa mali na hiyo inawafanya kila wakati kuendelea kuusoma na kuulewa moto na mbinu bora za kuuzima pindi kunapotokea majanga.

Mchachura alibainisha kuwa maji si njia pekee inayotumika kuzima moto na kueleza, ili kuzima moto na kuokoa mali ni lazima kuwa na uelewa wa mali unazokwenda kuokoa huku akitoa mfano kuwa ukiwa unazima moto kwenye vifaa vya chuma huwezi kutumia maji kwani utapoteza muundo wa chuma husika na kubainisha kuwa ili kuzima na kuokoa mali ni sharti kuwa na uelewa wa aina ya mali unayopaswa kuiokoa.

# Ulega alia uhaba madaktari mifugo

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema idadi ya madaktari na wataalamu wa mifugo waliopo nchini hawatoshi kuenea maeneo yote ya nchi kuwasaidia wafugaji mifugo yao isife kwa magonjwa.

Ulega aliyasema hayo juzi jijini Arusha wakati wa ufunguzi wa kongamano lililoandaliwa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH) kwa wataalamu wa mifugo kutoka nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na baadhi kutoka nchi zingine duniani.

Alisema sekta ya mifugo ni kubwa na lazima kuwapo mbinu mbadala za kuwasaidia wafugaji kuhakikisha mifugo yao haipati maradhi wala kufa kwa magonjwa.

"Wafugaji wengi wapo vijijini kwa idadi ya madaktari au wataalamu wa mifugo tulionao haitoshelezi kusema wataenea kote, tunao kama 5,600 kote nchini ukilinganisha na ukubwa wa sekta ni wakati wa kuweka mikakati namna ambavyo tunaweza kuwasaidia kufika hadi vijijini."

Alisema umefika wakati wataalamu wa mifugo wajengewe uwezo ili kutoa huduma zaidi maeneo ya vijijini na kulinda usalama wa mifugo na mlaji wa mazao yatokanayo na mifugo.

Ulega alisema lengo la kuwakutanisha wataalamu hao ni kuwajengea uelewa wa pamoja na kupanga mikakati wanavyoweza kusaidiana na wasaidizi kukuza sekta ya mifugo katika nchi zilizopo kwenye jumuiya hizo.

Kwa upande wake Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania (VCT) Dk. Amani Kilemile, alisema majukumu waliyonayo ni kuhakikisha huduma za matibabu ya mifugo zinakuwa bora kwa kufuata sheria zilizoanzisha baraza hilo kwa kusimamia pia ubora wa elimu kwa wataalamu wa mifugo kuanzia ngazi ya cheti.

Alisema baraza linahakikisha kuwatambua wataalamu wa mifugo ambao wamesajiliwa kupitia baraza hilo pamoja na kufuatilia mienendo yao ukiwamo utendaji wao wa kazi katika kuhudumia mifugo kwa njia sahihi inayokubalika kitaalamu.

Alisisitiza kuwa ni muhimu kwa wataalamu wa mifugo kufanya kazi kwa kufuata maadili ya kazi ikiwa na lengo la kuhakikisha inakuwa salama na inatibiwa kwa kufuata taratibu zote zinazokubalika kitaalamu.



Meneja wa Mauzo wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Roman Degelewa (wa pili kushoto), akikabidhi pikipiki kwa Bakari Juma (kulia), kama mkopo kutoka benki hiyo, wakati wa kuchezesha droo ya kwanza ya Bonge la Mpango – Mchongo wa Kusini maalum kwa wateja wa mikoa ya kusini hususan kipindi hiki cha mavuno ya korosho, katika tawi la NMB Mtwara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yaagiza ukaguzi SACCOS

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

SERIKALI wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, imesema itapeleka wataalamu wa fedha kukagua hesabu za Chama cha Akiba na Mikopo (KIUMA SACCOS), kutokana na malalamiko yaliyoko, kuimarisha na kuboresha utendaji wake.

Hayo yamesemwa jana na Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, George Bisani wakati wa Mkutano Mkuu cha KIUMA SACCOS.

Aidha, aliiagiza SACCOS hiyo kuunda tume ya kufuatilia mikopo iliyotolewa nyuma ili kujua ukomo wake, dhamana zilizowekwa, mikataba na marejesho ya kila mwezi ili kuondoa malalamiko.

Bisani alisema kuna malalamiko ya wanachama kuwa bodi inatoa mikopo zaidi ya mara moja kwa mwanachama mmoja bila kujali ana mkopo mwingine au la jambo linaloonyesha kuna upendeleo na rushwa.

Meneja wa SACCOS hiyo, Bonus Ndunguru na Mwenyekiti, Varentino Masudi walithibitisha kuwapo kwa malalamiko na kuahidi kuyafanyia kazi kwa mujibu wa sheria za ushirika.

# NMB yapewa tano kusaidia makandarasi

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ya Zanzibar imeipongeza Benki ya NMB kwa kuleta masuluhisho maalum rafiki kwa ajili ya makandarasi huku ikiamini ndiyo njia rahisi ya kusaidia kuwakuza makandarasi wazawa kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohammed, alipokuwa anazindua rasmi warsha ya NMB na makandarasi wa Zanzibar.

"Tuna kila sababu ya kupongeza uongozi mzima wa NMB kwa kuamua kuja na suluhisho ambalo linawalenga makandarasi. Hili ni jambo jema na naamini litawaongezea ari ya kufanya kazi kwa weledi na ubora na kuinua makandarasi wazawa," alisema Dk. Khalid.

Aliwataka makandarasi kuchangamkia fursa hizo zinazoletwa na NMB, na kuwasihi kutumia fedha za mikopo wanazopata kutoka benki kwa ajili ya kazi walizokopea na si kwa shuguli zingine ambazo zinaweza kusababisha ugumu katika kurejesha.

Tusiwe na tabia ya kubadili matumizi ya mikopo tunayopewa kwani kufanya hivyo, italeta ugumu katika kurejesha na baadaye badala ya kunyanyuka kama ilivyo azma ya NMB, tutaishia kushuka chini zaidi. Matumizi mazuri ya fedha ni jambo la muhimu na la kuwa nalo makini katika kutekeleza kazi zetu hasa kwa fedha za mikopo tunazochukua kutoka kwenye benki kama NMB," alisema.

Mwakilishi wa NMB ambaye ni Mkuu wa Idara ya Miamala wa Benki hiyo, Linda Teggisa, alisema benki hiyo imesimama katika nafasi ya kuendelea kuongeza fursa ya upatikanaji wa huduma za kifedha ili kuendelea kuwawezesha makandarasi kutekeleza miradi mbalimbali.

"Benki ya NMB ni mdau mkubwa wa sekta ya ujenzi nchini, hivyo imeona umuhimu wa kuandaa warsha hii na kuwakutanisha wadau wote wa sekta hiyo kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kuwaelezea fursa nyingi kutoka NMB. Tunaamini baada ya hapo, zitakwenda kuongeza tija katika ufanyaji kazi wa makandarasi hawa," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka, alisema sekta ya ujenzi ni ya muhimu kwa Zanzibar kwa sasa kwa kuwa ni miongoni mwa sekta ambazo zinaongeza ajira rasmi na zisizo rasmi kwa wananchi wa Zanzibar.

"Sekta za utalii na ujenzi ndizo sekta zilizoongeza ajira nyingi sana kwa Zanzibar kwa kipindi cha karibuni. Zaidi ya ajira 50,000 zimetokana na sekta hizi huku ujenzi ikichangia ajira mpya 26,371," alisema.



## CCM yasisitiza kanuni uchaguzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa kimewataka wagombea wote walioteuliwa kugombea nafasi mbalimbali, ndani ya chama hicho kuheshimu kanuni za uchaguzi na kanuni za uongozi na maadili.

Pia kimetoa onyo kali kwa wagombea hao kutofanya kampeni za kupakana matope, pamoja na kutoa rushwa kwa sababu ni kinyume na maadili ya chama hicho.

Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, Musa Matoroka, ametoa onyo hilo jana ofisini kwake, wakati akizungumza na mwandishi wa gazeti hili juu ya ratiba za uchaguzi ngazi ya Jumuiya Mkoa wa Arusha pamoja na chama.

"Wagombea wote ambao wameteuliwa kugombea nafasi mbalimbali ndani ya CCM katika mkoa wa Arusha na jumuiya zake, wazingatie kanuni za uchaguzi na kanuni za uongozi na maadili. Watakaokiuka kanuni hizo watachukuliwa hatua kali za kinidhamu ili iwe fundisho kwa makada wengine wenye tabia kama hizo," alisisitiza. Kwa mujibu wa Matoroka, CCM ina intelijensia yake ni kubwa na iko kazini kufuatilia mienendo ya wagombea wote ili kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa amani na utulivu.

Pia alisema watendaji wa CCM na jumuiya zake watatenda haki kwa wagombea wote, kwa sababu wagombea wote ni sawa na hakuna mwana CCM ambaye ni muhimu au bora kuliko mgombea mwingine. "Wagombea wote ambao majina yao yamerudi ni dhahiri kuwa wana sifa za kuwa viongozi, lakini mwisho wa siku kila mgombea atambue kuwa nafasi moja hivyo atakayeshinda aungwe mkono na mimi kama mkurugenzi wa uchaguzi nitahakikisha haki inatendeka kwa wote,"alisema.

Kuhusu baadhi ya wagombea kutuhumiwa kutoa rushwa na kufanya kampeni za kupakana matope, alisema mpaka sasa hajapokea malalamiko yoyote na iwapo kuna mgombea atabainika kukiuka miiko na maadili ya CCM katika uchaguzi atashughulikiwa kikamilifu.

"Ni marufuku kwa mgombea yeyote kufanya kampeni za kupakana matope au kutoa rushwa kwa wajumbe, ili wamchague kuwa kiongozi kwa sababu uongozi kwenye CCM haununuliwi kwa fedha," alisema.

Kuhusu orodha ya majina ya wagombea wa nafasi za uenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha pamoja na jumuiya zake ngazi ya mkoa na ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Matoroka alisema ni mapema kutoa majina hayo na hivi sasa anaendelea na utaratibu wa kuwaandikia barua makada walioteuliwa kugombea nafasi mbalimbali.

"Kwa sasa ni vigumu kutoa majina ya wanaogombea nafasi mbalimbali katika mkoa wetu wa Arusha kwa sababu nina jukumu la kuandaa barua za wagombea walioteuliwa, lakini sijapata maelekezo ya kutoa majina hayo kwenye vyombo vya habari," alisema.

Awali katika uchaguzi huo makada waliojitokeza kugombea nafasi ya uenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha walikuwa 22, huku makada walioteuliwa wakiwa watatu pekee.

# Wadau wajenga nyumba ya mtumishi afya

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WADAU wa maendeleo kutoka Ujerumani kupitia Shirika la Help for Maasai Children, wametoa msaada wa kujenga nyumba ya watumishi wa afya kwenye Zahanati ya Nameloki, katika Kijiji cha Losinoni Juu, Kata ya Oldonyowas, wilayani Arumeru mkoani humo.

Ujenzi wa nyumba hiyo umegharimu Sh. milioni 30 na lengo la kujenga miundombinu hiyo ni kuunga mkono juhudi za serikali ya Tanzania katika kuboresha na kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi hususani wa vijijini.

Akizungumza jana wakati wa akikabidhi nyumba hiyo, mwakilishi wa wadau hao kutoka Ujerumani, Andreas Reinke, alisema wamefikia hatua hiyo baada ya kutambua kuwa kuna adha ya upatikanaji wa matibabu kwa wananchi wa eneo hilo.

Alisema kutokana na adha hiyo, aliamua kujenga zahanati na nyumba ya mtumishi ili wananchi wapate huduma za dharura hasa nyakati za usiku.

"Tulijenga zahanati, tukaona tujenge na nyumba ya mtumishi kwa ajili ya kuongeza wigo wa upatikanaji huduma za afya kwa wepesi kwa wananchi wa Losinoni. Kupitia jambo hili tunaungana na serikali ya Tanzania kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya unaimarika kwa wananchi wote," alisema Reinke.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Selemani Msumi, licha ya kuwashukuru wadau hao, alikiri kuwa msaada huo una mchango mkubwa kwa wananchi.

Alisema msaada huo utatekeleza vipaumbele vya serikali ikiwamo kusogeza huduma kwa wananchi kwa lengo la kupunguza vifo vya wanawake na watoto nchini.

Mkurugenzi huyo aliwataka wananchi hao kuutunza mradi pamoja na wahudumu wa afya waliopangiwa kufanya kazi hapo ili udumu kwa sasa na vizazi vijavyo.

"Wananchi mmepata zahanati na serikali imeleta madaktari hapa. Hakikisheni mnatunza miundombinu na mali zote pamoja na kushirikiana na watumishi hawa kwa kuwa ni ndugu zenu, ni Watanzania wenzetu," alisema.

Wananchi wa Losinoni Juu walikiri na kufurahishwa uwapo wa zahanati na nyumba ya daktari kwa kuwa imewarahisishia upatikanaji wa huduma wanapokuwa wagonjwa hasa wajawazito na watoto.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe, akionyesha kwa waandishi wa habari juzi, gari linalomilikiwa na raia wa Kenya, lililotumika kusafirisha wahamiaji haramu hivi karibuni. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# RC ahimiza matumizi takwimu kwa maendeleo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAASISI ya Watakwimu Tanzania (TASTA) imehimizwa kuweka ajenda mahsusi ya kutoa elimu ya matumizi ya takwimu, kwa taasisi mbalimbali zikiwamo za elimu ya juu na umma kwa lengo la kuchagiza maendeleo katika jamii.


Akizungumza jana jijini hapo katika mkutano wa tano wa mwaka wa chama hicho, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alisema ili watu wengi waepuke kutaja takwimu bila kuwa na uhakika nazo ni muhimu chama hicho kuweka ajenda ya kutoa elimu ya matumizi ya takwimu sahihi.

"Watakwimu wamekuwa na nafasi za kipekee kuharakisha maendeleo ya nchi kwa sababu takwimu ni muhimu, hivyo ni muhimu kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia, hatua itakayorahisisha uchakataji wa data.

"Tumeshirikiana kwenye sensa na tumeona teknolojia mwaka huu jinsi tumekusanya taarifa kwa kutumia vishikwambi. Madososo yalikuwa marefu ila umemudu, hivyo mwendelee kuimarisha mbinu za uzalishaji wa takwimu kwa kutumia teknolojia ili kusaidia upatikanaji na ukusanyaji wa takwimu zitakazosaidia mipango ya maendeleo," alisema. Mwenyekiti wa TASTA, Titus Mwisomba, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili masuala mbalimbali ya ustawi wa chama hicho ikiwamo kuendelea kushirikiana na serikali.

Alisema kwa mfano, walishiriki sensa ya watu na makazi hasa katika ufundishaji wa wadadisi waliokusanya taarifa kutoka ngazi za kaya. "Ni jukumu kubwa la watakwimu kuhakikisha takwimu zinazozalishwa zinazingatia taratibu, vigezo na taaluma ambayo tunayo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Dk. Amina Msengwa, alisema watakwimu nchini wanapaswa kufuata utaratibu na vigezo hatua itakayowezesha upatikanaji wa takwimu sahihi.





# Waomba msaada kukabiliana njaa

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WANANCHI wa Kijiji cha Elkaria katika kata ya Sepeko wilayani Monduli wameiomba serikali kuwasaidia kutatua tatizo la njaa inayoikabili kata hiyo, linalotokana na ukame ulioko.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wananchi hao walisema kuwa wamekumbwa na tatizo la njaa kwa kipindi cha muda mrefu sasa ambapo walibainisha kuwa awali walikuwa wakitegemea maji kutoka katika Mto Nanja kwa ajili ya kilimo pamoja na mvua lakini kwa sasa kwa kipindi cha muda mrefu hawaja vipata hivyo wameshindwa kulima.

Nariba Siberi, mkazi wa kijiji cha Elkaria, alisema kutokana na ukame uliopo katika kijiji hicho wanakabiliwa na ukosefu wa chakula kutokana na kutolima kwa kipindi kirefu kwa sababu ya ukosefu wa mvua.

"Tumekuwa tunakabiliwa sana na tatizo la ukame hali inayotusababishia mifugo yetu kukosa chakula, sisi wenyewe, japo kuwa serikali ilitusaidia kutuletea chakula cha bei nafuu lakini kutokana na hali ya uchumi tumeshindwa hata kwenda katika makao makuu ya halmashauri kuchukuwa chakula hicho," alisema mkazi mwingine, Lembris Simon. Diwani wa Sepeko, Diwani Kimai, alisema kuwa katika kata yao hali ni mbaya sana ya chakula kwani wamekuwa wanalima kwa msimu mmoja lakini katika kipindi hiki wameshindwa kulima kutokana na kutokuwapo na mvua. Alisema kuwa kata hiyo inawananchi zaidi ya 16,000 ambao wote wanauhitaji wa chakula, lakini hadi sasa hawajapata mvua na wamekuwa wakitegemea maji katika bwawa la Nanja kwa ajili ya kilimo lakini kutokana na kukauka Kwa bwawa hilo wameshidwa ata kulima mahindi Kwa ajili ya chakula.

"Suala la chakula ni tatizo sana katika kata yetu kwani katika kipindi hiki hakuna chakula kutokana na ukame uliopo katika kata hii tulikuwa tunategemea mvua ili tuoteshe lakini kwa kipindi hiki hamna mvua yoyote iliyonyesha," alisema.

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Frank Mwaisumbe, alisema wamesikia tatizo hilo na wameshaanza kulifanyia kazi .

# Babati yajivunia mafanikio lishe shuleni

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

HALMASHAURI ya Mji wa Babati mkoani Manyara, imefanikiwa katika masuala ya lishe shuleni baada ya kutoa huduma hiyo kwa shule za msingi za serikali 34 kati ya 36.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri hiyo, Simon Mumbee, wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii juu ya utoaji wa chakula shuleni.

Alisema shule ambazo hazitoi chakula shuleni katika halmashauri hiyo ni shule ya msingi Himiti na Bonga.

Mumbee alisema mpango wa kutoa chakula shuleni unaratibiwa na wazazi kwa kujiwekea utaratibu wa kuchangia chakula shuleni.

"Wazazi wao wenyewe ndio wanakaa kwenye vikao vyao na kukubaliana namna ya kuwa wanachangia chakula cha watoto wao," alisema Mumbee.

Naye Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Laurencia Peter, akizungumzia chakula shuleni, alisema kuna uhusiano mkubwa kati ya chakula shuleni na kuelewa darasani.

Peter alisema ni vizuri wazazi wakawa tayari kuchangia chakula shuleni ili kuwahakikishia lishe bora wanafunzi na kuwasaidia kujifunza bila tatizo.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) ya mwaka 2019, zaidi ya watoto milioni 200 duniani hawapati lishe toshelezi.

Pia Programu Jumuishi ya Taifa ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ( PJT-MMMAM) iliyozinduliwa Desemba 13, mwaka jana, inaeleza kuwa idadi ya watu na afya wa Tanzania na utafiti wa kitaifa wa lishe na miongozo mbalimbali ya lishe, haizungumzii namna bora ya lishe kwa watoto kati ya miaka mitatu mpaka minane.

PJT-MMMAM inasema msisitizo upo zaidi kwenye afua za lishe ya mama mjamzito, mtoto mchanga na kijana.

Mkazi wa Gendi, Johanitha Bernard, akizungumzia utoaji wa chakula shuleni, alisema hakuna tatizo isipokuwa wanaozembea kuchangia chakula ndio wanakuwa watu wa kulalamika.



Nabii Mkuu wa Kanisa la Ngurumo ya Upako la Arusha, Dk. GeorDavie Kasambale (kushoto), akisalimiana kabla ya mazungumzo na Meya wa Jiji la Bujumbura, Jimmy Hatungimana, alipofanya ziara ya siku saba nchini Burundi juzi, pia alipokea tuzo ya amani kutoka katika Taasisi ya Mandela Peace Center. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# RC awataka wananchi kuhama kupisha upanuzi wa barabara

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, amewataka wananchi waliopo pembezoni mwa barabara ya Mianzini jijini Arusha hadi Ngaramtoni wilayani Arumeru, kupisha eneo hilo ili Desemba 26, mwaka huu, kazi ya kubomoa nyumba ianze kwa ajili ya upanuzi.

Mongela alitoa agizo hilo jana baada ya kukagua na kutembelea eneo la ujenzi wa barabara hiyo, kufuatia baadhi watu kulalamikia ujenzi huo wa barabara.

"Naagiza wananchi wote mnaofahamu mpaka ndani ya mita 20 za barabara nawapa mwezi mmoja mpishe ujenzi uanze kwa sababu mkandarasi hawezi shinda kuanza kazi yake kwa sababu yenu,"alisema.

Pia alisema tayari serikali ilishatoa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, lakini wapo watu wachache wanaokwamisha, hivyo vizuri kila mmoja wakati sheria bila shuruti.

Kwa mujibu wa Mongela, ujenzi wa barabara ya Mianzini hadi Ngaramtoni awali wananchi walipaswa kupisha mita 40, lakini sasa wanatakiwa kupisha mita 20.

"Serikali imeona kupisha mita 40 wananchi wengi wataumia na kuleta maumivu kwa wananchi wake, hivyo ikapunguza hadi mita 20, hivyo hakuna haja ya watu kuanza kulalamika,"alisema.

Pia alisema kutokana na hatua hiyo hakuna fomu za tathmini wala fidia sababu mita 20 zimeondolewa na lazima barabara ijengwe kiwango cha lami ili kuleta maendeleo kwa wakazi wa maeneo ambayo barabara nitapita.

"Maendeleo yoyote ninavyojua mimi yanapokuja lazima yaje na maumivu, kinachotakiwa kuyapokea na kusonga mbele bila kuyakwamisha kwa manufaa ya wengi na wapo wenzenu wakati analalamika, wapo wanaotarajia mambo mazuri mara tu barabara hii itakapokamilika," alisema.

Awali akizungumza kwa niaba ya wenzake, Anastazia Mollel, aliomba miezi mitatu ya kuhama eneo hilo na ulipaji wa fidia wa sehemu za nyumba zao zitakazovunjwa.

Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Arusha, Mhandisi Reginald Massawe, alisema hatua ya mradi huo kuanza itasaidia kufungua fursa katika maeneo hayo.

Hata hivyo aliwaomba wananchi walioko maeneo ya barabara itakapopita kufuata maagizo ya serikali, ili kuleta maendeleo.

AFYA NA MAZINGIRA

ALHAMISI NOVEMBA 17, 2022

Ukurasa 14



**KONGAMANO MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA**
**Tanzania inashika namba tano wingi wagonjwa sikoseli duniani**



**Misukosuko ya mabadiliko tabianchi duniani, nini somo kwa Watanzania?**

Ukurasa 16

# Lijue eneo lisilo na mwenyewe, kufikia panahitaji wiki na nusu

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kinachoitwa 'Remote Experiences: Extraordinary Travels from North to South' Mpiga picha David De Vleeschauwer na mwandishi wa habari za usafiri Debbie Pappyn walisafiri kuyafikia maeneo 12 yaliyofichika zaidi, yasiyotambulika na ya mbali zaidi ambayo hayajaguswa na utalii.

Wakaenda hapo ambako hapafikiwi, wawili hao wakitumia kuwahimiza wengine kusafiri kuyafikia na kwa malengo zaidi na kutunza vyema sayari.

Hakuna mtu anayemiliki eneo hilo la ncha ya kaskazini ni kama karatasi ya barafu inayobadilika kila wakati inayoelea katikati ya Bahari ya Aktiki.

Meli kubwa zaidi duniani na yenye nguvu zaidi ya kuvunja barafu inayotumia nyuklia, husafiri kila msimu wa joto linalofikia hadi nyuzi joto 90° Kaskazini ikiwa na abiria 100, wote wana shauku kubwa ya kukanyaga eneo hili muhimu kijiografia.

Kwa wengi wao, wakati huo ni zaidi ya kuongeza orodha tu ya kufika katika maeneo fulani. Meli inayopasua barafu yenye unene wa mita tatu, huelekea huko, imeundwa jina na Russia ikibeba ujumbe "Miaka 50 ya Ushindi" kama kumbukumbu ya miaka 50 ya ushindi wa Umoja wa Kisovieti (USSR) katika Vita Kuu ya Pili.

Kwenye kuadhimisha uzinduzi wake, meli hiyo ilibeba mwenge wa Olimpiki hadi mahali hapo mnamo mwaka 2013 wakati wa maandalizi ya michezo ya Olimpiki ya majira ya baridi.



Mandhari ya kisiwa kisicho na mwenyewe. **PICHA: MTANDAO.**

Hapo kukaendeshwa na vinu vya nyuklia vya megawati 171 na jenereta mbili za megawati 27.6, meli hiyo inayovunja barafu yenye urefu wa karibu mita 160 inaweza kukimbia mwendokasi kilomita 40 kwa saa na kusafiri bila kusimama kwa karibu miaka sita bila kurejea nchi kavu kwa ajili ya kujaza mafuta.

Kukiwa na vinu vya nyuklia, vituo vya kusimama kwa ajili ya kuweka mafuta vinakaribia kuwa historia.

Meli hiyo inaweza kutembea baharini bila kusimama kwa miaka sita 6 mfululizo bila ya kujaza mafuta. Ni safari ya kawaida baharini ndani ya meli ya kifahari.

Njia ya kuelekea eneo hilo la Kaskazini kabisa ya sayari ambako mhimili wa mzunguko wa dunia hukutana na uso wake, inachukua siku 11 kwa mwendo wa kawaida usiozidi kilomita 20 kwa, wakati wa kupasua barafu iote.

Duniani, wasafiri huichukua safari hiyo ni mahsusi ya kukanyaga ardhi ya pembe ya dunia, kupata uzoefu na ushuhuda wa kuvutiwa na Aktiki, wakitazama sehemu kubwa ya barafu ya bahari. Jua halitui kamwe katika majira ya kiangazi ya Aktiki na bado mwanga hubadilika kila mara, ukiakisi barafu nyeupe na angavu.

Kuna wakati hali ya hewa ni ya baridi na hali mbaya na isiyo na utulivu, yenye ukungu mnene. Hilo halijalishi kama uko nje au mtu anatazama kupitia matundu ya meli.

Baada ya siku kadhaa kusafiri, mtu anapofika kwenye eneo hili la ncha ya Kaskazini, abiria huwa na bashasha na baadhi wanaielezea kama hisia ya mwanzo mpya.

North Pole imejificha na ni eneo dogo. Katika Kisiwa cha Hooker, ndani ya ukanda huo, boti za Zodiac hubeba abiria kwenye barafu karibu na Rubini Rock ili kushuhudia miamba inayouvutia.

Abiria wanaalikwa kujiunga katika eneo hilo, kujifunza ukubwa halisi wa jangwa hili lililoganda. Wakati helikopta inapopaa kutoka kwenye meli, meli kubwa ya chuma inabaki kuelea hubadilika na kuwa chembe ndogo nyekundu katika bahari yenye rangi nyeupe inayometa na njia zake kwenye barafu zikiwa bado zinaonekana kama mshipa katika bahari ya Aktiki yenye giza na baridi.

Helikopta huzunguka meli na kuruhusu abiria kufahamu - mazingira hayo. Kabla ya safari hiyo, hakuna mtu ambaye angeweza kutambua kwamba mandhari hiyo ikoje na inaweza kufikiwa, kwenye ncha ya Kaskazini ya dunia.

Sasa, baada ya kukanyaga eneo hili, wasafiri hatimaye wanaelewa ukubwa na barafu nyeupe linalotandaza sehemu ya juu kabisa ya dunia yetu.

- ***Kwa mujibu wa makala ya BBC iliyotokana na simulizi kutoka kitabu 'Remote Experiences: Extraordinary Travels from North to South.'***

AFYA

### KONGAMANO LA MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA

# Tanzania inashika namba tano wingi wagonjwa sikoseli duniani

## • Wataalamu wachambua, waanika maradhi

**Na Anthony Gervas, Mwanza**



Dk. Asteria Mpoto; Mratibu wa Ugonjwa wa Selimindu, kutoka Wizara ya Afya. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

KONGAMANO la nne kitaifa la magonjwa yasiyoambukiza 'sikoseli' (selimundu) lililofanyika jijini Mwanza, limewaibua wanafunzi wa shule za sekondari jijini humo kushiriki na kupata uelewa kuhusu elimu iliyotolewa na wataalamu, kupitia Wizara ya Afya nchini.

Ni mkutano uliojumuisha washiriki zaidi ya 400 kutoka katika taasisi na sekta za kidini, elimu, afya, taasisi za umma na wadau mbalimbali kama Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba Muhimbili (MUHAS) kwa ushirikiano na Chuo kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya Bugando (CUHAS) kupitia waandaaji kongamano, Wizara ya Afya.

Kulikuwapo wanafunzi 48 wa shule za sekondari jijini Mwanza, ambazo ni Pamba, Buhongwa na Nsumba Mwanza. Pia, walimu walishirikishwa kupata uelewa na elimu ya magonjwa yasiyoambukiza na watoto sikoseli, moyo, kansa (saratani), presha na kisukari.

Ajenda kuu ya kongamano hilo iliyojadiliwa na wataalam wa afya kutoka taasisi mbalimbali, kuhusu magonjwa hayo yanavyopatikana, pia namna ya kukabiliana nayo kuyadhibiti jicho la kipekee kikaoni likigusa maradhi 'sikoseli' kwa watoto wanaozaliwa nao.

**MTAALAMU WA WIZARA**

Dk. Asteria Mpoto kutoka Wizara ya Afya, Idara ya Tiba, kitengo cha Magonjwa Yasiyoambukiza akiwa ni msimamizi wa huduma za sikoseli, anabainisha kuwa ugonjwa huo ni wa kurithi ambao unaathiri chembechembe nyekundu za damu, pia unasababisha upungufu wa damu, maumivu makali katika mifupa na maambukizi kwenye damu.

''Duniani watu milioni 20 wana ugonjwa wa 'sikoseli' (selimundu)' ikiwa kila mwaka watoto 300,000 huzaliwa na ugonjwa huo. Tanzania ni nchi ya tano kuwa na wagonjwa hao, ikishika nafasi ya tatu Afrika,' anasema Dk. Asteria.

Mtaalamu huyo na msimamizi wa kiserikali kuhusu maradhi hayo, anazitaja dalili za sikoseli kwa watoto chini ya miaka sita, kuwa ni kwamba huvimba miguu, kusikia maumivu makali kila mara, anapungukiwa damu na kudumaa mwili.

Anasema kutokana na hali hiyo, Tanzania kila mwaka wanazaliwa watoto 11,000 wenye maradhi sikoseli, hivyo serikali inahimiza kuchukuliwa tahadhari mapema kuzuia kutolewa elimu, kwani huenda idadi ikaongezeka kila mwaka ikafika mara mbili ya sasa, ifikapo mwaka 2050.

"Mikoa iliyoathirika zaidi na ugonjwa huo Tanzania ni Kanda ya Mashariki, Morogoro, Dar-es Salaam, Pwani, Kanda ya Magharibi, mikoa ya Kigoma na Tabora pamoja na Kanda ya Ziwa, mkoa wa Mara," anafafanua Dk. Asteria.

Anasema tafiti zilizofanyika zinaonyesha asilimia 20 ya Watanzania wana vinasaba vya sikoseli na kwa miaka miwili, takribani wagonjwa 283,836 walipata huduma ya matibabu hayo na taarifa zao zilikusanywa na kuingizwa kwenye mfumo wao kitaifa.

Mwaka jana anasema, nchini kulifanyika upimaji wa awali wa watoto wachanga katika Siku ya Maadhimisho ya Sikoseli Duniani, yaliyofanyika jijini Mwanza katika Hospitali ya Kanda Bugando.

Serikali inasema imeimarisha huduma zake na kuanzisha kliniki 28 katika hospitali za rufani za mikoa na wilaya nchini, huku matibabu yake yakiingizwa katika Kitabu cha Mwongozo wa Kitaifa.

Vilevile anaeleza upatikanaji dawa, nao sasa upo kupitia mfumo kwa wagonjwa wenye bima za afya, wizara ikiendelea kusaidia kutekeleza mikakati ya kuboresha huduma nchini.




Pia anasema, Wizara ya Afya imeanzisha uratibu wa magonjwa yasiyoambukiza na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) inaendelea kuimarisha mfumo wa ununuzi na usambazaji dawa kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa hao.

Anarejea mwaka 2017, zilianzishwa kadi za wagonjwa hao ili watambuliwe kirahisi, wakitarajia mwaka huu watazindua na kuzisambaza katika hospitali za rufani za mikoa nchini, ugonjwa ukiwa umepewa kipaumbele na serikali.

Kwa mujibu wa Daktari Asteria, Wizara ya Afya ina mpango wa kuanzisha vituo 10 vya mfano bora vya upimaji na kutoa huduma nchini, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam; KCMC, Kilimajaro; Bugando Mwanza; Hospitali ya Kanda Mbeya' na Benjamin Mkapa jijini Dodoma.

**BINGWA WA BUGANDO**

Emmanuel Ambrose, ni daktari bingwa wa magonjwa ya watoto, Hospitali ya Kanda Bugando, anafafanua upande wa Kanda ya Ziwa Tanzania kuna kiwango kikubwa cha ugonjwa huo, ila wanaougua hawajitambui.

Anaeleza watu wengi wana chembechembe za sikoseli na katika kliniki yao Bugando takribani wagonjwa 1,000 wanaenda kupata matibabu, akilalamika tatizo kubwa wanachelewa kupata huduma ya vipimo kwa wakati, wakijikuta wameshambuliwa, pia na magonjwa mengine kama figo.

"Mwingiliano wa watu katika jamii moja yenye ugonjwa ule, kuoana bila ya kupima afya, pia ni chanzo cha kuzaliwa watoto wa aina hiyo. Ni vyema kupima kabla hawajawa wanandoa," anasema Dk. Ambrose.

Anaeleza Hospitali ya Kanda Bugando, inaendelea kupima vinasaba vya ugonjwa huo bure, pia inatoa elimu, ikishirikiana na Wizara ya Afya, inayoendelea kusambaza mpango wa elimu kuhakikisha unawafikia hadi vijijini, kuhusu magonjwa yasiyoambukiza.

**WANAFUNZI WAELEZA**

Mussa Mzunya, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Pamba jijini hapa, anaiambia Nipashe kuwa mjadala kwenye kongamano umempa ufahamu na uelewa wa ugonjwa huo kwa watoto na chanzo chake.

Pia, anaorodhesha darasa la magonjwa mengine anayoyataja kuwa ni moyo, saratani, figo,kisukari na presha, akihiadi kuwa balozi bora kwa wenzake.

"Kikubwa ni kuzingatia kaulimbiu ya wataalam Wizara ya Afya inayosema 'badili mtindo wa maisha boresha afya' kuepuka matumizi ya chumvi nyingi, sukari, vyakula vya mafuta, vinywaji vyenye sukari nyingi wanavyotumia binadamu kila siku,' anasema Mzunya.

Pia, anataja manufaa ya darasa la kufanya mazoezi, kula vyakula vitokanavyo na mimea asili na mafuta kama vile alizeti, karanga na matunda ya asili.

Anasema msongo wa mawazo nao ni somo alilolipata hata anuia kuwa mwelimishaji wa magonjwa hayo na kufikisha ujumbe kwa wenzake kuhusu 'sikoseli'na magonjwa mengine yasiyoambukiza.

Mwanafunzi kidato cha kwanza, kutoka Shule ya Mwanza Sekondari, Aisha Abdillah, anasema kongamano limemjengea uwezo kufahamu magonjwa hayo, ikiwamo sikoseli kwa watoto wanaozaliwa.

Abdillah, anasema ameweza kutambua magonjwa mengine kama ya ajali na afya ya akili, ambayo hakuyafahamu awali, akiahidi atakaporudi kuwa mwalimu kwa wanafunzi wenzake, akiwashauri kuanzisha vikundi shuleni vya utoaji elimu.

"Elimu niliyoipata hapa nitaitumia shuleni,ikiwa ni pamoja na kuepuka kutumia vinywaji vyenye sukari nyingi kama vile soda,kula biskuti,chokleti, kashata na vitu vyenye mafuta mengi na chumvi.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mwanza, Awe Minjo, anayefundisha masomo ya biashara kidato cha pili na tatu, anasema atatumia vipeperushi vya magonjwa yasiyoambukiza kwa ajili ya wanafunzi kujisomea shuleni.

Minjo anaeleza, atatengeneza kipindi maalum shuleni kwa ajili ya wanafunzi kupata elimu hiyo na uelewa ili waweze na wao kuwafikishia wazazi ujumbe huo nyumbani.

MAZINGIRA

IKOLOJIA HIFADHI YA NYERERE...

# Ujue mti matambiko ulioshindikana kung'oka kwa greda, unapoteza watu

- Utitiri mimea adimu na viumbe ajabu
- Historia shule, inaposhuhudiwa 'live'

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**



Mti wa ajabu unaoshindikana kung'oka kwa nyenzo zote. **PICHA: ASHTON BALAIGWA.**

HIFADHI ya Taifa ya Nyerere kwa sasa, ndio kubwa kuliko zote ukanda wa Afrika, baada ya kuanzishwa mwaka 2019, ikimegwa kutoka iliyokuwa Pori Tengefu la Akiba la Selous.

Aliyekuwa Rais, Dk, John Magufuli, akaipandisha hadhi na kuipa jina la mwasisi wa taifa, Mwalimu Julius Nyerere. Ilianza rasmi Novemba 19, mwaka 2019 na ina ukubwa kilomita za mraba 30,893.

Jina la Selous linatoka kwa Mwingereza mwindaji maarufu aliyeitwa, Frederick Selous, wakati wa kuanzishwa koloni la Afrika ya Kusini na Mashariki. Aliuawa katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia.

**BAIOANUAI NYETI**

Ofisa Uhifadhi Mwandamizi wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (TANAPA) Seth Mihayo, anasema hifadhi hiyo ni ya kwanza kwa ukubwa na imesheheni baioanuai za kipekee, ikilinganishwa na nyinginezo nchini.

Anataja baioanuwai hizo za muunganiko wa vitu mbalimbali, ikiwamo uoto pekee wa asili, mito, mabwawa, maziwa, miinuko na mabonde yanayofanya viumbe hai, wakiwemo wanyama, ndege, wadadu na anaowaita kitaalamu, reptiliani na amfibiani."

Mihayo anasema, hivyo vinaifanya hifadhi iwe na mandhari ya kuvutia, ikitoa hisia za kipekee kwa wanaozuru hapo hata ukaipa hadhi katika kundi la 'urithi wa dunia' tangu mwaka 1982.

Mihayo anataja vivutio vinginevyo ni wanyama kama Simba, Chui, Mbwa Mwitu, Tembo,Twiga, Nyumbu,Punda milia, Tandala wakubwa, Viboko, Ngiri, Nyani, Swala, Pala na Kongoni.

Anataja kuwapo aina 450 za ndege zimerekodiwa kuwemo, hapo akiorodhesha Tumbusi, Mwewe, Batamaji na Korongo, huku Reptilia waliopo ni Mamba, Kenge, Kobe, Vinyonga na aina mbalimbali za Nyoka.

Ofisa huyo anasema kuna zaidi ya aina 2000 za mimea anayotumia mfano miti ya mibuyu, migude, mpinga, mninga, mkongo, miombo, tagalala, migunga, mikoche ikiwa katika mandhari uwanda wa nyasi, misitu ya miombo na uoto mbalimbali kwenye milima na mabonde.

Vivutio vingine kwa mujibu wa Mihayo, ni kuwapo maziwa makubwa matano akitaja kwa majina; Tagalala, Manze, Siwandu, Mzizimia na Nzelekela, yakiwa na upekee unaoleta mvuto wa utalii maji na michezo ya kuvua samaki.

Pia, ndani ya Hifadhi ya Nyerere, Mihayo anasema ipo mito mikubwa akitaja Rufiji, Ruaha Mkuu, Kilombero, Luwega, Mbalang'andu na Njenje, inayowafanya wanyama na viumbe hai kuonekana kwa urahisi kutokana na mandhari yaliyopo.

**MAENEO KIHISTORIA**

Mhifadhi Mihayo anasema, Hifadhi Nyerere, ina kumbukumbu ya Vita vya Majimaji vilivyoanza mwaka 1905 mpaka 1907, kukiwa kumeundiwa makumbusho yake.

Anasema Vita vya Majimaji, Mtemi Kinjekitile Ngwale, kiongozi wa vita aliwashawishi wenzake kuwaaminisha amechukua maji kwenye moja ya mito iliyopo Hifadhi ya Nyerere, yakiwa na uwezo wa kuibadilisha risasi kuwa maji, akiwajengea imani wamudu kuwapinga wakoloni.

"Mababu zetu wakiongozwa na Mtemi Kinjekitile, walikuwa wanaelekea kushinda, ilibidi wakoloni watumie mbinu ya kuchoma maghala ya chakula ili kuwe na njaa. Kwa hiyo, wazee wetu wamepigana vita hiyo katika eneo la kihistoria lipo Songea, ambalo kwa sasa ndio Hifadhi ya Nyerere " anasema Mihayo.

**VITA VYA DUNIA**

Mihayo anataja historia nyingine ya eneo hilo, kuna kaburi la Afande Kapteni Fredrick Courtney Selous wa Jeshi la Waingereza, aliyekuwa mwindaji na aliuawa na Wajerumani katika vita hivyo vya dunia.

Anasema, kamanda huyo alipendwa sana na wanavijiji waliozunguka eneo hilo na alipofariki waliomba azikwe katika eneo hilo.

Pia, Mihayo anataja kumbukumbu nyingine ni historia ya utumwa wa biashara ya pembe za ndovu, wauzaji walitokea Kusini mwa Afrika wakapita ndani ya Hifadhi ya Nyerere wakielekea Rufiji, Kilwa na Bagamoyo.

Ofisa Mihayo anasema, kuna historia ya utamaduni wa makabila mbalimbali mahali hapo, ikiwemo kuhama kwa Wangindo waliotokea Msumbiji kupitia hifadhini hapo, wakielekea Ifakara wilayani Kilombero, mkoa wa Morogoro.

**SIMULIZI YA IKOLOJIA**

Hifadhi ya Nyerere inatajwa ndiko penye Ikolojia kubwa barani Afrika, yenye Tembo na Simba wengi, Mbwamwitu waliotapakaa na kuonekana kirahisi na sasa ndio wanyama waliopo hatarini kutoweka.

Mhifadhi Mwandamizi anasema, katika miaka ya hivi karibuni iligunduliwa mifupa ya mijusi wakubwa sana walioishi hifadhini humo, sasa inakuwa vivutio vya kitalii.

Kwa mujibu wa Mihayo, mifupa hiyo imepelekwa Berlin, Ujerumani kwa ajili ya kuhifadhiwa na kwamba historia inaonyesha makazi yake halisi yalikuwa ndani ya Hifadhi ya Nyerere.

Mhifadhi huyo kuna anayoitaja 'mti wa ajabu wa asili' ambao ulitumiwa kufanya matambiko na jamii kutatua shida mbalimbali, sasa umekuwa kivutio kikubwa unashindikana kukatwa wakati wa upanuzi wa barabara kwa kile kinachoelezwa 'kuwa na mazingara.'

Mti huo unafahamika kwa jina 'Marula' umekuwa kivutio kwa kuwa katikati ya njia, hata kulazimika eneo hilo kuwekwa barabara pacha, baada ya kushindwa kuondolewa wakati wa upanuzi wa barabara ndani ya Hifadhi ya Nyerere, inayotokea Kijiji cha Mloka wilayani Rufiji, mkoa wa Pwani.

Mihayo anaeleza wakati wa upanuzi huo wa barabara, licha ya kutumika vifaa vya kisasa kama ma-greda ya kukata miti mikubwa, ilishindikana kukatika na vifaa hivyo viliishia kuharibika, mti ukibaki.

"Wakati wa utengenezaji barabara, walipokuwa wakijaribu kuukata ili kupitisha barabara, ilishindikana kutokana na vifaa vyote vikiwemo magreda vilivyotumika kukata yakaharibika, ikiwa ni pamoja na wahusika kupotea kimazingara. Hivyo, umepewa jina la mti wa ajabu," anaeleza Mihayo.

Anasimulia hata walipoleta mitambo mingine ngazi ya juu zaidi waondoe mti huo, ilishindikana navyo vikaishia kuharibika, hata makandarasi wakalazimika kuacha eneo penye mti kuwa katikati, barabara hiyo ikitengenezwa pacha kuukwepa mti.

Mihayo anasema baada ya kufanyika utafiti wa kihistoria, kukabainika kulikuwapo vijiji kipindi cha nyuma hifadhi, ikiwamo kijiji cha Mloka na mahali hapo kukafanyika mambo ya 'mizimu' na matambiko na ili kuuenzi, wakaamua kuuacha mti huo uwe sehemu ya kivutio cha utalii.

**MWENYEJI ASIMULIA**

Mohamed Haule, ni mkazi wa kijijini Mloka, Rufiji kilichoko jirani na hifadhi hiyo, anasimulia kuwa mti huo wa ajabu umekuwa ukisababisha baadhi ya watu wanaofika katika maeneo hayo kufanya shughuli tofauti na matambiko, ikiwamo kuchoma mkaa, wakapotea katika mazingira ya kutatanisha.

"Katika kipindi cha nyuma, yupo mtu mmoja aliienda katika maeneo ya mti huo kwa ajili ya kukata miti na kuchoma mkaa, lakini alipotea kwa muda wa siku kadhaa akiwa anazunguka tu maeneo hayo hayo, mpaka wana kijiji walipopata taarifa ndio wakaenda kumtafuta na kumpata, lakini alikuwa haelewi anakokwenda," anasema Haule.

Pia, kuhusu kushindwa kutolewa mti huo wakati wa upanuzi wa barabara, Haule anasema kwamba yeye binafsi alishuhudia magreda hayo yalivyoshindwa kung'oa mti huo na kuishia kuharibika katika namna tata, hivyo ikalazimika mti huo kuachwa katikati ya barabara.

- ***Soma makala zaidi ya Hifadhi Nyerere kesho.***

MAZINGIRA

# Misukosuko ya mabadiliko tabianchi duniani, nini somo kwa Watanzania?

**Na Pankras Luoga**

HADI sasa umefika wakati takriban asilimia kubwa ya watu wana taarifa kubwa na ama kufahamu au kushuhudia uwepo wa ongezeko kubwa la matukio, yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi duniani.

Pamoja na kuibuka kimbunga na mafuriko katika nchi za Marekani, China, Pakistani, Sudan, Uganda na ukame mbaya kuwahi kutokea nchini Kenya na Ethiopia taarifa za vyanzo vya matukio hayo, zinaonyesha kuna uwezekano mkubwa, zinasababishwa na mabadiliko ya tabianchi duniani.

Umoja wa Mataifa umekusanya nchi mbalimbali duniani nchini Misri, ukiwamo ujumbe wa Tanzania kujadili hali ya mazingira na joto duniani inayoongezeka kila kukicha, athari zake na hatua za kuchukuliwa.

Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa mdau mwandamizi amehudhuria na kuwasilisha mada yake nini kifanyike, wiki iliyopita akiwa mdau mwandamizi katika siku za awali za mkutano huo uliokoma wiki hii.



Hali ya foleni ya maji mkoani Dodoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mabadiliko hayo yanatokana na shughuli za kibinadamu, ikiwa ni pamoja na ukataji ovyo miti, kuongezeka idadi ya viwanda na vyombo vya usafirishaji vyenye kutoa na kuongeza hewa ya ukaa, uchomaji moto ovyo, uendeshaji kilimo kisichozingatia uoto wa asili endelevu, matumizi ya baruti, sumu na mabomu katika kuendesha shughuli za uvuvi duniani.

Hivyo vyote vinatajwa kuleta uharibifu mkubwa wa mazingira duniani na kuchangia kutokea madhara makubwa kwenye maisha ya binadamu, yanayoonyesha uwezekano wa kutokea majanga mengine, ikiwa ni pamoja na mlipuko wa magonjwa ambayo hayajawahi kutokea duniani kama vile corona.

Itakumbukwa taarifa za kimbunga katika jimbo la Florida nchini Marekani na ukame nchini Kenya, zinasema hayo ni matukio mabaya kuwahi kutokea katika kipindi cha takribani miaka 40 iliyopita.

**HALI ILIVYO NCHINI**

Nchini Tanzania, tayari wataalamu wameshatoa taarifa za uwepo wa mvua za wastani na chini ya wastani, kwa maana maeneo mengi nchini yatakuwa na upungufu wa mvua mwaka huu.

Wananchi wengi wameipokea taarifa hiyo kwa mshtuko na hofu kubwa, hasa ikizingatiwa nchi imekuwa katika jitihada kuhakikisha inajitosheleza na kujinasua dhidi ya athari za janga la Uviko 19, linalotikisa dunia nzima kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Hayo yanaendana na gharama ya ki - maisha ya watu zaidi ya milioni 14, na zaidi ya watu 800 nchini kwetu wakiguswa na hata imeathiri kwa kurudisha nyuma maendeleo katika nyanja zote za maisha, yaani kiuchumi, kijamii kuanzia elimu, afya hadi mahusiano na kusonga kwenye utamaduni na siasa.

Ikiwa bado alama za madoa yake yapo kwenye maisha ya jamii, ikileta ugumu kwa wananchi, kunapokewa taarifa mbaya ya kuwepo tishio lingine lenye kuathiri ustawi wa jamii.

Hilo linaleta dai la nguvu za kiserikali kupitia wizara zinazohusika kama vile maliasili na zinazohusika na maliasili, pia mazingira kuweka nguvu zaidi katika kutoa elimu, kuchunguza na kufanyika tathmini ya kina kufuatilia kwa karibu na kitaalamu, juu ya mabadiliko ya tabianchi kitaifa.

Ni dhana inayotajwa itasaidia kuibua taarifa kamili na ya kitaalamu, inayoaminika zaidi kuhusu mabadiliko hayo na kujua athari zake na namna inavyohatarisha maisha ya binadamu na namna jamii inavyoweza ikapunguza na kujikinga na majanga hayo.

Mfano tajwa ni katika aina za miti ya kupanda maeneo ya vyanzo vya maji, miti ya kupandwa kuzuia upepo, ile ya kuzuia mmomonyoko wa udongo na mafuriko katika maeneo ya makazi.

Kuna watu wengi katika jamii hawajashirikishwa saba katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi na elimu ya madhara yake.

Kasoro inayojitokeza ni kwamba, pale hapatachukuliwa hatua stahiki katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi kidunia, kutakuwapo alama ya kukwama katika kujikomboa dhidi ya athari hiyo ya kimazingira kwa ujumla.

Hatima ya yote inatajwa ni watu katika jamii kila mmoja ana wajibu wa kuhakikisha anafanya tathimini na ufuatiliaji wa mazingira, pia kuchukua hatua mapema, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Baadhi ya hatua zinazotakiwa kuchukuliwa, ni pamoja na kuanza kupanda miti kwa aina wanayoshauriwa na wataalamu kwenye maeneo yao, kulingana na mazingira na mahitajio ya sehemu husika.

**FAIDA GANI?**

Inatajwa, pale kila mmoja katika umma atazingatia angalizo la kuwepo tishio la mabadiliko ya tabianchi katika kipindi kilichopo, kuweza kupambana na mabadiliko ya tabianchi yanayogonga hodi inaleta mageuzi makubwa,

kimantiki, inapofanyika tathimini na ufuatiliaji wa karibu ya mazingira yake, basi mategemeo ni kupatikana faida kadhaa, kuanzia kwa mtu binafsi, jamii, taifa na jumuiya kimataifa.

Kwanza, inaorodheshwa, kuona hali halisi ya maendeleo ya mazingira yake, kugundua mapema mabadiliko yoyote ya tabianchi hata kama ni madogo.

Hivyo, inapata muda wa kufanya marekebisho ya kasoro zinazoanza kujitokeza, ikiwa ni pamoja na kufuata kikamilifu masharti ya kimazingira kama kutokata miti ovyo na kutopanda miti ili kutunza mazingira yanayotuzunguka.

Nafasi ya uwezekano inakuwa pale kila mmoja katika jamii anapofuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa mazingira kupambana na mabadiliko ya tabianchi na mwisho ahakikishe anafanya tathimini na kufuatilia kwa karibu hali mazingira yake yake.

Hapo anakuwa akilinganisha na hali yake ya awali, ili kutambua mapema mabadiliko yaliyoko kimazingira na tabianchi katika eneo lake, ili achukue hatua mapema za maboresho.

Mambo kama vile kuchoma moto ovyo, ukataji miti kiholela, matumizi ya sumu na mabomu katika uvuvi na shughuli nyinginezo za kuharibu mazingira, hazipaswi kupewa nafasi.

***Makala hii ni tathmini binafsi ya kitaalamu ya mwandishi, ambaye ni Mhadhiri Msaidizi katika fani ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya miradi ya Afya, katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili anapatikana kwa simu: + 255 757 645746.***




Wakazi wa Mkata, wilayani Handeni, mkoani Tanga wakihangaikia kupata maji.

AFYA

## DARASA LA MTAALAMU WA MUHAS...

# Vituo afya vilivyo sehemu hatari kwa mgonjwa, anayeuguza, mtoto

**Na Pancras Luoga**



Kinamama wakiwa kliniki.

"Muuguzaji wa mgonjwa aliyekuwa mzima anakufa, halafu mgonjwa aliyekuwa anaumwa anapona na kurudi nyumbani," ni usemi wenye ukweli na unatia simanzi.

Ufafanuzi wa hoja hiyo ya elimu ya umma kwa upande wa afya, unamaanisha kwenye kituo cha afya, zahanati au hospitali kunapatikana magonjwa hatari na baadhi yake magumu kuyatibu, sambamba na gharama kubwa.

Ni kawaida sana kusikia mtaalamu wa afya au mlinzi katika kituo fulani cha afya, akitamka "hairuhusiwi ndugu zaidi ya mmoja wa mgonjwa kuingia ndani kwenda kumwona mgonjwa husika!"

Katika kupokea hoja hiyo, hushangaza kuona wana - ndugu wanakuwa wabishi, wakihisi 'wanabaniwa' na watu wenye 'roho mbaya' kumwona ndugu yao ambaye ni mgonjwa.

Kigumu zaidi ni pale panashuhudiwa ndugu hao huwa na watoto wadogo, baadhi wako mkononi na mgongoni. Hapo, baadhi wana - ndugu wanakuwa wakali na kutumia njia mbadala kuweza kuingia ndani penye wagonjwa wao.

Wengine huwa tayari hata kulaghai kwa namna mbalimbali za hadaa, ili mradi waruhusiwe kuingia ndani ya hospitali kumwona mgonjwa wao.

Japo ndugu hufanya hivyo kwa nia njema wakiamini ni namna ya kuonyesha kujali, ushirikiano na upendo wao kwa ndugu ndani ya kipindi anachopitia changamoto za kiafya, lakini wataalamu wa afya nao wana nia njema zaidi ya ulinzi wao kiafya.

**KILICHOKO NDANI**

Msingi mkuu hapo ni kwamba, sura kuu ya hatari imejificha katika kitendawili, penye kutoa huduma za afya kuna hatari kubwa zaidi, kwani ndiko penye kila aina

ya vijidudu, vikiwemo vya magonjwa yanayoitwa 'nosokomia'. Kwa kifupi, ni yanayopatikana maeneo ya huduma za matibabu.

Pia ni magonjwa yanayombukizwa kwa mtu au mgonjwa na humuingia mhusika kwa kugusana na vijidudu hivyo na inalaezwa, matibabu yake ni magumu.

Ni aina ya madhara yanayojitokeza katika mazingira, pale ndugu wa mgonjwa huingia kwenye kituo cha afya kwa lengo la kumwona anayeumwa wodini

**SURA YA MADHARA**

Nini madhara ya ndugu wa wagonjwa kutosikiliza na kutofuata ushauri huu? Hapo kunatajwa mengi, kwa wanaosikiliza au kushindwa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya.

Baadhi ya athari hizo, zinatajwa kwa baadhi ya ndugu hao kuingia na wadudu wapya toka nyumbani na kumwambukiza mgonjwa.

Pili, ina sura kinyume chake, ndugu hao kupata maambukizi ya magonjwa ya nosokomia na kurudi nayo nyumbani, ambako huenda na hatari ya kuwaambukiza wengine.

Hapo wanaambukizwa, kuna kundi la wazee na watoto, ambao mifumo yao ya kinga iko chini. Wakati huohuo, ni kwamba, namna ya kumtibu mgonjwa huyo ni ngumu na kunahitajika gharama kubwa sana.

Hiyo inajenga maana, pale mwanajamii atakapoambukizwa, basi ina sura ya kuathiri mustakabali wa uchumi wa familia na jamii nzima na kuna wakati,

inasababisha kutokea vifo kifamilia.

Hapo ndipo kuna mazingira yanayozua kitendawili cha anayeuguza mgonjwa anakufa na kumuacha mgonjwa akirudi nyumbani mwenye afya bora.

**NINI CHA KUFUATWA?**

Wajibu wa kwanza kiafya, unatajwa ni kwa ndugu wa wagonnjwa ni lazima waanze kujitathimini na kuelewa kuwa, utaratibu huo wa kuingia mtu mmoja tu kwenda kumwona mgonjwa, ikijumuisha kumpelekea chakula umewekwa kwa nia njema.

Mtazamo mkuu ni kuwezesha kulinda afya zao na jamii nzima, akiwamo ndugu yao anayeumwa. Mfano, hapo unatolewa pale ndugu wa mgonjwa mwenye mtoto mdogo ni vizuri asing'ang'anie kuingia maeneo ya hospitali kumuangalia mgonjwa, isipokuwa kama hakuna mbadala wa kufanya hivyo.

Pia, kuna ushauri kwamba, wagonjwa nao wanaaswa wajitahidi kufuata taratibu zilizoko, kwani zina msaada unaowalinda wao pia ndugu zao kiafya.

Katika mantiki ya kijamii, inatajwa hakuna anayependa kuwazuia wanandugu kumwona mwanao mwenye matatizo ya kiafya na kumpa faraja, ila wanafanya hivyo kwa nia njema ya kutetea usawa wa afya kwa jamii nzima.

Sura kuu ya majumuisho hapo ni kwamba, wahusika wakuu wanapaswa kupewa ushirikiano na jamii ikubali ushauri wao na kuacha kulalamika katika sura wananyimwa fursa ya kuwaona ndugu zao wagonjwa.

**FAIDA INAVYOPATIKA**

Inanusuru ndugu kuambukizana maradhi, na kuwapa fursa wataalamu husika kudhibiti hali ya maradhi tajwa kusambaa kati ya wana ndugu.

Pili, kunatajwa kupunguza uwezekano wa mtu kupatwa magonjwa aina ya nosokomia, ambayo zaidi hupatikana katika maeneo ya kutoa huduma.

Ndani ya mafanikio hayo kudhibiti maambukizi, kwa jamii nayo inajikuta imeokoa gharama kubwa ambazo ingetumia, endapo ingekabiliwa na kusambaa, maradhi hayo miongo mwao.

Hilo linabebesha somo kuu la wagonjwa na jamii ianze kujitafakari na kufuata taratibu za kuwaona wagonjwa kama zilivyowekwa na wataalamu wa afya katika vituo husika vya kutoa huduma, huku ndugu wenye watoto wadogo wajitahidi kutoenda maeneo ya kutoa huduma hizo na watoto wadogo.

Kiafya, watoto mifumo yao ya kinga haipo imara kukabili mapambano na aina za magonjwa, ikiwamo nosokomia.

***Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi katika fani ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya Miradi ya Afya, katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili (MUHAS) na anapatikana kwa simu: + 255 757-645746.***



Wagonjwa wakiwa katika wodi na baadhi ya waliofika kuwaangalia, katika hospitali ya wilaya iliyoko mkoani Songwe. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

# Mganga Mkuu Moro: Mkoa tumevalia njuga chanjo, baada ya rekodi ya kusuasua

**Na Christina Haule, Morogoro**

MKOA wa Morogoro hadi sasa unatajwa katika lawama kwamba upo katika orodha ya chini zaidi katika chanjo kitaifa dhidi ya ugonjwa Uviko 19.

Pengine, daraja hilo la kusuasua, linaanzia kwenye kutojua maana ya dhana 'kuchanja.' Hapo ndipo darasa la Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Dk. Kusirye Ukio, kuhusu chanjo linapochukua nafasi akisema "kinga juu ya ugonjwa unaokusudiwa, ambao ukimpata mtu unaweza kuwa na madhara makubwa."

Dk. Ukio anaendelea: "Chanjo kazi yake inatayarisha mwili kabla hujakutana na kiumbe ambacho kinasababisha madhara makubwa kwake. Unapokuwa tayari unakutana nacho, mwili tayari unakuwa na kinga ya kutosha kuweza kukabiliana nacho.

"Chanjo inazuia madhara yanayotokana na magonjwa ambayo ni hatarishi kwa jamii, kama corona ambayo yana madhara makubwa. Kwa hiyo, kuliko kumeza dawa ambayo inatibu kirusi, ni vizuri kuutayarisha mwili na kama kuna madhara yanayotokana nayo, basi hayawi makubwa kama asiyepata."

Kutokana na hali hiyo, anajenga hoja yake kutoa rai kwa umma na kimkoa kujitokeza kupata chanjo mbalimbali zinazopitishwa na serikali, ikiwamo ya maradhi Covid -19, ili kutayarisha miili kupata kinga za kutosha kukabiliana na magonjwa hatarishi.

Anarejesha tathmini ya wagonjwa wa Uviko - 16 kwa sasa ni wachache, pia madhara yake hayako juu, kama ilivyokuwa awamu iliyopita ya mlipuko huo, ambayo yameipatia serikali usumbufu na gharama kubwa kiserikali.

Sasa anasema chanjo imeokoa maisha ya watu na kupunguza gharama za tiba na kuboresha afya ya jamii.

**HALI YA MORO**

Anasema hadi sasa, hospitali mkoani hazijapokea ama wagonjwa au waliodhurika nao. Vilevile anagusia kwamba, mkoa haujapata taarifa ya ama vifo au waliodhurika na chanjo hizo.

Mtaalamu huyo anasema, wanaendelea kupokea majibu ya tathmini ya chanjo na madhara yake, huku akihamasisha watu kujenga tabia ya kutoa taarifa pale wanapopata madhara husika.

Dk. Kusiriye anatumia fursa hiyo, kuwataka wanaosambaza uvumi hasi dhidi ya ugonjwa huo, kuacha upotoshaji na wasimamie taarifa sahihi, ikianzia na kupata ufahamu wa jambo husika kwa kina.



Watumishi wa Idara ya Afya, akiwemo Mratibu wa Chanjo Dk. Masumbuko Igembya (kushoto) wakifuatilia kikao kuhusu Uviko-19 inayotolewa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Urio Kusirye (hayupo pichani).

Kwa mujibu wa Dk. Kusirye, serikali ina utaratibu wa kuthibitisha usalama wa ama dawa au chanjo inayoenda kutumika kwa wananchi, na daima haiwezi kujikita katika kile chenye madhara.

Hapo anatoa elimu, akifafanua ni kawaida kuwapo uwezekano wa kuwa na madhara madogo kwa wanaochanja, kama vile kuumwa kichwa, homa kupanda kwa muda mfupi, lakini hata penye madhara hayafikii hatua ya kifo au madhara makubwa kama, baadhi ya watu wanavyoamini.

Kuhusu aina za chanjo, Dk. Kusirye anaainisha kwamba zipo za aina nyingi akiorodhesha zinazidi 10, katika makundi kama ya watoto wadogo; pia wa umri wa shule; saratani ya shingo ya kizazi; ugonjwa wa manjano; kinamama wanaohudhuria kliniki, akinena nyingi zina gharama kubwa kwa serikali.

**MRATIBU CHANJO**

Mratibu wa Huduma za Chanjo Mkoa wa Morogoro, Dk. Masumbuko Igambye, anasema tangu wameanza kutoa huduma chanjo mwaka jana, mpaka sasa hawajawahi kupata mkasa unaohusu madhara.

Hapo Dk. Igambya anazama katika hoja yake, akigusa maeneo ya kitaalamu kama mabadiliko ya kijenetiki au kibaiolojia kama vile mtu kuzubaa.

"Nathibitisha kwamba hakuna kisa au visa vilivyoripotiwa kwa mtu kubadilika tabia za kimaumbile au za kijenetiki, kwa sababu tu alipata chanjo ya Uviko-19 na mimi mwenyewe ni mmoja wa niliyepata chanjo na sasa nina mtoto wa miezi sita" anasema.

Dk. Igembya anasema, uzinduzi wa chanjo za Uviko-19 mkoani Morogoro ulifanyika mnamo Agosti 3, mwaka jana katika vituo 26 vya awali na baadaye idadi yake kufika vituo 367.

Anasema walengwa wenye sifa za kupata chanjo hiyo mkoani Morogoro wapo 1,544,177 watu wazima umri unaoanzia miaka 18, akioanisha na sensa ya awali ya mwaka 2012.



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Urio Kisirye, akizungumza na watumishi wa Idara ya Afya, kuhusu utekelezaji wa chanjo mkoani hapa. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE.**

Dk. Igembya anasema hadi kufikia Oktoba 31, mwaka huu, mkoa umefanikiwa kuchanja watu 1,021,581 ambao ni sawa na asilimia 66 ya malengo ya mkoa, hivyo kuna watu 520,000 wasiofikiwa na huduma hiyo ya chanjo.

Anasema, dira iliyoko kimkoa ni kuhakikisha kila mlengwa mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea anapatiwa mahali aliko, pasipo kuathiri utendaji wake wa kazi wa kawaida, ukienda sambamba na elimu ya afya, pia kuhamasisha tahadhari ya mikusanyiko ya umma, mfano sokoni na kwenye nyumba za ibada.

Dk. Igembya anatoa wito kwa wakazi mkoa wa Morogoro kujitokeza kupata huduma za chanjo katika vituo vyote vya kutolea huduma za chanjo za kawaida vilivyopo mkoani hapo, huku wasioweza kufika wakiendelea kufuatwa mahali walipo.

**KUTOKA NGO**

Mkurugenzi wa asasi isiyo ya kiserikali inayoshughulika na elimu kwa jamii (DIRA Organization -DIRA) Erasmo Tullo, anaishauri serikali kuona umuhimu wa kuzishirikisha asasi za kiraia kutoa elimu hiyo kwa jamii, ambayo ni muhimu kwa afya ya umma.

Tullo anasema suala la chanjo ya Uviko-19 ni mtambuka kwa jamii ambalo linapaswa kupewa kipaumbele ili kuona umuhimu wa kujikinga na kuwa salama wakati wote.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Afya, hadi Agosti 14 mwaka huu, nusu ya Watanzania walengwa walijitokeza kupata chanjo na huku lengo ni kuona angalau asilimia 70 inafikiwa ifikapo mwezi ujao kwa kila mkoa.

Taarifa hiyo inasema, Morogoro ni kati ya mikoa 12 ambayo kiwango cha uchanjaji uko chini hadi mwezi huo Agosti, 2022, ikiwa ni kiashiria cha kuwapo kundi la Watanzania ambao hawakupata chanjo na wanahitaji kuelimishwa na kuhamasishwa kupata chanjo, ili kujikinga na ugonjwa huo hatari.

Taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO), inaonyesha kuwapo kasi ya maambukizi zaidi katika Bara Asia Mashariki na Asia ya Kusini Mashariki, huku nchi kama China ambako ndio chimbuko la janga hilo, kukitajwa mlipuko mwingine hivi karibuni, wakati Afrika, kasi ya maambukizim ikiwa chini.

AFYA

# Vyoo vipya vilivyowaengua wanafunzi wa Kahama kutoka zama magonjwa mlipuko

## • Mahudhurio duni, kuhara damu, matumbo....




Vyoo vya wanafunzi vilivyojengwa katika Shule ya Msingi Nyanhembe, Manispaa ya Kahama. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

**Na Shaban Njia, KAHAMA.**

KUKOSEKANA matundu hayo ya vyoo ya uhakika kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, zilizoko pembezoni mwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, kunatajwa kumechangia sana wanafunzi wengi kukosa masomo yao kwa wakati, huku kukiwepo magonjwa ya mlipuko yanayotokana na uchafu wa mazingira.

Ni hadithi inayoendana na yasiyoridhisha, wanafunzi wanalazimika kujisaidia vichakani, kutokana na vyoo kujaa au idadi kubwa ya wanafunzi kuingia chooni wakati wa mapumziko na kusababisha kukosa sehemu ya kujisitiri wakati huo.

Zao lake sasa inatajwa magonjwa ya milipuko kama vile kipindupindu, magonjwa yanayoathiri mfumo wa mkojo (UTI) na kuumwa matumbo, wanafunzi wakitumia muda mrefu kujitibu kuliko kuwa darasani.

Pia, inatajwa ndani ya halmashauri hiyo, shule nyingi za msingi zina idadi kubwa ya wanafunzi kuanzia 500 na zaidi, huku baadhi yake zikiwa na matundu nane ya vyoo, kati ya hayo manne ya wanafunzi wa kiume na manne ya kike. Walimu nao wanalazimika kutumia vyoo katika makazi yaliyopo jirani na shule.

Mikasa ya namna hiyo, ndipo shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania, liliamua kuingilia kati katika shule tisa za kata ya Iyenze na Kilago Manispaa ya Kahama, vilevile ikajenga chumba cha kubadilisha taulo za kike katika shule tisa

Ni ujenzi unaoendana na kujengwa visima vya muda mrefu vya maji safi na salama na kuyasogeza katika shule hizo za msingi, kuhakikisha vyoo vinakuwa na maji ya uhakika,kwa ajili ya usafi na kujikinga na maradhi ya kuambukiza yatokanayo na uchafu wa mazingira.

Dominick Mbamba, Mratibu Mradi wa World Vision Tanzania, Walyenze- Kilago, anasema wamekuwa wakijenga matundu ya vyoo kwa shule za msingi zenye wingi wa wanafunzi na zinapungukiwa na matundu ya vyoo, lengo ni kuwanusuru na magonjwa ya mlipuko, ili wasome na kutimiza ndoto zao.

Anasema shirika limefanikiwa kujenga matundu nane ya vyoo katika shule Nyanhembe yenye jumla ya wanafunzi 570, kwa ajili ya wanafunzi wa kike na kiume, yakiwa na chumba maalumu cha kubadilishia taulo za kike na sehemu ya kuchoma taulo za kike zilizotumika, ikiwagharimu Sh. milioni 39.3.

Mbamba anasema, matundu ya vyoo ya namna hiyo pia yamejengwa katika shule nane za msingi katika kata ya Iyenze na Kilango. Anazitaja shule hizo ni Kawe, Wame, Ilungu, Gilime, Iyenye, Tulole na Isalenge, zikiwa na mifumo ya huduma ya maji.

"Shule zetu za msingi za pembezoni, vyoo vimechakaa sana na baadhi havifai kabisa kwa matumizi ya wanafunzi wetu na ndio maana sisi World Vision tumekuja na miradi ya kujenga matundu ya vyoo katika shule za msingi kata za Kilago na Iyenze," anasema Mbamba.

**BIMA YA AFYA**

Mbamba anasema, pia wanatarajia kutoa bima za afya ya NHIF kwa watoto 69 wanaotoka katika mazingira magumu na wenye magonjwa sugu, ikiwa na thamani ya Sh. milioni 7.452 ili ziwasaidie kupata matibabu kwa kipindi cha miaka miwili.

Mbamba anasema katika kuwabaini watoto hao, kwa sasa wanashirikiana na serikali za vijiji, watendaji kata na ofisi ya ustawi wa jamii, kupitia mikutano ya hadhara inayofanyika katika vijiji na wanaopendekeza watoto hao ni wananchi wenyewe, hali inayosaidia kusiibuke malalamiko ya upendeleo.

Pia, anaahidi watatoa bima za CHF iliyoboreshwa kwa kaya 300 zenye mazingira magumu sawa na wanufaika 1,800 katika kata za Iyenzena Kilago Manispaa ya Kahama yenye thamani ya Sh. milioni 12 kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Anasema, watatoa vifaa tiba katika kituo cha afya Iyenye na zahanati ya Kilango vya Sh. milioni 20 ili kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba na matibabu kwa wananchi na sasa wanamsubiri Mfamasia wa Manispaa kuwapatia mahitaji na kununua kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

**MWALIMU MKUU**

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyanhembe, Clement Nelson, analipokea hilo kwa bashasha akisema baada ya kujengewa vyoo vya kisasa, wameondokana na hali ya wanafunzi kuugua magonjwa ya mlipuko, ikiwemo kipindupindu, kuhara damu na matumbo wawapo shuleni.

Anasema, shule imejengewa matundu ya vyoo yakiwa na 2.
miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu, akifafanua: "Siku zote tunafahamu inapofikia muda wa mapumziko, iwe ya asubuhi au mchana, kitu cha kwanza wanafunzi hukimbilia chooni kukidhi haja zao. Ilikuwa tabu na wengi walijisaidia vichakani. Sasa hali hiyo imetoweka baada ya kupata msaada wa vyoo vya kisasa."



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyanhembe Clement Nelson (wa kwanza kulia), akionyesha choo kilichokuwa kikitumiwa na wanafunzi wa kiume awali shuleni hapo.

**WAKUU SERIKALI**

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama Robert Kwela, anaahidi katika bajeti ijayo ya mwaka wa fedha, halmshauri yao itahakikisha inatenga fedha za kuweka mifumo ya maji katika baadhi ya vyoo visivyokuwa na maji vilivyojengwa na shirika hilo, ili kukamilisha namna ya kujihami dhidi ya magonjwa ya mlipuko kwa wanafunzi.

Katibu Tawala wa Kahama, Timothy Ndanya, anawataka wananchi kuitunza miradi hiyo, ili kuhakikisha inawanufaisha wanafunzi ipasavyo na kuondokana na maradhi ya mlipuko ya kuumwa tumbo, pia kupoteza muda wakati wa matibabu, badala ya kuwa darasani.

# Jifunze mambo matano tangu kuzuka janga la Uviko duniani

**Na Mwandishi Wetu**

SASA ni miaka miwili tangu nchi kukumbwa na janga jipya la Uviko 19 , pale Shirika la Afya Duniani (WHO) lilipotangaza rasmi kwamba mlipuko wake kuwa janga la kimataifa.

Ilikuwa Machi 11, 2020 dunia ilipobadilika, kwa kiwango kikubwa cha maradhi hayo. Kitaalamu kunaelezwa kuwepo mambo matano ya kujifunza, ikiendana na maajabu kutoka simulizi ya utengenezaji chanjo, chanjo ya kwanza ya Uviko 19, ilichukua miezi 11 kutengenezwa:

Mosi, chanjo za mRNA: Ni mara baada ya janga kuanza, watafiti walianza mbio kutengeneza chanjo kukimu watu dhidi ya Uviko-19.

Baadhi ya kampuni za dawa ziliamua kutumia aina ya teknolojia ambayo matokeo yake hayajawahi kutumika kutengenezea chanjo, iliyoidhinishwa kwa matumizi ya binadamu – mRNA, hatua hiyo ilisaidia.

Ni mchakato uliofanya kazi kwa kuchukua kipande kidogo cha hisia za kimwili unaoitwa mRNA na kuipaka kwenye mafuta. Hapo mfumo wa kinga ya mwili, ukaweza kujifunza kutambua uwe tayari kushambulia virusi halisi vya Covid-19, iwapo utaambukizwa

Pili, Uviko -19 ukasambaa kupitia hewa kuliko ilivyofikiriwa awali: Nchi nyingi zikabadili ushauri wa kuvaa barakoa na kuagiza zivaliwe katika baadhi ya mazingira.

Miezi minne baada ya mlipuko




Mtaalamu akiandaa sindano ya chanjo ya Uviko 19. **PICHA: MTANDAO.**

wa Uviko-19 ikatangazwa na WHO kupitia ujumbe kwenye mtandao wake wa Twitter ukisema "Covid 19 haiambukizwi kupitia hewa."

Wakati huo wataalamu wa WHO hawakuwa wakiwashauri watu kuvaa barakoa, Mkurugenzi Mtendaji wa Mpango wa Dharura wa Afya wa WHO, Dk Michael Ryan, akisema: "Hakuna ushahidi mahususi unaoashiria kuwa uvaaji wa barakoa una faida yoyote."

"Hatushauri utumiaji wa barakoa, pengine ujiskie mgonjwa," akaongeza Maria Van Kerkhove, kiongozi wa kiufundi wa maaradhi hayo wa WHO na baada ya shirika hilo kujifunza hilo,anasema watu wanapaswa kuvaa barakoa sehemu ya kawaida karibu wanapokuwa karibu na wengine.

Hapo ni baada ya kuwapo ushahidi haiambukizwi pekee kupitia matone ya mate au kamasi, pia hewani baada ya mtu kukohoa au kupiga chafya, au kugusa sehemu yenye virusi.

WHO inafafanua kwamba inaweza pia kuenea kupitia chembe ndogo zaidi zinazoweza kubaki hewani kwa muda mrefu zaidi. Ikabadilisha ushauri wake kwamba Uviko 19 unaambukizwa kupitia kuvuta hewa yenye virusi.

Kunawa mikono na kuosha maeneo yanayoguswa na watu wengi bado ni jambo linalotiliwa mkazo, lakini cha msingi ni kuvaa barakoa katika chumba kilicho na nafasi ya kuingiza hewa safi.

Tatu, kazi zahamia nyumbani: Dhana iliyopo sasa ya mlipuko wa Uviko 19, jamii inaweza kutumia muda wake kwenye simu za video. Umma wa watu kote duniani wamelazimika kufanya kazi nyumbani wakati wa janga la ugonjwa huo.

Ni kitu ambacho hakingewezekana kiufundi miaka michache iliyopita, lakini Uviko 19 umeonyesha kwamba inawezekana, hali inayoweza kubadilisha namna mamilioni ya watu wanavyofanya kazi.

Kampuni kubwa za mitandao ya kijamii ziligonga vichwa vya habari kote duniani Mei 2020 iliposema: "Wafanyakazi wa Twitter sasa wanaweza kufanya kazi wakiwa nyumbani milele miezi michache iliyopita imethibitisha kuwa tunaweza kuifanya kazi hiyo."

Kura za maoni 1,200 iliyofanywa na kampuni ya utafiti ya kiteknolojia, ilionyesha kuwa asilimia ya wafanyakazi wanaofanya kazi ya kudumu nyumbani kote duniani, iliongezeka mara mbili mnamo 2021.

Nne, janga Uviko 19 liliwaathiri walio hatarini zaidi katika jamii; Watu kutoka jamii zisizo na uwezo waliathiriwa sana na Uviko 19.

Huko Uingereza, utafiti katika Benki ya Biobank ya Uingereza uligundua sehemu iliyoathiriwa zaidi ya nchi ni asilimia 11.4 ya watu walikuwa walioambukizwa, na kutoka maeneo duni walikuwa asilimia 7.8%.

Katika nchi nyingi, taarifa na takwimu sahihi kuhusu madhara ya Uviko 19 hazipo, lakini kote duniani moja ya tofauti kubwa zaidi iliyojitokeza ni viwango vya chanjo.

Tano, hadi sasa tuna uhakika wa jinsi, au kama, janga la Covid-19 litaisha: Wazo sasa ni ikiwa watu watapata usugu dhidi ya ugonjwa huo, virusi vitakuwa tishio kidogo.

Pia, imebainika mifumo ya jamii ya kinga inapungua kadri muda unavyosonga na ndio maana kuna chanjo za nyongeza ni muhimu.

Kulingana na Profesa Shabir A Madhi, Mkuu wa Kitivo cha Sayansi ya Afya, akiwa mtaalamu wa Chanjo katika Chuo Kikuu cha Witwatersrand, Afrika Kusini, mwitikio wa kinga baada ya kuambukizwa au chanjo huchukua takriban miezi sita hadi tisa.

Ingawa chanjo ni kinga dhidi ya ugonjwa mbaya, zilizo bora hazionekani kuwazuia watu walioambukizwa Uviko 19 kuwaambukiza wengine.

Hiyo ni kwa sababu virusi vimebadilika kwa haraka na aina nyingine ya Uviko 19, inayoweza kuambukizwa kuibuka na huenda ikawa vigumu kudhibitiwa kwa chanjo.

***Kwa mujibu wa habari za kimataifa.***


---

## CHEMSHABONGO NA -00 23 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. kiungo cha kutembelea
5. nasaba 8. kitu cha duara kinachofanya gari itembee
10.tayarisha 11.gari kubwa ya abiria 13.ghasia 14.vunja kanuni za nchi 15.Rome ni mji mkuu
16.safisha mwili 18.minyoo ya kuvulia samaki 20.dakika 60
22.shimo la kuzikia wafu 23.njiwa
24.Bamako ni mji mkuu 25.heshima


Chini:
1. askari wa akiba
2. toa sauti ya kuonyesha kukataa
3. lugha ya Pakistani
4. utoaji uhai kiumbe 5. masafa
6. kukataa kutii sheria za nchi
7. jicho 9. tia hatarini
12.itikadi ya kuendesha uchumi na utamaduni wa nchi
17.taifa lililoasisiwa na Kwameh Nkrumah 18.sayari tunayoishi
19.dhihirishia kitu kilivyo
20.mdudu mdogo jamii ya chungu
21.mwanzo



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

KAAKAA
MAANANI
OSAMA
PAKA
KASHA
ARUSI
KISIWANI
MAISHA
AIBIKA
SHAA
MAISHA
MZAHA
MADIWANI
KINGA

OKA
TAI
AKA
MDAU
DANI
DHAKA
ARIA




Majibu toleo lililopita





## HABARI MBEYA

# Mil. 100/- zakamilisha ujenzi zahanati ya Itezi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

ZAIDI ya Sh. milioni 100 zimetumika kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya Itezi jijini hapo, fedha zilizotolewa na serikali, michango ya wananchi pamoja na Taasisi ya Tulia Trust.

Spika wa Bunge la Tanzania ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson jana alizindua zahanati hiyo na kudai kuwa itapunguza mzigo kwa Hospitali ya Igawilo ambayo inahudumia wagonjwa kutoka maeneo mbalimbali ikiwamo kata ya Itezi.

Alisema pia serikali imewezesha ujenzi wa vituo vya afya katika maeneo mengine kikiwamo cha Iyela, Iduda na Ndanyela.

"Serikali ilitoa fedha zaidi ya Sh. bilioni 11 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wazazi Meta kusaidia huduma za mama na mtoto, tulipokea Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Igawilo ambayo imepandishwa hadhi," alisema Dk. Tulia.

Aliwahamasisha wananchi kuendelea kushiriki kwenye shughuli za maendeleo kwa kuanzisha na kubuni miradi mbalimbali ya pamoja ambayo itawawezesha kujikwamua kiuchumi.

Alisema aliianzisha Taasisi ya Tulia Trust kwa lengo la kuwasaidia wakazi wa Jiji la Mbeya kupata mikopo yenye riba nafuu ili kutimizi malengo yao kama vile mikopo ya bodaboda, bajaji na mitaji ya shughuli za ujasiriamali.

Meya wa Jiji la Mbeya, Issa Mohammed, alisema kupitia mapato ya ndani wanaendelea kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya na zanahati.

Alisema miongoni mwa zahanati ni pamoja na Itezi ambazo kimejengwa kwa mapato ya ndani kwa kushirikiana na wadau wengine.

Kuhusu mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani alisema wanaendelea kukusanya na kuvikopesha vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

# Aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi Mbeya aachiwa huru

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, imemwachia huru aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Dk. Samwel Lazaro, baada ya ushahidi wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha ipasavyo tuhuma alizokuwa akikabiliwa nazo tangu mwaka 2017 za kughushi, kuwasilisha nyaraka za uongo na kutumia madaraka yake vibaya katika ujenzi wa uzio wa soko la Mwanjelwa jijini hapo.

Hukumu ya kesi hiyo ya uhujumu uchumi ilitolewa baada ya kusikiliza maelezo ya ushahidi wa pande zote mbili za shauri hilo ikiwa ni pamoja na kufungwa kwa ushahidi wa Jamhuri Septemba, mwaka huu na baadaye ushahidi wa utetezi.

Hakimu Mkazi wa Mahakama Kuu ya Mbeya, Andrew Scout, alitoa uamuzi wa kumwachia Lazaro baada ya ushahidi wa upande wa mashtaka kudaiwa kuwa na kasoro na kutia shaka mshtakiwa kutenda kosa la kughushi nyaraka na kutumia madaraka yake vibaya kama Jamhuri ilivyodai licha ya mshtakiwa kukana kuhusika na shauri.

Ushahidi dhidi ya kiongozi huyo wa zamani wa Jiji la Mbeya kuhusika na makosa hayo uliongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wakili Sospeter Tyeah, ulielezwa na Hakimu Scout kwamba umetia mashaka kwa kuwa hakuna shahidi aliyeiambia mahakama kwamba mkurugenzi huyo aliruhusu ujenzi kabla ya bodi ya zabuni.

Akirejea ushahidi huo, Hakimu Mkazi Scout, alisema shahidi namba tano wa upande wa mashtaka alionesha wazi kwamba katika ujenzi huo wa uzio wa Soko la Mwanjelwa, ulizingatia kanuni na taratibu za kitaaluma na mkandarasi hawezi kuanza ujenzi kabla ya kupewa mchoro wa ramani ambao uliwasilishwa kwa mkandarasi wa kutoka kwa Halmashauri ya Jiji tofauti na madai ya Jamhuri kwamba ujenzi ulianza kabla bodi haijaruhusu.

Kuhusu madai ya Dk. Lazaro kughushi nyaraka, mahakama hiyo ilisema ilipata mashaka na kutendeka kwa kosa hilo kwa kuwa mshtakiwa alikiri sahihi zote kuwa za kwake na zilifuata utaratibu na hakukuwa na sahihi yoyote iliyoelezwa na Jamhuri kwamba ilifojiwa, kufananishwa wala kubishaniwa mahakamani hapo.

Hata hivyo, katika utetezi wake, Dk. Lazaro ambaye kwa sasa ni mtumishi jijini Dodoma, alikana kutenda makosa yote matatu ya kughushi nyaraka, kutumia madaraka yake vibaya na kutoa maelezo ya uongo akisema kila kitu kilifanyika kama inavyotakiwa kwa kuzingatia kanuni na taratibu za ujenzi na ununuzi.

Scout alirejea kuwa kama mahakama ilivyosema baada ya uchunguzi kufanywa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), hakuna mahali walipokosoa ujenzi huo kwenda kinyume au kutoendana na thamani ya fedha zilizotumika kujenga uzio huo wa soko.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Mkazi wa Mahakama Kuu ya Mkoa wa Mbeya, Andrew Scout, alisema amemuachia huru Dk. Lazaro pamoja na hukumu hiyo mahakama imeweka wazi haki ya kukata rufani kwa upande usioridhika.



Wakazi wa Mtaa wa Itezi Mashariki, Kata ya Nsalaga jijini Mbeya, wakiendelea kuokoa mali zilizokuwa kwenye nyumba ya Mchungaji wa Kanisa la Baptist Itezi, Daniel Mwandenga, ambaye nyumba yake iliteketea kwa moto juzi. Hakuna mtu aliyejeruhiwa katika tukio hilo.
**PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TARI yaanza kusambazia wakulima mbegu bora alizeti

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), ikishirikiana na wadau wa kilimo Nyanda za Juu Kusini, imeanza kusambaza mbegu bora ya alizeti kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo kufanikisha azma ya serikali ya taifa kujitosheleza kwa mafuta ya kupikia.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Mradi wa uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora za alizeti nchini, ambaye ni mratibu wa zao hilo, Frank Reuben, alisema usambazaji unaanza ili kuwahi msimu wa kilimo ambao unatarajiwa kuanza mwezi huu katika maeneo mengi nchini.

Alisema kwa sasa alizeti inalimwa katika mikoa yote nchini, kiwango kikubwa cha mbegu kinahitajika ili kukidhi mahitaji ya wakulima wa zao hilo nchini.

"Tunahitaji zaidi ya tani 50 za mbegu ya alizeti kwa ajili ya wakulima wote wa zao hilo nchini, hivyo ni lazima tuwe na mkakati madhubuti ya kufikisha mbegu hizo ili wakulima waweze kulima zao hili kwa wakati," alisema Reuben.

Alisema ili kuwafikia wakulima wengi zaidi na kwa wakati ni lazima serikali ishirikiane na wadau wengine wa kilimo.

Alisema kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, kazi ya uzalishaji wa mbegu bora ya alizeti inafanywa na Kampuni ya Highland Seeds Growers ambayo imepewa jukumu la kuzalisha zaidi ya tani 21 kwa ajili ya wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Pia mbegu zinazosambazwa kwa wakulima zimefanyiwa utafiti na kuthibitika kuwa ni bora na zina uwezo wa kuleta tija kubwa ya upatikanaji wa mafuta ya kupikia nchini. Alisema endapo kasi ya kilimo cha alizeti itaendelea kama ilivyo sasa upo uwezekano mkubwa wa Tanzania kuongoza duniani kwa uzalishaji wa zao hilo.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Kampuni ya Highland Seeds Glowers, Elizabeth Mallya, alisema kampuni hiyo imejiandaa vyema kutimiza wajibu wake wa kuzalisha mbegu za kutosha kwa ajili ya wakulima.

Alisema mbegu za alizeti zinazozalishwa na kampuni hiyo zitawafikia wakulima kwa gharama nafuu zaidi ikilinganishwa na zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.



# Waziri akiri matumizi hafifu ya utafiti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohammed Mussa, amesema bado kuna msukumo mdogo wa kufanya utafiti, kusambaza matokeo na kuyatumia.

Akizungumza juzi jijini hapo kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwenye kongamano la tatu la maendeleo ya biashara lililoandaliwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), alisema bado nchi imejenga utamaduni wa kufanya utafiti na ni jukumu la wataalamu wanaokaribia kustaafu pamoja na wale wanaofanya shahada za uzamivu.

"Lazima tuwe na mikakati ya pamoja ya kutayarisha watafiti tangu ngazi ya awali. Mataifa yanayoyoendelea yamekuwa yakitumia asilimia kubwa ya pato la taifa kushughulikia masuala ya utafiti.

"Mathalani mwaka 2019 taifa la Israel lilitumia asilimia 4.9 ya pato lake huku Jamhuri ya Korea yenyewe ikitumia asilimia 4.6 kwa ajili ya utafiti kwa masuala ya maendeleo ya teknolojia," alisema.

Waziri huyo alisema hakuna hata taifa moja la Afrika ambalo lilitumia zaidi ya asilimia moja ya pato lake la taifa kwa ajili ya utafiti na kukuza ubunifu na uvumbuzi katia masuala ya maendeleo ya teknolojia.

Awali, Mkuu wa Chuo cha CBE, Prof. Emmanuel Mjema, alisema kongamano hilo linazindua matokeo ya utafiti mbalimbali uliofanyika ndani na nje ya CBE.

"Miongoni mwa tafiti (utafiti) zilizofanywa (uliofanywa) ni changamoto za kurasimisha shughuli za wafanyabiashara wadogo, utambuzi wa fursa za ujasiriamali Jiji la Dodoma na matumizi ya simu janja katika kurasimisha biashara za machinga. Tafiti hizi zimesaidia wafanyabiashara wadogo kutambuliwa kukuza mitaji yao pamoja na kuchangia pato la taifa," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Erick Shigongo, alishauri serikali kuanzisha mfuko wa taifa wa ubunifu ambao utasaidia watu kufanya utafiti na kuzalisha bidhaa.

Alisema taifa lolote ambalo haliwekezi katika ubunifu haliwezi kukua na kwamba Tanzania ina wabunifu wengi ambao wataibadilisha nchi ikawa kituo (hub) cha teknolojia barani Afrika.

Shigongo alisema wako vijana wengi wabunifu lakini wanashindwa kusogea mbele kwasababu mitaji yao ni midogo hivyo uvumbuzi wao wameuweka ndani.

Akitoa mada kuhusu uchumi wa buluu, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Prof. Mohammed Makame Haji, alisema rasilimali zilizoko nchini hazijapewa msukumo mkubwa na kwamba kuna maeneo mengi ambayo yanaweza kutumika katika kukuza uchumi na kuibadilisha Tanzania kiuchumi.

Alisema miongoni mwa rasilimali hizo ni uchumi wa buluu na nchi inatoa kipaumbele katika uvuvi, kilimo cha majini, utalii na usafirishaji na kutengeneza ubunifu katika hatua mbalimbali zinazotumika katika maendeleo.

Prof. Haji alisema katika Bara la Afrika, kuna mataifa 54 na 38 kati ya hayo yapo kwenye maeneo ya Pwani ikiwamo Tanzania lakini bado yanajulikana kama mataifa yanayoendelea na kushauri kipaumbele kitolewe kwenye uchumi wa buluu kwa kuwa unalipa.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (katikati) na Ofisa Mkuu wa Biashara wa benki hiyo, Boma Raballa, wakipiga makofi wakati wa uzinduzi rasmi wa mfumo mpya wa kisasa utakaowawezesha mawakala wa benki hiyo kutoa huduma kwa urahisi zaidi kupitia simu janja jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Taka kuchakatwa kunufaisha wakulima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imeingia mkataba na Kampuni ya Hydro Craft Power Africa ya Zimbabwe kwa ajili ya kuchakata taka ili kubadilishwa kuwa mbolea.

Meya wa Jiji hilo, Prof. Davis Mwamfupe, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua Wiki ya Usafi wa Mazingira iliyoanza jana na inatarajiwa kufikia kilele Novemba 19, mwaka huu, kwa kufanya usafi katika soko la Bonanza.

Prof. Mwamfupe alisema jiji limeamua kufanya hivyo ili kuonyesha jamii kwamba taka zina thamani isipokuwa zinahitajika kuhifadhiwa vizuri.

Alisema kampuni itaanza kazi hivi karibu ili kuanza kuchakata taka hizo katika maeneo mbalimbali.

"Serikali inawajali sana wananchi wake ndiyo maana imeingia mkataba huo ili kuhakikisha wananchi wananufaika nazo," alisema Prof. Mwamfupe.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wakazi wa Dodoma kuzingatia suala la usafi ikiwamo kuhifadhi taka kwa ajili ya kuja kuzichakata hapo baadaye.

Akizungumzia kuhusiana na wiki ya usafi wa mazingira alisema jamii inapaswa kutambua hilo ikiwamo uboreshaji miundombinu kwa ajili ya majitaka ili yasisambae mtaani.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dk. Beatrice Ntayobwa, alitoa maelekezo kwa watendaji kuhakikisha wanasimamia suala la usafi ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Alisema inapaswa itengwe wiki ambayo wananchi watapewa elimu ya namna ya kutunza mazingira katika maeneo wanayoishi.

Diwani wa Chang'ombe, Jumanne Ngede, alisema kata hiyo kila mwaka inashika nafasi nzuri kwenye usafi hivyo serikali isiwe na wasiwasi wowote.

# Bil. 1.5/- kujenga kampasi ADEM Mbeya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) kwa ajili ya ujenzi wa chuo kampasi ya Mbeya na kwamba kukamilika kwake kutaboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

Mtendaji Mkuu wa ADEM, Dk. Siston Mgullah, aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya wakala wa vipaumbele vyake kwa mwaka huu wa fedha.

"ADEM inatoa shukrani za pekee kwa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutupatia fedha za ujenzi wa kampasi ya Mbeya na kuendelea kututengea fedha za ukamilishaji wa ujenzi huo ambao kukamilika kwake kutaboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji," alisema.

Akizungumzia mikakati ya taasisi hiyo kwa mwaka huu wa fedha, Dk. Mgullah alisema wamejipanga kudahili walimu 2,343 katika kozi za CELMA, DEMA na DSQA, kuandaa kiongozi cha mwalimu mkuu na kuandaa mwongozo wa utawala bora wa viongozi wa serikali za mitaa.

Pia alisema wakala umejipanga kutoa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa shule kwa walimu wakuu wapatao 17,000, kutoa mafunzo ya utawala bora kwa wasimamizi wa elimu katika mamlaka za serikali za mitaa.

"Kutokana na maendeleo ya teknolojia kwa sasa tunajipanga kuanza kutoa mafunzo kwa kwa njia ya masafa, kwa sasa tuna mradi na wenzetu wa Chuo Kikuu Mzumbe kwa ajili ya kuandaa moduli za kuendeshea mafunzo ya masafa, tumeshafika mahali pazuri," alisema.

Kuhusu mafanikio ya wakala katika mwaka wa fedha uliopita, Dk. Mgullah alisema walidahili walimu 1,839 katika mafunzo ya Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA) na Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule (DSQA) ili kuwapa ujuzi na maarifa walimu katika usimamizi, ufuatiliaji na tathmini katika elimu.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari - MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema serikali inaweka fedha nyingi kwenye sekta ya elimu nchi nzima na kwa mwaka wa fedha 2022/23, sekta ya elimu pekee imetengewa Sh. trilioni 5.8.

Alisema fedha hizo ni nyingi ambazo zinahitaji usimamizi wa karibu, hivyo viongozi kwenye taasisi zinazosimamia elimu lazima wawe na ujuzi na mbinu nzuri za kusimamia maendeleo ya elimu ili kupata thamani ya fedha zilizotolewa na serikali.





# Uchaguzi mdogo Jimbo la Amani, Desemba 17

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UCHAGUZI mdogo wa Jimbo la Amani, unatarajiwa kufanyika Desemba 17, mwaka huu baada ya kuwa wazi kutokana na kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Mussa Hassan Mussa.

Maandalizi ya uchaguzi huo yameanza kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwanoa wasimamizi wa uchaguzi huo.

Akifungua mafunzo kwa wasimamizi hao jana, Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi NEC, Balozi Omar Ramadhan Mapuri, aliwataka wasimamizi hao kufuata taratibu za uchaguzi ili uwe huru na kuondoa malalamiko wakati wote wa mchakato huo.

Alisema hali hiyo itasaidia kuondoa vurugu na mivutano ya kisiasa ambayo inaweza kuvuruga amani.

Aidha, alisema ni wajibu wao kutambua kuwa wameaminiwa na kuteuliwa kwa sababu ya imani ya Tume, kuwa wana uwezo wa kufanya kazi hiyo na muhimu kujiamini na kufanya kazi kwa weledi.

"Uchaguzi ni mchakato unaojumuisha hatua na taratibu mbalimbali za kufuata na kuzingatia na hatua hizo ndio msingi wa uchaguzi kuwa mzuri wenye ufanisi na hivyo kupunguza kama sio kuondoa kabisa malalamiko au vurugu wakati wote wa mchakato wa uchaguzi," alisema.

Aliwaasa wasimamizi kuvishirikisha vyama vya siasa na wadau wingine wa uchaguzi katika maeneo yao kwenye masuala ya uchaguzi ambayo wanastahili kushirikishwa na litawarahisishia utekelezaji wa majukumu yao.

Balozi Omar, aliwataka wasimamizi hao kufanya utambuzi wa vituo vya kupigia kura mapema ili kubaini mahitaji maalum ya vituo husika na kuona mpangilio mzuri utakaoruhusu uchaguzi huo kufanyika kwa amani na utulivu.

Nao washiriki wa mafunzo hayo walisema baada ya kumaliza mafunzo hayo watahakikisha wanausimamia uchaguzi huo kwa haki na uadilifu.

Ali Idarous Suleiman, miongoni mwa wasimamizi hao alisema uchaguzi huo utakuwa huru na haki na kuwaomba wananchi na vyama vya siasa kushiriki ili kumchagua mgombea atakayeweza kuwaletea maendeleo katika jimbo lao.

# Abdullah: Ushirikiano muhimu kukuza sekta ya nishati

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemedi Suleiman Abdullah, amesema ushirikiano wa pamoja unahitajika kukuza sekta ya nishati ya maji kwa nchi za Afrika ili kuboresha huduma hizo kwa wananchi wa nchi hizo.

Aliyasema hayo jana katika mkutano wa 16 wa kujadili masuala ya nishati kwa nchi za Afrika uliofanyika Mbweni mjini hapo.

Alifurahishwa kuona mkutano huo unazindua ripoti ya ugawaji wa maji barani Afrika ambayo itatoa muhtasari wa hali ya udhibiti wa utoaji wa huduma hizo.

Alisema kuwapo kwa ripoti hiyo kutatoa fursa kwa Zanzibar na nchi zingine kupata uzoefu kwa nchi mbalimbali jinsi ya udhibiti wa huduma ya maji unavyofanyakazi na namna ya kukabiliana na changamoto katika udhibiti wa huduma hiyo.

Aidha, alisema mkutano huo utatoa fursa kwa washirika wa ndani na nje ya nchi kuwa na mtazamo wa pamoja wenye lengo la kubadilishana mawazo na uzoefu katika mifumo ya udhibiti wa majisafi.

Alisema kuwa nchi zote duniani zinapambana na kufikia malengo ya dunia ya maendeleo hasa upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wote na ni wajibu kwa taasisi za udhibiti huduma hiyo kusimamia ipasavyo sekta husika ili kufikia malengo hayo ya dunia.

Aliipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), wanavyosimamia sekta hiyo na kueleza kuwa Serikali ya Zanzibar itaendelea kuwajengea uwezo watendaji wa mamlaka hiyo pamoja na kukuza ushirikiano na taasisi nyingine.

Mwenyekiti wa umoja wa taasisi zinazodhibiti huduma za nishati Afrika, Balthazar Nganikiye, alisema lengo la kuwapo kwa mkutano huo ni kuzijengea uwezo mamlaka za udhibiti wa nishati nchi za Afrika pamoja na kukuza ushirikiano kwa nchi hizo.

Aidha, alisema umoja huo una jukumu la kujua changamoto zinazozikabili nchi za Afrika katika usambazaji wa maji na kujadili njia bora ya kutatua changamoto hizo.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaaban Ali Othman, alisema mkutano huo utatoa fursa kujua njia nzuri zinazotumiwa na nchi za Afrika hasa katika suala la usambazaji wa maji jambo ambalo litasaidia serikali kuwafikishia wananchi wake huduma hiyo.



Kamishna wa kinga, tiba na marekebisho ya tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar, Juma Zidi Kheri (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, walipotembelea kituo cha kurekebisha tabia cha waraibu Kidimni, Wilaya ya Kati Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yafungua kituo tiba waraibu dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMISHNA wa kinga, tiba na marekebisho ya tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar (waraibu), Juma Zidi Kheri, amesema serikali imefungua kituo cha tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya ambacho hutoa tiba, mafunzo ya ufundi na ujasiriamali ili wanapotoka katika chuo hicho wawe na ujuzi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari waliofika kituoni hapo huko Kidimni, Wilaya ya Kati Unguja, ziara iliyoandaliwa na Wizara ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Alisema lengo la kituo hicho ni kuwapatia tiba waraibu hao kuachana na matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema ujuzi wanaoupata kituoni hapo utawasaidia kuajiriwa, kujiajiri wenyewe na kupata kipato kwa ajili ya kuendesha maisha yao.

Alisema kituo hicho kimeanza Januari mwaka huu na kina waraibu 50 wote wanaume, matarajio yao ni kupokea waraibu 200 kila mwaka ili kuwatoa katika dimbwi la matumizi ya dawa za kulevya.

"Suala la matibabu ni la ridhaa na huwezi kumtibu mtu kwa kutumia nguvu hivyo vijana waliopo hapa wapo tayari kutibiwa na kuachana na dawa za kulevya," alisema.


Alisema kituoni hapo wanapatiwa elimu ya ujasiriamali kwa vitendo na nadharia na watakapomaliza masomo kuwaunganisha na idara ya uwezeshaji kwa ajili ya kupatiwa mikopo ili kuendesha miradi.

Aidha, alisema kituo hicho kina miradi mbalimbali kinaendeshwa kwa kuwashirikisha vijana hao ikiwamo ufugaji wa ng'ombe, kuku na kilimo cha mboga.

Alisema miradi hiyo inatokana na fedha za ahuweni za UVIKO-19 na wamepatiwa na serikali Sh. milioni 400.

Waraibu waliopo kituoni hapo, walisema kuwa wengi wao wamejiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya kutokana na ushawishi, lakini sasa wameamua kuacha matumizi hayo.

"Tunaiomba jamii tunaporudi uraiani watupokee na kuacha kutunyanyapaa kwa sababu sasa tumeacha matumizi ya dawa za kulevya," alisema mmoja wa waraibu hao ambaye hakutaka kutajwa jina lake.





# Mganga akutwa amejinyonga chumbani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MGANGA wa kienyeji, Salum Samweli (45), mkazi wa mtaa wa Mlimani Kata ya Muhungula, Kahama mkoani Shinyanga, amekutwa akiwa amefariki dunia huku akidaiwa kujinyonga chumbani kwake baada ya kufanya usafi ndani na kutoa zana zote za kazi nje.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo ambao hawakutaka kutajwa majina yao, walisema lilitokea Novemba 11, mwaka huu, na kwamba walikuta mwili wa mtu huyo umening'inia huku amepiga magoti chumbani kwake.

Walisema walikuta amejinyonga kwa kutumia shuka la kimasai na kwamba wameshanganzwa na namna alivyokufa huku amepiga magoti.

Mama anayekuwa akiishi na mganga huyo, kabla ya kifo usiku wake alipika chakula wakala pamoja kisha akamwomba afanye usafi chumbani kwake aondoe zana zote za uganga.

Alisema baada ya usafi waliingia kulala kila mtu kwenye chumba chake na majira ya saa 7:00 saba usiku, ilisikia sauti na kishindo. Alisema alipoingia chumbani kwa mganga huyo, alimwambia arudi akalale hakuna tatizo lolote.

Pia alisema aliendelea kusikia sauti hizo na kulipokucha alikuta mlango uko wazi na mwili ukining'inia chumbani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi, (ACP) Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba wanaendelea na upelelezi ili kujua chanzo cha kifo chake.

Alisema mwili wa marehemu umehifadhi katika chumba cha kuhifadhia maiti Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa uchunguzi zaidi na utakapokamilika, utakabidhiwa kwa ndugu



Mbunge wa Same Mashariki, Anne Kilango Malecela, akionyesha kiti kwa viongozi mbalimbali wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoka kata 14 za jimbo hilo juzi, kabla ya kukabidhi mradi wa viti 100 kwa kila kata ili wafanye biashara ya kuvikodisha na kujiinua kiuchumi. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

## RC aonya wavamizi wa hifadhi misitu

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani, amewaonya wananchi waliovamia Msitu wa Nyahua na kufanya shughuli za kibinadamu huku akiwataka kuondoka haraka ili kuokoa chanzo hicho muhimu.

Akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Makibo, Kata ya Nyahua, alisema ni lazima kuhifadhi misitu ili kukabili mabadiliko ya tabianchi, hivyo ni marufuku kuingia kwenye eneo hilo kufanya shughuli za kibinadamu.

Pia alisema wananchi wanapaswa kutambua faida za kuhifadhi misitu kuwa ni pamoja na kupata mvua, kunyonya hewa ukaa inayoharibu anga, hivyo kupata fedha kutoka kwa wahisani wanaofuatilia waliohifadhi misitu baada ya kupima kiwango cha hewa iliyonyonywa.

"Utunzaji wa mazingira unatakiwa kutiliwa mkazo, eneo la Sikonge kwa misitu iliyohifadhiwa mnaweza kupata hata zaidi ya Sh. bilioni 50 kupitia hewa ukaa, utalii na shughuli mbalimbali zinazofanywa na wahisani wa mazingira na kuongeza pato letu," alisema.

Alisema ni muhimu wananchi hao wakaondoka ili msitu huo ufikie sifa zinazotakiwa huku akiahidi kuwa serikali itachukua hatua kali kwa wote watakaoendelea kuharibu.

# Watakiwa kufichua ukatili wa kijinsia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI mkoani Shinyanga wametakiwa kuwafichua wanaofanya ukatili wa kijinsia, ili wachukuliwe hatua kukomesha vitendo hivyo kwenye jamii na kulinda heshima na haki ya kila binadamu.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Kikundi cha Sauti ya Mama kutoka Dar es Salaam, Samila Rashid, wakati wakitoa elimu ya kupinga mimba na ndoa za utotoni kwa wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari katika Manispaa ya Shinyanga.

Alisema matukio mengi ya ukatili wa kijinsia yanafanywa na watu wa karibu wanaofahamika na kuaminiwa, huku jamii ikimaliza kesi kifamilia, hivyo akawataka kuacha kufumbia macho na badala yake watoe taarifa.

"Naomba wananchi wa mkoa wa Shinyanga ili matukio haya ya ukatili wa kijinsia yapate kupungua ama kuisha kabisa, msiwakumbatie wahalifu bali wafichueni sababu wanafahamika," alisema Samila.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliwapongeza wanakikundi hao kwa kutoa elimu hiyo ya ukatili wa kijinsia shuleni, huku akiwaonya watu ambao bado wanaendekeza vitendo hivyo kuwa serikali itawashughulikia pamoja na kuwafunga jela.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Holy Smile mkoani Shinyanga, Arnold Bweichum, alisema katika kukabiliana na vitendo vya ukatili hasa mimba na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga, wameamua kutoa elimu ya ukatili shuleni, ili wanafunzi wawe wanatoa taarifa wanapokuwa wakifanyiwa ukatili.

Alisema elimu hiyo wameitoa kwenye shule tano mkoani Shinyanga na kwamba itakuwa endelevu kwa kushirikiana na kikundi hicho cha Sauti ya Mama, ambacho kinaundwa na wasanii wa filamu hapa nchini, ili kuhakikisha elimu ya ukatili inafika maeneo mengi.

# Kombora la Russia latua Poland

**WARSAW,** Poland

POLAND imelalamika kuwa kombora lililotengenezwa na Russia lilitua katika eneo lake na kuua watu wawili katika kijiji cha Przewodow.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Lukasz Jasina alitangaza jana kuwa balozi wa Russia nchini humo, ameitwa ili kutoa maelezo ya kina kuhusu tukio hilo.

Taarifa hiyo haijasema nani aliyerusha kombora hilo na pande zote mbili katika mzozo huo zinatumia mabomu yaliyotengenezwa na Russia.

Przewodow iko kwenye mpaka wa Poland na Ukraine, kaskazini mwa jiji la Lviv.

Makombora yaliripotiwa kushambulia kijiji cha Przewodow, yapata maili nne sawa na km 6.4km kaskazini mwa Ukraine, mapema jana. Raia wawili wa Poland waliuawa katika mlipuko huo, zima moto walisema.

Marekani na washirika wengine wa Magharibi wanachunguza lakini hawajathibitisha ripoti kwamba yalikuwa makombora ya Russia yaliyopoteza mwelekeo.

Hata hivyo, Russia inakanusha kuhusika na shambulio hilo.

"Hakuna kombora tulilorusha karibu na mpaka wa jimbo la Ukraine na Poland " wizara yake ya ulinzi ilisema katika taarifa, na kuongeza kuwa ripoti hizo ni uchochezi wa makusudi unaolenga kuzidisha hali ya wasiwasi.

**Hili ndilo jibu la Russia kwa Indonesia, India, China na nchi nyingine zote zilizozungumzia haja ya kumaliza vita. Inauambia ulimwengu kwamba inataka kuendelea. Sasa ni wakati wa dunia kujibu.**

Waziri Mkuu wa Poland Mateusz Morawiecki, aliwataka watu kuwa watulivu baada ya kombora lililotengenezwa na Russia kuwaua watu wawili katika kijiji cha Poland karibu na mpaka wa Ukraine.

"Ninatoa wito kwa Wapoland wote kuwa watulivu katika kukabiliana na janga hili.Ni lazima tujizuie na kuwa waangalifu," Morawiecki alisema baada ya mikutano ya dharura ya serikali yake.

Pia alisema kuwa majeshi ya Poland yataongeza ufuatiliaji wa anga yake kufuatia tukio hilo.

"Tuliamua kuongeza utayari wa kupambana na vitengo vilivyochaguliwa vya jeshi la Poland, kwa msisitizo maalum katika ufuatiliaji wa anga," aliwaambia waandishi wa habari.

Wakati huo huo, Viongozi wa mataifa tajiri duniani ya G7 wameitisha kikao pembeni ya mkutano wa G20 huko Bali, Indonesia kujadili tukio hilo.

Ikulu ya Marekani ya White House iliitisha mkutano wa dharura ambao hawakuruhusiwa waandishi kuhudhuria.

Mwandishi mmoja aliuliza iwapo Rais wa Marekani Joe Biden, anaweza kutoa taarifa kuhusu shambulizi hilo la kombora.

Hata hivyo, Biden alijibu kwa kusema "Hapana."

Majibu kutoka kwa nchi za Nato, pamoja na Ikulu ya White House, yamekuwa ya tahadhari na hakuna lawama yoyote ambayo imehusishwa na kombora hilo.

Katika ujumbe wake wa Twitter, Rais wa Marekani alisema amezungumza na Rais wa Poland Andrzej Duda na kutoa uungaji mkono kamili kwa uchunguzi kuhusu mlipuko huo.

**RUSSIA YASHAMBULIA**

Wakati hayo yakijiri, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alisema mashambulizi ya makombora yanayoendelea nchini mwake yana ujumbe wa Russia kwamba haina nia ya kumaliza vita.

Katika hotuba yake ya jana usiku, Zelensky alisema jumla ya makombora 90 yalirushwa, na kuharibu miundombinu ya nishati, biashara na majengo ya makazi.

"Mara tu baada ya siku ya kwanza ya mkutano wa kilele wa G20 kumalizika nchini Indonesia,mashambulizi yalitokea" alisema.

Aliongeza "Russia inaambiwa kuhusu amani, lakini inarusha makombora kujibu. Inaambiwa juu ya machafuko ya kimataifa ambayo ilisababisha, na inazindua droni za Irani kujibu,".

Zelensky alisema mashambulizi hayo yamesababisha kukatika kwa umeme nchini kote, ikiwemo katika mikoa ya Kyiv, Lviv, Kharkiv na Zhytomyr.

"Hili ndilo jibu la Russia kwa Indonesia, India, China na nchi nyingine zote zilizozungumzia haja ya kumaliza vita. Inauambia ulimwengu kwamba inataka kuendelea. Sasa ni wakati wa dunia kujibu," alisema.

Zelensky aliongeza kuwa zaidi ya makombora 70 na ndege zisizo na rubani 10 zimedunguliwa, na aliwashukuru washirika wote wanaosaidia kulinda anga ya nchi yake.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi Sergei Lavrov alikuwa mjini Bali kama mwakilishi wa nchi yake katika G20, lakini aliondoka kwenye mkutano huo mapema Jumanne jioni kabla ya mashambulizi ya Russia. **BBC**

## Wanajeshi zaidi kutoka Kenya wawasili mashariki DRC

**NAIROBI,** Kenya

KUNDI la pili la wanajeshi kutoka Kenya walitarajiwa kuwasili Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo jana.

Wanajeshi hao ni sehemu ya kikosi cha kikanda kilichotumwa kwa misheni ya kulinda amani mashariki mwa nchi hiyo.

Makundi yenye silaha yameongeza mashambulizi katika miezi ya hivi karibuni na kuibua wasiwasi kuhusu tishio kwa usalama wa eneo hilo.

Zaidi ya wanajeshi 900 wa Kenya watakuwa na makao yao karibu na mji wa Goma katika eneo hilo lenye hali tete.

Wanaungana na wanajeshi wa Burundi ambao wamekuwa wakifanya kazi katika jimbo la Kivu Kusini tangu Agosti.

Watasaidia jeshi la Congo kupambana na waasi ambao wamefanya uharibifu tangu mwaka uliopita.

Waasi wa kundi la M23, wameteka maeneo katika miezi ya hivi karibuni na kuwahamisha maelfu ya watu kutoka kwenye makazi yao.

Serikali ya Congo inatazamiwa kuanza tena mazungumzo na wawakilishi wa makundi mbalimbali yenye silaha baadaye mwezi huu katika mji mkuu wa Kenya Nairobi. **BBC**



Magari ya maofisa wa polisi yakiwa katika eneo ulikotokea mlipuko wa bomu katika kijiji cha Przewodow, mashariki mwa Poland jana. **PICHA: REUTERS**

## Museveni asema ebola inadhibitiwa

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, amewahakikishia watalii kutoka mataifa ya kigeni kwamba mlipuko wa Ebola katika taifa hilo utadhibitiwa.

Katika hotuba yake ya jana, Rais Museveni alibainisha kuwa watalii wa kigeni walikuwa wakighairi kwenda nchini humo na mikutano ya kimataifa ilikuwa inaghairishwa au kuhamishiwa katika nchi nyingine.

Alisema janga hilo lipo ndani na kwamba kesi zinazoendelea ni katika wilaya sita pekee kati ya 146 zilizoko nchini humo.

"Uganda iko salama na wageni wa kimataifa wanakaribishwa," aliongeza.

Alisema kuwa orodha ya watu walioambukizwa virusi hivyo imetolewa kwa mamlaka ya uhamiaji ili kuwazuia kusafiri kimataifa.

Baadhi ya kesi 141 zilizo na vifo 55 zimerekodiwa tangu kuzuka kwa ugonjwa huo.

Rais Museveni alisema mafanikio yamepatikana katika kudhibiti janga hilo. Kwa siku 18, hakukuwa na kesi zilizothibitishwa katika wilaya ya Mubende, ambako ni kitovu cha mlipuko huo, ingawa kisa kimoja kiliripotiwa Jumatatu, kwa mujibu wa maofisa wa afya.

Museveni alisema kuwa juhudi za kudhibiti janga hilo zinatatizwa na baadhi ya wananchi wanaokataa kuzingatia vikwazo vya afya.

Pia usafiri wa pikipiki, unaojulikana kama boda boda, ulikuwa ukikaidi sheria za kutotoka nje katika maeneo yaliyoathiriwa na kusafirisha abiria badala ya mizigo pekee.

Katika wilaya ya Kassanda, watu 10 wa familia moja walikufa kwa ugonjwa wa Ebola baada ya kufukua maiti iliyozikwa na timu rasmi ya mazishi na kuzika tena kulingana na imani zao za kidini.

Jijini Kampala, watu wawili waliohusishwa na kesi tofauti walitoroka kutoka vituoni, mmoja alifika hadi mji wa Masaka na mwingine katika jiji la Jinja na wote wawili walifariki dunia.

Ingawa janga hili limeenea katika wilaya mbali na ilikoanzia, maofisa wa Uganda wanaonekana kuwa na imani kwamba mlipuko huo unaweza kudhibitiwa kabla haujasambaa. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**FRANELLA FRANCOS HALLA** Anatangaza kupotea kwa hati yake yakusafiria (Passport) yenye namba **TAE 091230** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji tarehe 25/02/2019, Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi kilicho karibu nae.

TAARIFA YA POLISI: **WMB/RB/895/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha MAKOLE Mkoa wa DODOMA**

**MADAI NO. 189/2022**

**KUITWA SHAURINI MSHTAKIWA**
**(Aya ya 9 nyongeza ya III ya sheria ya mahakama za Mahakimu)**

**Kwa... ISSLAH ABDALLAH**
**MZANZIBAR, MSALATO**

**Kwa kuwa imelazimika uhudhurie ili ujibu shtaka dhidi yako la MADAI TSHS. 5,000,000/=**

Unaamriwa na Mahakama uhudhurie mbele ya Mahakama hii siku ya tarehe 22 mwezi 11 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi/mchana ili shauri liweze kusikilizwa. Endapo utashindwa kuhudhuria siku na muda uliopangwa hapo juu, na ikithibitika kwamba umepokea kuitwa shaurini, hati ya kukamatwa itatolewa dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 16 mwezi 11 mwaka 2022.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA KILINDI**

**MAOMBI MADOGO NA. 40 YA MWAKA 2022**

**MALISELI JOHN NG'ORA…………………MSHINDA TUZO**

**DHIDI YA**

**LAMIA ABEDI SAID ……………………MSHINDWA TUZO**

**KWA MSHINDWA TUZO**
**LAMIA ABEDI SAID**

**KUITWA SHAURINI**

Mshinda tuzo ameleta maombi madogo dhidi yako mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) kilindi-Tanga. Maombi haya yamepangwa kusikilizwa tarehe 24/11/2022 saa tatu asubuhi. Hivyo basi unatakiwa kufika wewe mwenyewe au wakili wako kwa tarehe iliyopangwa. Endapo hautahudhuria shauri hili litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Kilindi leo tarehe 15/11/2022

**MHINA ER**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KILINDI**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 124 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late PETER SIMON MUSHI**

**By 1.NATHALIA PETER MUSHI**
**2……………………………….**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 28 Day of 11/2022

Dated at MOROGORO this 15 day of 11/2022.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 123 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late:JOSEPH WILLIAM LUPEMBE**

**BY 1. THERESIA RAMADHANI CHUMA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 06th DECEMBER………2022

Dated at MOROGO this 15th day of NOVEMBER………2022

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**MOHAMED ABDIRAHMAN AIDARUS** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma: cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0303-0064** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ARUSHA-MERU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2004 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0302-0538** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ARUSHA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2007. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/KIG/RB/442579/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VALENCE EMILY MYOVELA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI SJ40** yenye usajili namba **T712 BDW** na CHASSIS NAMBA: **SJLOT125264.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:**SO/RB/7612/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VERONICA VALENTINE TEMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUBARU IMPREZA** yenye usajili namba **T121 DPC** na CHASSIS NAMBA: **GH2034958.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SO/RB/7610/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PROGRESSIVE CONSTRUCTION LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX** yenye usajili namba **T 683 BRZ** na CHASSIS NAMBA: **JTFDS696500039423.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.. POLISI TAARIFA: **SO/RB/7593/2022**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 122 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**WILSON ISMAEL SHAYO**

**BY 1. ANNUNCIATA ANSELM LYIMO**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 07th DECEMBER………2022

Dated at MOROGO this 15th day of NOVEMBER………2022

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARY MARCUS MSIGWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **YUTONG ZK6932D1** yenye usajili namba **T331 DJU** na CHASSIS NAMBA: **LZYTETD24G1059900.** Kwa yeyote takaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SO/RB/7591/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARY MARCUS MSIGWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya agri aina ya **YUTONG ZK6932D1** yenye usajili namba : **T330DJU na CHASSIS** NAMBA: **LZYTETD21G1059899.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA : **SO/RB/7592/2022**

---

**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL**

**FOR: ROMBO**

**AT: ROMBO**

**APPLICATION NO: 102 OF 19**

**MICHAEL ZAKARIA TARIMO……………APPLICANT**

**VERSUS**

**FLOMENA SAMBONANGA SHIRIMA & 5 OTHERS…………RESPONDENT**

**SUMMONS/NOTICE**

**TO: ZENAS AZAEL MREMI, PRIVA AZAEL MREMI, VERA AZAEL MREMI, HILDA MICHEAL TARIMO AND WINIFRIDA MICHAEL TARIMO**

Take notice that the above matter is coming for mention/hearing on 21 day of November, 2022 before the H.I. LUKEHA Hon. Chairman of the Tribunal. You are hereby commanded to appear at 8:30 am when the case will be mentioned/heard. You are further ordered to file Written Statement of Defence and all documents you intend to rely for your defence within 21 days upon receiving this summons.

**TAKE FURTHER NOTICE:** that if you will fail to attend and file your defence within the required time and if it will be proved that you were served with this summons, this Tribunal may enter Judgment against you in your absence.

Given under my hand and the seal of this Tribunal on this 29th day of November, 2022.

Chairman
District Land and Housing Tribunal

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## H. Baba aanza kumchokonoa Harmonize

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, H. Baba, amedai kitendo cha Harmonize kumchagua Kajala kuwa Meneja wake ni matokeo ya kumuiga Wizkid ambaye mke wake, Jada P ndiye meneja wake.

H. Baba amesema meneja na mahusiano ni vitu viwili tofauti, huwezi kuvichanganya na kupata matokeo mazuri na pengine ndio sababu ya baadhi ya wasanii kuondoka katika lebo yake ya Konde Music.

"Wanataka kuiga kwa Wizkid, hawawezi. Meneja au mke wa Wizkid alikuwa anamsimamia Chris Brown, kwa hiyo kuja kumsimamia Wizkid ni jambo jepesi kwa sababu ana uzoefu, sasa huyu dada yetu hana uzoefu wa hicho," alisema H. Baba.

Utakumbuka tangu Kajala kuwa Meneja wa Konde Music, wasanii watatu, Cheed, Killy na Anjella wameachana na lebo hiyo.



## Mbosso ahairisha ziara Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Mbosso, ametoa sababu za kusitisha ziara yake ya nchini Marekani ambayo ilitarajiwa kuanza Novemba 25 hadi Desemba 16, mwaka huu.

Kupitia Instagram yake, Mbosso amesema sababu kubwa ni kimatibabu na daktari wake amemtaka kutokusafiri au kukaa kwenye ndege kwa zaidi ya saa nane.

"Natangaza kuahirisha ziara yangu ya muziki nchini Marekani na hiyo ni kutokana na ushauri wa daktari wangu, hivyo chochote kitakachojiri nitawajulisha," aliandika Mbosso.

Mbali na hivyo, Mbosso ameahidi kuwa ziara hiyo itaendelea mapema atakapopata ruhusa ya daktari wake.





# BEYONCE, ADELE WACHUANA TUZO ZA GRAMMY

**LOS ANGELS,** Marekani

WAKATI tangazo la walioteuliwa kuwania tuzo za Grammy mwaka huu limetolewa juzi Jumanne, ushindani mkubwa umeibuka kati ya waimbaji Adele na Beyonce kuwania nafasi ya juu.

Wawili hao wanawania katika sehemu mbili tofauti za mashindano hayo kama ilivyokuwa mwaka 2017.

Beyonce, anaongoza katika orodha ya wateule wa tuzo za Grammy, akipata teuzi tisa za dhahabu, akiwa anaongoza, na Kendric Lamar, akipata teuzi nane naye muimbaji Adele kutoka Uingereza akipata teuzi saba, kadhalika muimbaji Brandi Carlile naye akipata teuzi saba.

Tangazo la wateuzi wa mwaka huu wa Grammy linaonekana kuweka tena steji moja, waimbaji Adele na Beyonce kuwania nafasi ya juu, katika sehemu mbili tofauti za mashindano hayo kama ilivyokuwa mwaka 2017.

Baadhi ya wale walioteuliwa kuwania tuzo ya albam ya mwaka ni pamoja na Kendric Lamar, Adele, Brandi Carlile, Lizzo, Bad Bunny, Mary J Blige, Harry Styles, Abba, Coldplay na Beyonce.

Utambuzi na uteule wa Beyonce unatokana na kutoa albamu yake kabambe yenye miondoko ya disco ijulikanalo kama "Renaissance".

Albamu iitwayo "Mr. Morale And The Big Steppers", la Kendik Lamar, Adele naye na albamu yake ya 30 huku Brandi Carlile na albamu yake, In These Silent Days.

Waimbaji hawa wanne kadhalika nyimbo zao zimeteuliwa katika kundi la rekodi ya mwaka. Wimbo wa Adele, Easy On Me, ulitia fora sana mwaka jana.

# TFF, UNFPA WAINGIA MKATABA WA KIJAMII MASHINDANO YOTE

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia mkataba wa miaka mitano na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Masuala ya Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), kwa ajili kutumia michezo ya mashindano yote chini ya TFF kutokomeza mambo ya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto wa kike.

**Akizungumza na gazeti hili jana katika hafla ya makubaliano hayo, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema UNFPA amekuwa mshirika mwenza wa shirikisho hilo kwenye mambo ya kijamii ikiwamo kwenda sambamba na kufikia malengo ya taasisi hiyo.**

Alisema wameingia makubaliano hayo kupitia ligi zote zinazoendeshwa na Bodi ya Ligi Tanzania inayosimamiwa na TFF ili kuhakikisha wachezaji wanakuwa mstari wa mbele kupinga unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto wa kike.

"Makubaliano hayo ni makubwa na yanathamani kubwa kuliko ile tunayosaini ya fedha, TFF tumekubaliana na UNFPA kwa ajili ya kusaidia jamii, vifo vya kinamama wakati wa kujifungua, kusaidia mahitaji ya umuhimu na ya hiyari ya uzazi wa mpango kumfikia kila mhitaji.

"Kutokomeza maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuhakikisha kila ujauzito unathamani, kila uzazi ni salama na kila malengo ya vijana yanafikiwa," alisema Karia.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA Tanzania, Mark Bryan Schreiner, alisema amefurahi kuona vijana wa Tanzania wakicheza mpira na kufurahia na kuendelea kutimiza ndoto zao hasa watoto wakike.

Alisema mpira wa miguu unatazamwa na mamilioni ya watu na kwamba kupitia soka afya za wachezaji zinakuwa imara na bora.

"Tumeingia makubaliano na TFF kwa ajili kufikia jamii kwa haraka kwa sababu ya mchezo wa mpira wa miguu umekuwa ukifuatiliwa na zaidi ya mamilioni ya watu ndani na nje ya mipaka ya Afrika.

"Kupitia soka tunaweza kufikia kwa ukaribu na kupunguza mimba za utotoni kwa wasichana wadogo na kuzuia vifo vya kina mama wajawazito, takwimu zinaonyesha wakimama zaidi 30 wanapoteza maisha katika changamoto za kujifungua," alisema Schreiner.

Alisema UNFPA na TFF kupitia ligi zote watatokomeza mila kandamizi kwa kupinga mimba za utotoni na ukeketaji kwa mtoto wa kike.



Waogeleaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania wakiwa katika picha ya pamoja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Kuogelea kusaka taji Kanda ya Tatu Afrika*

**Na Mwandishi Wetu**

WAOGELEAJI 63 wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Tanzanites na Diamond), leo wanaanza kampeni ya kutwaa ubingwa wa michuano ya Kanda ya Tatu Afrika kwenye bwawa la Klabu ya Dar es Salaam Gymkhana jijini.

Mashindano hayo yataanza saa 2.00 asubuhi na kushirikisha waogeleaji wengine 200 kutoka nchi nyingine 10 za bara la Afrika.

Nchi hizo ni Uganda ambayo itawakilishwa na waogeleaji 45, Burundi (10), Rwanda (14), Eritrea (5), Ethiopia (7), Zambia (23), Afrika Kusini(18), Sudan (14) na Djibouti ambayo itawakilishwa na waogeleaji 16. Pia kutakuwa na wengine 48 kukamilisha jumla ya waogeleaji 263.

Kwa ujumla waogeleaji hao watashindana katika staili tano tofauti za kuogelea mmoja mmoja na pia kutakuwa na mashindano ya relei (relay) huku jumla kukiwa na matukio 140.

Waogeleaji wa timu ya Tanzanites ambao wamepewa jukumu la kuiletea sifa Tanzania katika mashindano hayo kwa upande wa wanawake ni Bridget Heep, Maryam Ipilinga, Crissa Dillip na Lorita Borega.

Wengine ni Amylia Chali, Filbertha Demello, Aminaz Kachra, Aliyana Kachra, Lina Goyayi, Sophia Latiff, Ria Save, Natalia Ladha, Sarah Tibazarwa, Muskan Gokan na Sarah Shariff.

Waogeleaji wanaume ni Julius Missokia, Max Missokia, Kabeer Lakhani, George Nangale, Austin Okore, Aryan Bhatt, Nabeel Gahhu na Mark Tibazarwa.

Wengine ni, Peter Itatiro, Delbert Ipilinga, Ethan Alimanya, Romeo Mwaipasi, Hilal Hilal, Collins Saliboko, Mohameduwais Abdulllatif, Michael Joseph na Aaron Akwenda.

Waogeleaji wa timu ya Diamond ambao watashiriki katika mashindano hayo ni Zainab Moosajee, Aamina Takim, Myra Makwaia, Abigail Mutungwa, Mahek Desai, Amaris Nanyaro, Catherine Maokola, Aaliya Takim, Mischa Ngoshani, Naisae Teggisa, Rahma Semizigi na Kalya Temba.

Kwa upande wa wanaume ni Kaysan Kachra, Hape Coleman, Alberto Itatiro, Luke Okore, Zac Okumu, Isaac Mukani, Enrico Barretto na Sahal Harunani. Wengine ni Christian Fernandes, Salman Yasser, Delhem Rashid, William Chengula, Elia Kimimba, Santo Bash,George Coleman, Nathan Kagoro, Sayi Goyayi, Elia Hangi na Revocatus Joseph.

Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya mashindano hayo, Hadija Shebe alisema kuwa maandalizi yote yamekamilika na kuwaomba wadau wa mchezo huo kujumuika kuipa sapoti timu ya Tanzania.

## Ligi za Wilaya kuchezwa na U20

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF), limeelekeza kuwa kuanzia sasa Ligi za Wilaya zitachezwa na wachezaji vijana walio na umri chini ya miaka 20.

Rais wa TFF, Wallace Karia alisema hayo kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa shirikisho hilo jijini Mwanza, akiweka wazi kuwa wameamua kufanya hivyo kwa makusudi kwa ajili ya kuwasaidia wachezaji vijana ili wapate timu za kucheza kwa sababu hakuna raslimali za kutosha za wengi wao kucheza ligi za vijana.

Karia alisema vijana wengi kwa sasa nchini wanashindwa kuonyesha vipaji vyao kwa sababu wachezaji wanaostaafu kucheza ligi za madaraja ya juu wamekuwa wakishuka chini na kucheza madaraja ya huko, hivyo kuziba vipaji vinavyotakiwa kuonekana.

"Tunaelekeza mikoa kuwa ligi za wilaya zichezwe na vijana wasiozidi umri wa miaka 20, tunafanya hivyo makusudi kwa sababu nchi yetu imekuwa kubwa, hatuna raslimali ya kuweza kucheza ligi za vijana, sasa utakuta vijana wanakwama kwa sababu kuna wanaostaafu huko juu, halafu wanakuja huku wanacheza tena ligi za madaraja ya chini," alisema Karia.

## Black Sailor yaona mwezi Ligi Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Black Sailor imeona 'mwezi mchana' baada ya kufanikiwa kuonja utamu wa ushindi wa Ligi Kuu Zanzibar kwa mara ya kwanza tangu kuanza kwa msimu huu baada ya kushuka dimbani mara 12.

Black Sailor juzi ilifanikiwa kupata alama hizo tatu baada ya kuwafunga Maafande wa Polisi bao 1-0 katika mchezo uliochezwa Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Bao pekee la 'Mabaaria Weusi' hao lilipachikwa nyavuni na Ali Saleh katika dakika ya 14 ya mchezo huo wa kukamilisha mzunguko wa 12 wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Salehe Machupa, alisema malengo yao ni kuhakikisha timu hiyo inakwenda mapumziko ya dirisha dogo angalau ikiwa na alama 10.

Kuhusu timu yake kuburuza mkia katika ligi hiyo, alisema ni kweli timu haipo katika nafasi nzuri kwenye msimamo na kwamba ni kawaida kwa klabu za soka duniani kukumbwa na upepo mbaya wa kutopata matokeo mazuri katika msimu, hivyo bado hawajakata tamaa kwa kuwa ipo nafasi nyingine ya kurekebisha makosa yaliyowakumba katika mzunguko huu wa kwanza.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### RONALDO HATAKIWI UNITED




KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amesema Cristiano Ronaldo hatakiwi kuichezea tena Manchester United kutokana na mahojiano yake na Piers Morgan. ***(ESPN)***

#### PAVARD TAYARI MILAN


MCHEZAJI anayelengwa na Manchester United, Benjamin Pavard, mwenye umri wa miaka 26, amesema atakuwa tayari kujiunga na AC Milan kutoka Bayern Munich licha ya beki huyo wa Ufaransa kuhusishwa na Mashetani Wekundu hao. ***(Football Italia)***

#### MILAN AGOMBEWA EPL



MANCHESTER City, Chelsea, Tottenham, Liverpool, Arsenal na Manchester United zote zina nia ya kumsajili beki wa Slovakia, Milan Skriniar, huku Inter Milan wakitumaini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, atasaini mkataba mpya. ***(90 Min)***

#### MBAPPE KUMBADILI RONALDO



KLABU ya Manchester United inapanga kumbadilisha fowadi wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 na mshambuliaji wa Paris St-Germain mwenye umri wa miaka 23, Kylian Mbappe. ***(Mirror)***

#### BARCA HAITASAJILI JANUARI

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, amesema miamba hao wa Hispania hawataweza kusajili mchezaji yeyote Januari. ***(Football Espana)***

#### KROSS ATAKIWA CITY



KLABU ya Manchester City inaweza kumnunua kiungo wa kati wa Ujerumani, Tony Kroos, lakini Real Madrid wana matumaini kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ataongeza mkataba wake. ***(Sport)***

#### SAMBA AGEUKA LULU



LEICESTER, Everton na Brighton zote zina nia ya kumsajili kipa wa Lens na Ufaransa, Brice Samba, 28. ***(90min)***

#### AACHANA NA URENO



KIUNGO wa kati wa zamani wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Fabio Carvalho, 20, ameachana na timu ya Ureno chini ya umri wa miaka 21 kupitia ujumbe mfupi wa simu. ***(Mirror)***

#### MOYES YUPO SALAMA



KLABU ya West Ham imemwambia Kocha David Moyes kwamba kibarua chake kiko salama licha ya timu yake kupoteza mchezo wao wa tisa msimu huu Jumamosi. ***( 90 Min)***

#### MATVIYENKO NA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inavutiwa na mlinzi wa Shakhtar Donetsk na Ukraine, Mykola Matviyenko, 26. ***(Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KANE AIPA NAFASI ENGLAND KUSHINDA KOMBE LA DUNIA

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, anaamini England haina hofu tena ya kukiri kuwa inaweza kushinda Kombe la Dunia.

**Kane na wenzake wanaelekea Qatar kwa Kombe la Dunia la 2022 wakiwa wamepungukiwa na kiwango baada ya kushushwa ngazi ya juu ya Ligi ya Mataifa ya Uefa kufuatia sare tatu na kupoteza tatu katika Kundi A3.**

Kikosi hicho cha Kocha Gareth Southgate, hakijashinda tangu ushindi wa 3-0 wa kirafiki dhidi ya Ivory Coast Machi mwaka huu, lakini nahodha Kane amesema hawatakwepa kueleza matumaini yao ya kubeba Kombe la Dunia.

Mshambuliaji huyo aliiambia Sky Sports kuwa: “Lazima tuamini kuwa tunaweza kushinda, ninaangalia nyuma miaka 10, 15 iliyopita na ilikuwa karibu kama tuliogopa kusema tunataka kushinda”.

> ●●● Lazima tuamini tunaweza kushinda, ninaangalia nyuma miaka 10, 15 iliyopita ilikuwa...

Mchezaji huyo alisema anadhani moja ya mabadiliko makubwa ambayo wamefanya kwa miaka minne au mitano iliyopita na Southgate si kuogopa kusema hivyo, na itakuwa ngumu na wanalazimika kufanya kazi kwa bidii sana, kuwa na bahati kidogo na kuwa na mambo mengi yatakayowasaidia kufikia hilo.

Presha imeongezeka kwa Southgate baada ya matokeo mabaya ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, lakini Kane amesema kutokuwa na ushindi kumepunguza matarajio na huenda ikaisaidia England katika mechi yao ya kwanza ya Jumatatu dhidi ya Iran.

“Mchezo wa kwanza ni muhimu sana, kwa hakika, bila shaka hakijakuwa kipindi kizuri zaidi kwa muda mrefu kwa England tangu Southgate achukue jukumu la kuinoa timu hatujapata maajabu kama tulivyokuwa.”

Aliongeza kwa kusema kuwa anahisi kuwa wangeshinda kila mchezo kabla ya mashindano hayo ingekuwa wana uhakika wa kushinda na watashinda, na hiyo inaweza kuja na shinikizo tofauti.

Kane, ambaye amekuwa akichezea Tottenham kila mara katika Ligi Kuu England, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, anaamini kuwa michuano hiyo ya katikati ya msimu itamsaidia kupiga hatua.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,051,2

MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
SINGIDA BS FC
1 | 1.42
X | 3.98
2 | 6.99

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MBAPPE KUMBADILI RONALDO MAN UNITED



**MANCHESTER,** Engand

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuwa inampango wa kuziba pengo la Cristiano Ronaldo, wakipanga kuweka dau kubwa la kumnunua nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe.

Kwa mujibu wa gazeti la The Mirror, Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, amecheza mechi yake ya mwisho akiwa na 'Mashetani Wekundu' baada ya kumkashifu kocha wake kwenye mahojiano yake ya wiki hii.

Mbappe anachukuliwa kuwa mchezaji wa thamani zaidi katika soka duniani, akiwa amefunga mabao 169 katika michezo 193 katika misimu yake mitano iliyopita akiwa na wababe hao wa Ufaransa.

Ingawa kumekuwa hakuna dalili kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, angeichukulia United kama mahali pazuri pa kutua kwa hatua inayofuata ya maisha yake ya soka, ripoti hiyo inadai kuwa yeye ndiye mlengwa wao namba moja.

Gazeti la The Mirror linadai kwamba ikiwa United wataweza kumwondoka Ronaldo katika mkataba wao, watakuwa moja ya klabu pekee barani Ulaya ambayo inaweza kumudu matakwa ya mkataba wa nyota huyo wa juu wa Ufaransa.

Mkataba wa mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki, ni pendekezo la kifedha ambalo limesababisha hata vigogo kama vile Liverpool kumtangaza kuwa ni ghali sana.

Ripoti hiyo pia inasema United itasukuma mbele mipango yao ya kuwekeza kwa mshambuliaji hadi Januari.



## Hazard atakubali kuondoka Real

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard anataka kuokoa maisha yake ya soka Real Madrid, lakini hatakuwa na malalamiko yoyote iwapo klabu hiyo itamtaka aondoke mwishoni mwa msimu huu.

Winga huyo wa zamani wa Chelsea amekabiliwa na wakati mgumu nchini Hispania, huku majeraha kadhaa yakiharibu matumaini yake ya kuhamishia kiwango chake Ligi Kuu ya England kwenda LaLiga.

Sasa Hazard ana nafasi kubwa ya kuonyesha anachoweza kufanya kwenye hatua tofauti, anapojiandaa kucheza sehemu ya Ubelgiji kwenye Kombe la Dunia huko Qatar.

Akitarajiwa kufikisha umri wa miaka 32 Januari, Hazard amefunga mabao mawili pekee na asisti moja katika mechi 15 alizoichezea Madrid mwaka 2022, akianza mara nne tu na kucheza kwa dakika 532 pekee kwenye kikosi cha kwanza. Amebakiza zaidi ya miezi 18 kwenye mkataba wake.

Ikizingatiwa kuwa Hazard alishinda Mpira wa Fedha kwenye Kombe la Dunia la 2018, kama mchezaji wa pili bora katika mashindan hayo, amekuwa na kiwang cha kushuka kwa kushan gaza kutoka mchezaji mku hadi mchezaji wa sehem ndogo.

Hazard alikuwa mcheza bora wa mwaka wa Chelse katika kampeni yake y mwisho kwenye Uwanja w Stamford Bridge, msimu w 2018-19.

Akizungumza na gaze la Marca, Hazard alisem "Lazima nithibitishe kwa ki mtu kuwa naweza kuchez soka. Watu wana shaka n ninachoweza kufanya, lakin siwezi."

07,683/-

# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/11/22 | 18:00 | Fleetwood Town vs Bolton Wanderers | 3.05 | 3.35 | 2.24 |
| 02. 19/11/22 | 18:00 | Burton Albion vs Plymouth Argyle | 2.65 | 3.40 | 2.50 |
| 03. 19/11/22 | 18:00 | Port Vale vs Charlton Athletic | 2.33 | 3.35 | 2.90 |
| 04. 19/11/22 | 18:00 | Cambridge United vs Accrington Stanley | 2.40 | 3.35 | 2.80 |
| 05. 19/11/22 | 18:00 | Colchester United vs Doncaster Rovers | 2.27 | 3.25 | 3.10 |
| 06. 19/11/22 | 18:00 | Grimsby Town vs Stevenage FC | 3.00 | 3.25 | 2.32 |
| 07. 19/11/22 | 18:00 | Cove Rangers FC vs Greenock Morton FC | 2.55 | 3.35 | 2.60 |
| 08. 19/11/22 | 18:00 | Inverness Caledonian Thistle FC vs Ayr United FC | 2.90 | 3.45 | 2.31 |
| 09. 19/11/22 | 18:00 | Queen of The South FC vs Montrose FC | 2.48 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 19/11/22 | 18:00 | Albion Rovers FC vs Stranraer FC | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 11. 19/11/22 | 18:00 | Annan Athletic FC vs Elgin City FC | 2.31 | 3.40 | 2.90 |
| 12. 19/11/22 | 18:15 | SD Ponferradina vs Real Oviedo | 2.55 | 3.05 | 2.85 |
| 13. 19/11/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs CD Leganes | 2.28 | 3.05 | 3.30 |
| 14. 19/11/22 | 22:00 | MVV Maastricht vs Almere City FC | 2.60 | 3.60 | 2.45 |
| 15. 20/11/22 | 19:00 | Sakaryaspor vs Bandirmaspor | 2.80 | 3.30 | 2.45 |
| 16. 20/11/22 | 19:00 | Qatar vs Ecuador | 3.30 | 3.10 | 2.26 |
| 17. 20/11/22 | 21:00 | Racing Santander vs Burgos CF | 2.30 | 2.95 | 3.40 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 17/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3813 | Arka Gdynia Youth vs Cracovia Krakow Youth | 1.57 | 4.19 | 4.48 |
| 13:00 | 4369 | Ghana vs Switzerland | 3.83 | 3.38 | 1.99 |
| 14:00 | 3493 | FC Ingulets vs Dynamo Kiev | 8.35 | 4.86 | 1.29 |
| 14:00 | 4397 | Ihefu FC vs Polisi Tanzania | 2.60 | 2.70 | 3.20 |
| 15:00 | 5490 | FK Slavoj Trebisov vs FC Stk 1914 Samorin | 2.72 | 3.45 | 2.26 |
| 15:00 | 5683 | Macedonia U19 vs Serbia U19 | 5.86 | 4.49 | 1.42 |
| 15:30 | 2617 | Uhersky Brod vs FC Slovan Rosice | 3.85 | 3.80 | 1.73 |
| 16:00 | 2473 | Mbeya City vs Kagera Sugar | 2.21 | 2.80 | 3.85 |
| 16:00 | 3683 | Kansanshi Dynamos vs Zanaco | 2.61 | 2.57 | 3.05 |
| 16:00 | 5161 | Adama City FC vs Welayta Dicha FC | 2.49 | 2.68 | 3.07 |
| 16:40 | 3569 | Japan vs Canada | 2.14 | 3.28 | 3.48 |
| 16:45 | 3941 | Austria U21 vs Turkey U21 | 1.67 | 3.54 | 4.56 |
| 17:00 | 1975 | Mumbai City FC vs Bengaluru FC | 1.61 | 3.98 | 4.37 |
| 17:00 | 3078 | Iraq vs Costa Rica | 4.13 | 3.38 | 1.92 |
| 17:00 | 3895 | Gazelle FA de Garoua vs Young Sports Academy | 2.49 | 2.85 | 3.15 |
| 17:00 | 3928 | Ain M'lila vs JS Bordj Menaiel | 3.50 | 2.96 | 2.10 |
| 17:00 | 4763 | Montenegro U21 vs Slovenia U21 | 2.67 | 3.20 | 2.42 |
| 18:00 | 1226 | Accra Lions vs Hearts of Oak | 2.97 | 2.83 | 2.44 |
| 18:00 | 2519 | Tajikistan vs Russia | 19.23 | 9.11 | 1.11 |
| 18:00 | 4121 | Zlin vs Vyskov | 1.50 | 3.99 | 5.46 |
| 18:30 | 1544 | Sporting Gagnoa vs Societe Omnisport | 1.57 | 3.49 | 5.63 |
| 19:00 | 1329 | Teplice vs Zbrojovka Brno | 2.42 | 3.26 | 2.63 |
| 19:00 | 1355 | Banga Gargzdai vs Zalgiris | 9.75 | 5.46 | 1.23 |
| 19:00 | 4198 | Saint George FC vs Mekelakeya | 1.52 | 3.70 | 5.84 |
| 19:00 | 4814 | ASEC Mimosas vs AF Amadou Diallo | 1.49 | 3.89 | 5.84 |
| 19:00 | 5049 | Syrian Arab Republic vs Belarus | 7.87 | 5.04 | 1.36 |
| 19:00 | 5060 | Young Africans vs Singida BS FC | 1.42 | 3.98 | 6.99 |
| 19:00 | 5124 | Morocco vs Georgia | 1.45 | 4.32 | 7.24 |
| 19:00 | 5605 | Jordan vs Spain | 50.16 | 11.03 | 1.05 |
| 19:30 | 3750 | Romania vs Slovenia | 2.13 | 3.38 | 3.38 |
| 20:00 | 1229 | Montenegro vs Slovakia | 2.42 | 3.17 | 3.02 |
| 20:00 | 5148 | Malta vs Greece | 7.07 | 4.24 | 1.46 |
| 20:00 | 5630 | North Macedonia vs Finland | 2.14 | 3.33 | 3.43 |
| 20:00 | 5925 | Virtus Entella vs Lucchese | 1.84 | 3.20 | 4.70 |
| 20:45 | 5866 | Jong PSV vs Jong Utrecht | 1.65 | 3.95 | 4.44 |
| 21:30 | 4254 | Israel vs Zambia | 1.70 | 3.70 | 4.96 |
| 21:45 | 2453 | Portugal vs Nigeria | 1.26 | 5.65 | 11.10 |
| 22:00 | 2017 | Luxembourg vs Hungary | 5.04 | 3.68 | 1.69 |
| 22:00 | 4489 | Romania vs Italy U20 | 4.40 | 3.90 | 1.70 |
| 22:00 | 5808 | Scotland U21 vs Iceland U21 | 2.28 | 3.55 | 2.85 |
| 22:45 | 2596 | Ireland vs Norway | 2.72 | 3.22 | 2.62 |
| 23:00 | 2046 | Jong AZ Alkmaar vs Jong Ajax | 2.27 | 3.70 | 2.67 |
| 23:00 | 2966 | Swieqi United FC vs Fgura United | 3.00 | 3.40 | 2.27 |
| 23:30 | 4240 | Penafie vs Moreirense | 3.09 | 3.09 | 2.36 |

## IJUMAA - 18/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 03:00 | 2305 | Deportivo Pasto vs America De Cali | 2.67 | 2.86 | 2.67 |
| 03:00 | 5478 | Independiente Medellin vs Rionegro Aguilas | 2.02 | 3.01 | 3.68 |
| 09:00 | 2788 | Nanjing Fengfan vs Shanghai SIPG | 38.67 | 12.57 | 1.01 |
| 09:00 | 4142 | Suzhou Dongwu vs Wuhan Zall | 3.55 | 3.65 | 1.84 |
| 10:30 | 3174 | Dalian Aerbing vs Hangzhou NG | 2.57 | 3.10 | 2.57 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MKWASA ALIA PENALTI YA AZAM

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Boniface Mkwasa, amemnyooshea kidole mwamuzi, Heri Sasi, kuwa penalti aliyotoa ndiyo iliwavunja nguvu wachezaji wake, huku akiongeza kuwa kila kitu alikuwa ameshafanikiwa kwani aliwadhibiti Azam FC.

**Akizungumza baada ya mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Azam FC ikishinda bao 1-0 kwa mkwaju wa penalti ya Idris Mbombo dakika ya 73, Mkwasa alisema dalili za kuonewa zilianza kuonekana mwanzo tu kwenye mechi hiyo.**

"Hii ni mechi ya ugenini, lakini dalili za kuonewa zilionekana tangu mwanzo, imepatikana penalti ambayo sijui ukiiangalia kwenye marudio, lakini imetuvunja nguvu, lakini 'plan' (mpango) yangu ilikuwa imekamilika kwani wapinzani walikuwa wanapata shida sana kufunga kutokana na nilivyokitengeneza kikosi changu. Sijui lakini naona kama kuna tatizo kwenye waamuzi," alisema Mkwasa.

Alisema kwa jinsi timu yake ilivyocheza ilistahili kupata walau pointi moja.

"Tulijua tunacheza ugenini, kwa hiyo tulikuja na 'plan' na kuona tunazuia kwa umakini na kweli, lakini tumekuja kufungwa bao hili ambalo hata sijui kama ilikuwa penalti kweli, siwezi nikasema sana kwa sababu tunaheshimu maamuzi ya refa, lakini kusema kweli imetutoa kwenye mchezo kabisa," alisema kwa masikitiko.

Kocha Mkuu wa Azam FC, Kalimangonga Ongala, alisema timu yake inapata tabu sana kuzifunga timu ambazo zinaingia na mfumo wa kupaki basi.

"Ni kweli hilo nimeliona na niliongea na wachezaji wangu wakati wa mapumziko kuwa tuwe kwenye 'plan' yetu tunapokuwa hatuna mpira, lakini wanapokuwa nao wakati mwingine wawe wanajiongeza hasa kucheza na timu ambazo zinakaa nyuma ya mpira," alisema kocha huyo ambaye ameshinda mechi tano mfululizo tangu aichukue timu hiyo kutoka kwa Mfaransa Denis Lavagne.

Wakati Ruvu Shooting ikiwa imebaki na pointi zake 11 kwenye nafasi ya 13, Azam FC ina pointi 26 kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa mechi 12 ilizocheza.




Mchezaji wa timu ya Kikapu kutoka nchini Marekani, Alysha Clark, akiwaelekeza namna ya kumiliki mpira wasichana chini ya umri wa miaka 18 wakati wa mafunzo yanayotolewa kwa ushirikiano wa Ubalozi wa Marekani katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Banda nje Simba hadi Februari 2023

INATOKA UKURASA 32

akitokea Klabu ya Big Bullets ya Malawi.

Simba kwa siku za karibuni imekuwa ikizalisha majeruhi wengi kwani wakati Banda anaingia kwenye chumba cha majeruhi, Israel Mwenda naye alikuwa akiuguza jeraha lake na sasa amepona, lakini pia Shomari Kapombe naye alirejea uwanjani hivi karibuni, pamoja na Jmmyson Mwanuke ambao wote walishindwa kuitumikia timu hiyo kwa nyakati tofauti kutokana na kuwa majeruhi.

# *Yanga, Singida Big Stars mechi kiwango*

INATOKA UKURASA 32

katika mchezo huo kwa ajili ya kufikia malengo.

Kwa upande wa Singida Big Stars inayonolewa na Kocha Mserbia Hans van Pluijm, amesema wachezaji wake wote waliokuwapo kwenye mipango ya mchezo huo wa leo wako fiti na tayari kuvunja rekodi hiyo Yanga inayotamba kwa sasa.

Pluijm alisema wamejiandaa kushinda mchezo huo na wachezaji wake wana morali kubwa ya kupata matokeo mazuri katika mechi ya leo.

Alisema wanaiheshimu Yanga ila haiwahofii kwa sababu malengo yao ni kupata ushindi katika mchezo huo.

"Mchezo utakuwa mgumu kwa sababu tunahitaji kupata matokeo chanya na Yanga wakitaka kuendelea kulinda rekodi yao, nimewasoma vizuri, ina wachezaji wazuri na ni mabingwa watetezi, lakini wanarekodi yao ya kutofungwa, ninaamini maandalizi ya timu yangu na ubora wa kikosi changu kitaleta ushindani mkubwa.

"Kuhusu kuvunja rekodi ninaimani inawekezana kwa sababu ya maandalizi tunayofanya kuelekea mchezo wetu dhidi ya Yanga," alisema Pluijm.

Michezo
Alhamisi Novemba 17, 2022
Nipashe



Mbappe kumbadili Ronaldo United UKURASA 30

# Yanga SC, Singida Big Stars mechi kiwango leo

## ●●● Pluijm asema wapo fiti na tayari kuivunja rekodi yao ya kutofungwa, lakini...

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu Tanzania Bara itaendelea leo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwa mashabiki kushuhudia moja ya mechi kali na ya viwango wakati mabingwa watetezi, Yanga watakapoikaribisha Singida Big Stars, ambayo imekuwa ikionyesha soka la kuvutia msimu huu.

**Katika mchezo huo utakaopigwa majira ya saa 1:00 usiku, Yanga licha ya kutaka kulinda rekodi yake ya kutopoteza tangu msimu uliopita, lakini itakuwa ikilenga kuibuka na pointi tatu muhimu ili kuishusha Azam kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.**

Azam iliyoshuka dimbani mara 12, ipo kileleni ikiwa na alama 26 huku Simba ambayo ilicheza mechi yake ya 11 jana usiku wakati ikiivaa Namungo FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, kabla ya mchezo huo ilikuwa nafasi ya tatu kwa alama zake 21 na Yanga ya pili kwa pointi 23 zilizotokana na michezo tisa.

Kwa upande wa Singida Big Stars yenye pointi 18 zilizotokana na mechi 10 ilizocheza hadi sasa, ushindi kwao pia ni muhimu ili kuendelea kung'ang'ania nafasi ya nne iliopo.

Hata hivyo, Yanga leo wataendelea kuikosa huduma ya kiungo mshambuliaji, Stephane Aziz Ki, anayetumiki adhabu ya kufungiwa mechi tatu za Ligi Kuu, baada ya Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) kuwakuta na kosa la 'Fair Play' (mchezo wa kiungwana) kwa kukacha kusalimiana na wachezaji wenzao yeye na Clatous Chama wa Simba wakati timu hizo zilipokutana Oktoba 23, mwaka huu.

Nyota mwingine atakayekosekana kwa Yanga ni Shabaan Djuma, Gael Bigirimana na Kipa wao namba moja, Djigui Diarra.

Kuelekea mchezo huo wa leo Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wametumia muda mwingi wa kujiandaa kwa utimamu wa mwili baada ya uchovu wa safari ndevu kutoka Tunisia kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain kutua Dar es Salaam kabla ya kuunganisha Mwanza kwa ajili mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar.

Alisema wapinzani wao wana wachezaji wenye uzoefu, lakini wamejiandaa kupambania pointi tatu huku wakihakikisha wanalinda rekodi ya kutopoteza mechi.

"Tutakuwa na mabadiliko ya kikosi licha ya wachezaji kukosa muda zaidi wa kupumzika, tumejiandaa vizuri tutacheza kwa tahadhari kubwa ili kupata matokeo mazuri na kurejea katika nafasi yetu ya kwanza," alisema Kaze.

Alisema 'Ubeaten' (kutopoteza), haiwapi presha kwenye kupata matokeo katika michezo yao na kuhakikisha wanaendelea kufanya vizuri

INAENDELEA UK. 31



# Banda nje Simba hadi Februari mwakani

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Simba raia wa Malawi, Peter Banda, sasa ni rasmi atakuwa nje ya dimba kwa zaidi ya miezi miwili kutokana na majeraha na anatarajiwa kurejea dimbani Februari mwakani.

Banda ambaye aliingia kipindi cha pili kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Singida Big Stars, akifunga bao la kusawazisha, mechi hiyo ikiisha kwa sare ya bao 1-1 na baadaye kuumia enka, ataanza kuonekana tena wakati Simba ikianza mechi za hatua za makundi Ligi ya Mabingwa Afrika.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema awali ilionekana kama angekaa nje kwa muda wa wiki nne tu, lakini baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kina imeonekana atakuwa nje ya uwanja zaidi ya muda huo.

"Mtakumbuka alitolewa kwenye mechi dhidi ya Singida Big Stars kwa kuumia, na uchunguzi wa awali ilionekana angekaa nje kwa wiki nne, lakini baada ya kufanyiwa vipimo na uchunguzi rasmi, ni kwamba sasa atakaa nje zaidi ya miezi miwili, hivyo makadirio ni kwamba atarejea kikosini Februari kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa.

"Kwa hiyo wanachama na mashabiki wa Simba watambue kuwa hatutokuwa na Banda kwa mwezi huu, Desemba na Januari, hadi Februari ndipo atakaporejea, nadhani mwezi wa kwanza mwishoni ataanza mazoezi na kurejea mwezi huo tunaoutarajia," alisema Ahmed.

Banda alisajiliwa na Simba mwaka 2021 akitokea Sheriff Tiraspol ya Moldovia akiwa anaichezea kwa mkopo

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >